SEHEMU YA KWANZA:

1.0.0 UTANGULIZI:

Suala la huduma ya umeme lina umuhimu mkubwa katika maisha ya kila siku ya mwanadamu. Sote tunafahamu ni kwa kiasi gani Nchi yetu ilivyolipa umuhimu jambo hili, ambapo pamoja na umasikini wetu tulionao lakini Serikali imejitahidi kutandika miundombinu pamoja na mazingira mazuri ambayo yataiwezesha huduma hii kupatikanwa na kila mmoja wetu tena kwa urahisi.

Azma ya Serikali ni nzuri kwa kuamini kwamba, huduma ya umeme kwa wananchi wake si kitu cha anasa kama ambavyo wengine wanavyodhani, bali ni kitu cha lazima kwa kila mmoja wetu kukitumia. Hii ina maana kwamba hatuwezi kuifikisha Nchi yetu kwenye maendeleo bila ya kuifanya nishati hii kuwa ndio kichocheo kikuu na nyenzo ya kuyafikia maendeleo hayo katika ustawi wa jamii yenyewe, lakini pia katika nyanja ya ukuzaji wa uchumi.

Sehemu kubwa ya lengo hili imefikiwa, kwani kwa hivi sasa huduma hii ya umeme imesambaa maeneo mengi ya mijini na vijijini kwa Unguja na Pemba. Leo si ajabu tena vijijini kuwa na umeme na la kufurahisha zaidi ni kwamba, huduma hii ikiwa pia inatumiwa na wale wananchi wenye kipato cha chini.

Katika kufanikisha azma hiyo njema ya Serikali, ndipo Serikali ilipoanzisha Shirika la Umeme limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Nam. 3 ya Mwaka 2006, ili kuweza kusimamia upatikanaji wa huduma hiyo. Pamoja na utoaji huo wa huduma lakini kama Shirika lina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kuwa nalo ni moja kati ya eneo la kuingiza mapato kwa ajili ya kujihudumia wenyewe na kutoa mchango wake kwa Serikali.

1.1.0 Mapato ya Shirika la Umeme:

Kwa maana hiyo iliyoelezwa hapo juu, mapato ya Shirika yanategemea sana malipo ya huduma ambazo Shirika inazitoa kwa wananchi, wakati huo huo na wananchi nao hutegemea mno huduma wanazozipata ziendane na malipo wanayotoa. Vyenginevyo mambo haya mawili yasipoenda sambamba huzusha manung’uniko kwa wananchi wetu ambao ndio walengwa wa huduma hiyo.

Katika hili kuna kutokuridhika kwa wananchi ambapo baadhi yao wanadhani taratibu za kisheria za upatikanaji wa huduma hii hazifatwi. Hali ambayo wengine ama kucheleweshwa kuipata huduma hiyo, jambo ambalo linaleta usumbufu mkubwa au wakati mwengine kulipa malipo makubwa yakitafautiana na wengine, ijapokuwa aina ya huduma hiyo inafanana.

Aidha kwa upande mwengine wananchi kwa kuamini kwamba ZECO ndio Taasisi iliyopewa mamlaka ya kuunga na kuuza umeme hapa Zanzibar kwa mujibu wa Sheria, wanashangaa mno wanapoona kazi hii huwa wakati mwengine inapofanywa na Kampuni nyengine binafsi, hasa kwenye miradi mikubwa kama vile kwenye minara ya simu na baadhi ya hoteli.

Tunapozungumza kuanzishwa kwa Taasisi kwa mfano huo wa Shirika la Umeme hapa Zanzibar, huwa tunategemea pia suala la kupatikana kwa ajira ambazo zitawanufaisha wananchi wetu, ambao bila ya shaka ndio wahusika wakuu wa kuipata neema hiyo. Na kwa sababu ajira ni haki ya kila mwananchi mwenye sifa zinazostahili kuipata, basi ni imani yetu kwamba haki hiyo itakuwa ni mali ya kila mwenye kustahili. Haitakuwa haki ya watu fulani ama kwa uzawa wao, eneo au rangi zao.

Halikadhalika ndani ya ajira yenyewe taratibu za kazi zitakuwa zinafuatwa katika kutimiza majukumu ya kazi, lakini vilevile katika kutoa haki na fursa zilizo sawa kwa wote, hii ni kwa mfano kwenye upatikanaji wa mafunzo ya kazi na upandishaji wa vyeo au madaraja. Lakini jengine kubwa zaidi ni kuthamini kazi yenyewe na utunzaji bora wa mali za Shirika. Taratibu za ununuzi na uondoaji wa mali ziwe ndio muongozo wa uwajibikaji.

Aidha katika kuhakikisha Shirika linawahudumia vyema wananchi, ni lazima lijenge mazingira ya kuwa na huduma endelevu ambayo huwa haikosekani hata kwa wakati wa dharura. Kama tunavyofahamu kwamba huduma hii inapatikana kwa kununuliwa kutoka kwa Shirika la Ugavi wa Umeme, Tanzania (TANESCO), bila ya shaka kuna gharama zake na wakati mwengine ama kwa dharura ya matengenezo au vyenginevyo huduma hii hukosekana kwa muda.

Hali hiyo ama hutokea kwenye mitambo yao au mara nyengine kwenye mitambo yetu, kama ambavyo imetokezea mwaka 2010 kwa kipindi cha karibu miezi mitatu, kisiwa cha Unguja kilipokosa umeme. Hapa ndipo ambapo Shirika linahitaji kutumia umeme wake wa akiba. Kwa vyovyote vile hatuna njia nyengine mbadala isipokuwa kutumia majenereta yetu ya akiba. Ni kwa kiasi gani hayo yanatekelezwa na Shirika ni maswali yanayoulizwa na wananchi na yanataka majibu. Lakini je gharama za kila siku za Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kuilipa TANESCO haiwi kwamba ni mzigo mkubwa wenye kutuelemea! Na kama kuna deni la nyuma ni deni gani hilo lisilokwisha na ivi ni halali kuendelea nalo?.

1.2.0 Chimbuko la Kazi kwa Kamati:

Hayo yaliyoelezwa juu ni miongoni mwa baadhi ya maswali mengi ya wananchi kwa Shirika lao, ambayo kwa kweli yanakuja kutokana na matokeo yaliyo kinyume na matarajio yao. Kwa vile Shirika hili ni la Serikali kwa asilimia mia moja (100%) maana yake ni kwamba, hii ni mali ya walipa kodi wa nchi hii ambao ni wananchi, na wananchi wasemaji wao ni Wawakilishi waliowachagua, hayo ndiyo yaliyomfanya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Kuchaguliwa na Wananchi kupitia Jimbo la Kiwani Mhe. Hija Hassan Hija kwa kutumia haki yake chini ya kanuni za Baraza ya 27(l)(m), 27(3), 48(1) na 49(1) Toleo la 2011, kwenye Mkutano wa Saba wa Baraza la Nane, kuwasilisha hoja binafsi kwa mujibu wa Kanuni ya 117 ya kanuni za Baraza, kwa kulitaka Baraza liridhie kuunda Kamati Teule kwa ajili ya kulichunguza Shirika la Umeme kwa kuangalia maeneo yafuatayo:-

1) Upotevu wa fedha za Shirika unaotokana na uungwaji wa umeme unaofanywa na watendaji wasio waaminifu.

2) Sababu za usumbufu wanaoupata wananchi wakati wa kuomba na baada ya kulipia huduma ya kuungiwa umeme pamoja na suala la bei kubwa wanazopewa ukilinganisha na baadhi ya watu, makampuni, mahoteli, mabenki na makapuni ya minara ya simu za mikononi.

3) Taratibu za ajira katika Shirika zinazodaiwa kuwa za upendeleo Unguja na Pemba.

4) Iwapo mali za Shirika zinauzwa kwa kufuata taratibu za Sheria ya Uuzwaji na Ugavi wa Mali za Serikali na Sheria nyengine.

5) Iwapo upatikanaji wa majenereta 32 yaliyopo Mtoni ulifuata sheria zinazohusika na kwa nini hayatumiwi kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar, na

6) Kiwango cha deni linalodaiwa Zanzibar na TANESCO na iwapo kuna sababu za msingi za kuendelea kuwepo kwa deni hilo na athari zake kwa Maslahi ya Zanzibar.

Maelezo ya Mhe. Hija yalimalizika kwa kutoa Hoja iliyosisitiza haja ya kuundwa kwa Kamati Teule kwa lengo la kufanya kazi hadidu zote alizozieleza na ikabaki kazi ya Baraza la Wawakilishi kuamua juu ya hoja hiyo.

1.3.0 Muundo wa Kamati

Kutokana na umuhimu wa jambo hilo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, akichangia hoja hiyo ya Mhe. Hija, alikubaliana na kuendelea kwa mapambano dhidi ya ubadhirifu ndani ya vyombo vya umma, huku akiunga mkono jitihada zinazofanywa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika mapambano yao dhidi ya ubadhirifu wa mali za Umma na hivyo alipendekeza kuwa, badala ya kuunda Kamati Teule, kazi hiyo ya kufuatilia Hoja Sita alizozieleza Mhe. Hija, zikabidhiwe Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (P.A.C), huku Mhe, Hija akipendekezwa kuwemo katika Kamati hiyo. Hebu na tumnukuu Mhe. Mohammed Aboud Mohammed kama ifuatavyo:

> “Mhe. Spika, kwa kuwa hoja ya Mhe. Hija imeeleza kwa kina kuhusu upotevu wa pesa za Serikali. Mhe. Spika, naomba nipendekeleze kwa Baraza lako Tukufu kumuomba Mhe. Hija Hassan Hija kwamba badala ya kuunda Kamati Teule, basi kwa kuwa Kamati yetu ya P.A.C ina utaalamu mkubwa sana wa kufanya kazi hizi za kutizama upotevu wa fedha za Serikali, pamoja na mali za Serikali. Hivyo, naliomba Baraza lako likubali kwamba

Kamati ya P.A.C ndio ifanye kazi hii, ikimjumuisha na Mhe. Hija Hassan ambaye ana habari nyingi. Naomba kutoa hoja[1]"

Jambo la kusisitiza katika nukuu hiyo ni kwamba, Baraza lilikubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, baada ya Mtoa Hoja (Mhe. Hija Hassan Hija), kukubaliana na pendekezo la Mhe. Waziri, na hivyo ni sawa na kusema kwamba, kazi hii ni maalum kwa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali, ikitofautiana na zile kazi zake za kawaida, lakini ina uzito ule ule wa kazi za Kamati Teule na ripoti yake inatarajiwa pia kubeba maudhui ya Kamati Teule zinazoendelea kuudwa na Baraza la Wawakilishi. Hivyo kwa ujumla Kamati ilikuwa na Wajumbe wafuatao :-

1) Mhe. Omar Ali Shehe — Mwenyekiti
2) Mhe. Fatma Mbarouk Said — Makamo Mwenyekiti
3) Mhe. Abdallah Juma Abdallah — Mjumbe
4) Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) — Mjumbe
5) Mhe. Shadya Mohammed Suleiman — Mjumbe
6) Mhe. Farida Amour Mohammed — Mjumbe
7) Mhe. Mohamed Mbwana Hamad — Mjumbe
8) Mhe. Hija Hassan Hija — Mjumbe
9) Mhe. Shamsi Vuai Nahodha — Mjumbe.

Halikadhalika Kamati ilikuwa na Makatibu wawili ambao ni :-

1) Ndg Amour Mohammed Amour na
2) Ndg Othman Ali Haji.

1.4.0 Hadidu Rejea

Katika kufanya kazi hiyo Kamati ilikuwa inaongozwa na Hadidu Rejea zifuatazo :-

1) Upotevu wa fedha za Shirika unaotokana na uungwaji wa umeme unaofanywa na watendaji wasio waaminifu.

[1] Hansard, Baraza la Wawakilishi, tarehe 12/04/2012.

2) Sababu za usumbufu wanaoupata wananchi wakati wa kuomba na na baada ya kulipia huduma ya kuungiwa umeme pamoja na suala la bei kubwa wanazopewa ukilinganisha na baadhi ya watu, makampuni ya mahoteli, mabenki na makapuni ya minara ya simu za mikononi.
3) Taratibu za ajira katika Shirika zinazodaiwa kuwa za upendeleo Unguja na Pemba.
4) Iwapo mali za Shirika zinauzwa kwa kufuata taratibu za Sheria ya Uuzwaji na Ugavi wa Mali za Serikali na Sheria nyengine.
5) Iwapo upatikanaji wa majenereta 32 yaliyopo Mtoni ulifuata sheria zinazohusika na kwa nini hayatumiwi kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar, na
6) Kiwango cha deni linalodaiwa Zanzibar na TANESCO na iwapo kuna sababu za msingi za kuendelea kuwepo kwa deni hilo na athari zake kwa Maslahi ya Zanzibar.

1.5.0 Utaratibu wa Kazi

Utaratibu uliyotumika katika kuzifanya kazi Hadidu Rejea zilizohusika, Kamati ilifanya majadiliano na Uongozi wa Shirika kuhusiana na hoja mbali mbali; iliamua ni maeneo gani ya kutembelea pale ilipohitajika kufanya hivyo, ambapo kwa kuanzia Kamati ilianza kufanya kazi Kisiwani Pemba. Kuanzia Tarehe 30/04/2012 hadi tarehe 05/05/2012, na kuendelea Unguja kuanzia tarehe 7/05/2012 hadi 11/05/2012 ambapo ni awamu ya mwanzo na baadae kazi ziliendelea kwa awamu tofauti kwa mnasaba wa ruhusa ya Spika, na hatimae zilimalizika tarehe 01/10/2012, wakati Kamati ilipokutana na TANESCO.

Katika kutekeleza majukumu yake, wakati Kamati inapokutana na Uongozi wa Shirika, ilianza kazi zake kwa kujitambulisha kwa wafanyakazi wote wa Shirika kwa kuwa na mikutano nao kwa ujumla wao kwa pande zote mbili, Unguja na Pemba, lakini pia wakati ilipokutana na Uongozi wa Shirika, iliendelea na tabia hii ya kujitambulisha kwa Uongozi, madhumuni ya kazi zake na hatimae kuendelea na kazi.

Katika mikutano hiyo ya wafanyakazi kwa ujumla wao, kuna baadhi ya mambo yaliyojitokeza ambayo yalinasibika na kazi ambayo Kamati iliiendea. Kwa mfano katika mkutano wa wafanyakazi wa Pemba baadhi ya mambo yafuatayo yalijitokeza :-

1. Nafasi za masomo Pemba zinatolewa kwa upendeleo.
2. Ubadhirifu katika suala zima katika Uungwaji wa Umeme.
3. Pesa za likizo kwa wafanyakazi wa Shirika, hutolewa kwa upendelo.
4. Kuna upendeleo katika nafasi ya ajira kwa wafanyakazi wanaoajiriwa kwa muda, kutoajiriwa katika Mikataba ya kudumu ukizingatia kwamba, nafasi za ajira zinapotokezea, Shirika linachagua na kuajiri watu wengine huku likiwaacha wale wenye uzoefu wa kutosha.
5. Kamati imepokea malalamiko ya Vijana waliopeleka malalamiko yao kwenye Tume ya Utumishi Serikalini, kufuatia kutoajiriwa katika Nafasi ya ‘Cashier’ wakati walioajiriwa katika nafasi hiyo hawana sifa na Uajiri wao umefanyika kwa misingi ya upendeleo.
6. Suala la Kampuni ya GECCO kuwatumia baadhi ya wafanyakazi wa Shirika, wakati wa saa za kazi.
7. Hofu ya wafanyakazi na hatma yao kufuatia kusuasua kwa Shirika.
8. Uwepo wa makundi ya wafanyakazi baina ya ‘State Fuel’ na ‘ZECO’.

Halikadhalika na kwa upande wa wafanyakazi wa Unguja ambao walikutana na Kamati Tarehe 7 Mei, 2012 nao walitoa madukuduku yao ambayo yalilenga kwenye maeneo yafuatayo :-

1) Wafanyakazi hao walikuwa na wasiwasi na baadhi ya watendaji wenzao kwamba wanashiriki katika suala zima la uungwaji wa umeme usiofata sheria hasa kwa baadhi ya miradi ya mahoteli ya kitalii.
2) Walitilia mashaka juu ya matumizi makubwa ya Shirika kwa kuingia gharama zisizo za lazima, kwa mfano suala la kukodi gari ya kubebea nguzo za kuwekea umeme hasa baada ya ile iliyokuwa ikitumika kupinduka. Gari hilo lenye Nam. za usajili Z 158 BE, limekodiwa kwa gharama kubwa ambazo zingewezesha kununua nyengine mpya.
3) Waliielezea Kamati kwamba, kuna upendeleo mkubwa katika utoaji wa nafasi za masomo, ambapo kuna baadhi ya wafanyakazi hupewa fursa hiyo

kwa gharama kubwa bila ya kujali nafasi waliyonayo na mafunzo wanayoyasomea, wakati wafanyakazi wengine hawapewi fursa hiyo hata kama mafunzo wanayoomba ndio yanayooendana na aina ya kazi zao na ambayo yanapatikana kwa gharama nafuu.

4) Kuna uhamisho usiofata taratibu na unaoashiria chuki na aina ya sindikizo kwa baadhi ya wafanyakazi.
5) Utata wa ajira hasa kwa baadhi ya watumishi, kwa mfano ajira ya Mhasibu wa Tawi la ZECO Pemba, lakini pia wafanyakazi walionesha wasiwasi wao juu ya ajira za watumishi katika ngazi za Umeneja. Walikuwa wanajiuliza ni kwanini katika ngazi hizo watafutwe watu nje ya Shirika, wakiamini kwamba wenye sifa kama hizo na uwezo wapo kwenye Shirika.
6) Kuna watumishi ambao wana elimu ya kutosha kwa baadhi ya fani lakini Shirika haliwatumii ipasavyo.
7) Hakuna ushirikishwaji kwa wafanyakazi kupitia umoja wao, kiasi cha kupendekezwa kwa Muundo wa Utumishi wa Shirika ambapo chombo cha wafanyakazi hakikushirikishwa.
8) Wafanyakazi walionesha kutoridhika na 'Management' ya Shirika.
9) Kuwepo kwa makundi ya wafanyakazi baina ya 'State Fuel' na ZECO.
10) Shirika hutumia fedha nyingi kwa safari za wakubwa, ambazo hazileti tija kwa Shirika.
11) Wasiwasi juu ya kiwango cha mshahara anaolipwa Mshauri wa Teknolojia (IT Consultant) pamoja na Mkataba wake.
12). Kuna utaratibu usio wa kawaida wa mambo ya manunuzi kama vile vifaa vya matumizi ya Ofisi. Baadhi ya maduka yaliyopewa Tenda ya kuuza vifaa vya umeme hayana sifa. Kuwepo kwa utata na sababu ya kukataliwa kwa nguzo za Kampuni ya SANA lakini pia kuendelea kutumika kinyemela.

Aidha, Kamati ilipata fursa ya kukutana na Wakuu wa Idara mbali mbali wa Shirika kwa nyakati tofauti. Katika kikao hicho, wakuu hao wa Idara walishutumiana ikiwa ni pamoja na Idara moja kuzorotesha maendeleo ya Idara nyengine.

Kamati vilevile katika kuifanya kazi hii ilitumia Picha (kamera) pamoja na kurekodi maneno (Hansard) wakati wa mahojiano na wafanyakazi,

halikadhalika kufanya marejeo kwa baadhi ya nyaraka za Shirika, Sheria mbali mbali pamoja na taarifa nyengine zilizopatikana kupitia Taasisi zilizohusika, ikiwa ni pamoja na Tume ya Utumishi Serikalini, na kupita kwa watu mbali mbali walioitwa na kuwasilisha ushahidi wao kwa Kamati.

SEHEMU YA PILI :
UCHANGANUZI WA HADIDU REJEA ZILIZOKABIDHIWA KWA KAMATI:

HADIDU REJEA NAM. 1 NA NAM.2 :

1. **UPOTEVU WA FEDHA UNAOTOKANA NA UUNGWAJI WA UMEME UNAOFANYWA NA WATENDAJI WASIO WAAMINIFU.**

2. **SABABU ZA USUMBUFU WANAOUPATA WANANCHI WAKATI WA KUOMBA NA BAADA YA KULIPIA HUDUMA YA KUUNGIWA UMEME PAMOJA NA SUALA LA BEI KUBWA WANAZOPEWA UKILINGANISHA NA BAADHI YA WATU, MAKAMPUNI YA MAHOTELI, MABENKI NA MAKAMPUNI YA MINARA YA SIMU ZA MIKONONI.**

2.0.0 Maelezo ya Hadidu Rejea:

Katika kuifanyia kazi hadidu rejea nambari moja ambayo ilihusu Upotevu wa fedha za Shirika unaosababishwa na uungwaji wa umeme unaofanywa na watendaji wasio waaminifu, Kamati iliona ni vyema kazi hii ikaifanya kwa pamoja na hadidu rejea nambari mbili, ambayo ilihusiana na Sababu za usumbufu wanaoupata wananchi wakati wa kuomba na baada ya kulipia huduma ya kuungiwa umeme pamoja na suala la bei kubwa wanazopewa ukilinganisha na makampuni ya minara ya simu za mkononi, mabenki na mahoteli.

Hii ni kwa sababu dhana ya upotevu wa fedha kwa uungwaji wa huduma ya umeme usiofuata taratibu, unaofanywa na baadhi ya watendaji wasio waaminifu

matokeo yake ni kuleta usumbufu kwa wananchi wakati wa kabla na baada ya kuungiwa umeme huo. Aidha, hali hii huwa nafuu sana kwa baadhi ya watu, Makampuni ya Mahoteli, Simu na baadhi ya Makampuni mengine. Ili kupata ufafanuzi wa kina kuhusiana na hadidu hizi zote, ripoti ya Kamati itajikita katika maeneo yafuatayo :

2.1.0 Mapato ya Shirika la Umeme yanayotokana na uungwaji wa umeme:

Kwa mnasaba wa maelezo ya hapo juu, inafahamika wazi kwamba, unapozungumzia mapato ya Shirika, hutaacha kuzungumzia suala zima la utoaji wake wa huduma bora kwa wananchi, huku suala hili huwa chanzo cha mapato mazuri ya Shirika, na kwa vyovyote vile huduma zake za msingi haziishii kwenye uungwaji na uuzaji wa umeme tu, lakini ili mauzo hayo yakamilike ni lazima huduma za malipo ziwe ni endelevu. Bila ya shaka kuzifanya huduma hizo kuwa endelevu maana yake ni kuwa na wateja waliopata huduma hiyo kisheria. Wawe wameomba kwa mujibu wa taratibu na wanalipa kwa utaratibu ule ule uliowekwa kutokana na matumizi yao halisi.

Uungwaji wa umeme huo utakuwa ama kwa kuingiziwa ndani ya majumba yao au sehemu zao za biashara au kwenye maeneo ya uwekezaji au sehemu nyengine yoyote ambayo kisheria inakubalika kuwekwa huduma hiyo. Bila ya shaka katika kutekeleza kazi hii Shirika limejipangia utaratibu wa kufuatwa pamoja na bei kwa ajili ya malipo ya kazi hiyo.

Madhumuni makubwa ya kuweka utaratibu huo, kwanza ni kujua idadi ya wanaotumia huduma hiyo, mahitaji yaliyopo, huduma halisi zilizopo lakini jambo jengine kubwa zaidi ni suala la udhibiti wa mapato yanayotokana na malipo ya matumizi ya huduma hiyo. Shirika pia linaweza kuweka miundombinu yake vizuri katika kuhakikisha kwamba huduma hii inawafika wateja wengi na kwa urahisi, jambo ambalo litaliwezesha Shirika vilevile kukagua na kufanya matengenezo ya miundombinu hiyo kwa pale inapotokezea haja ya kufanya hivyo.

Katika utaratibu mzima unaohusu upangaji wa bei kwa ajili ya kuungiwa umeme, kumekuwa na tafauti ya viwango ambavyo ndivyo vinavyotofautisha malipo hayo. Bei hizo hutafautiana kwa njia mbalimbali; hii hutegemea sana aina ya maombi ya

matumizi ya mteja ambae yeye mwenyewe anakusudia kuutumia. Madhumuni yake hayo ndio yatakayoonesha ni kiwango kipi kitakidhi mahitaji yake. Kwa mfano wale wenye kuhitaji umeme mkubwa (*High Tension*) malipo yao huwa tafauti na wale wenye kuhitaji umeme wa kiasi (*Low Tension*). Tafauti hii pia hutegemea na masafa ya eneo ambalo umeme huo unatarajiwa kuchukuliwa na pale ambapo unahitaji kufikishwa, hii ina maana kwamba kwa ujumla wake huo, hesabu yake inajumuisha pamoja na idadi ya vifaa vitakavyotumika katika kazi hiyo; kama vile nguzo, waya, vikombe, stay n.k **(Kiambatisho Nam 1).** Kwa tafsiri hiyo maana yake ni kwamba wateja wa Shirika wamegawika makundi makuu mawili; kuna Wateja wadogo na Wateja wakubwa.

Kwa msingi huu, endapo utaratibu uliopo utafuatwa na Shirika kwa maana ya Watendaji wake, kama ulivyowekwa, basi Shirika litaingiza mapato kwa kiwango kikubwa, kwani wahitaji wa huduma hii ni wengi na kadiri msukumo wa maendeleo unavyowakumba wananchi wetu, na kwa vile kwa mujibu wa sheria Nam.3 ya 2006 imelipa mamlaka Shirika kuwa ndio muuzaji pekee wa umeme hapa Zanzibar, basi hapana shaka mapato hayo ni ya kudumu kwani hayana eneo jengine yanakokwenda. Kwa lugha nyepesi tunaweza kusema kwamba hii ni biashara isiyo na mpinzani.

2.2.0 Utaratibu wa Kufatwa katika Uungwaji wa umeme:

Kamati ilijulishwa kuwa ili kuhesabiwa kwamba umesajiliwa kihalali kama mteja wa Shirika kuna mambo ya kuzingatia ambayo kama tulivyoeleza mwanzo yatatafautiana kutokana na aina ya matumizi, kimsingi utaratibu ufuatao ndio uliowekwa kwa madhumuni hayo:-

(a) Kwa Wateja Wadogo

- Muombaji anatakiwa awe na Picha mbili ndogo (*Pass Port Size*);
- Awe na barua ya Sheha yenye kuthibitisha ukaazi wake;
- Alipie Fomu ya Usajili (Sh. 8,000/- kwa sasa);
- Ataacha anuani yake au nambari ya simu ili kumuwezesha kuwasiliana na Shirika kirahisi;
- Watendaji wa Shirika watalipima eneo linalotakiwa huduma hiyo;
- Makisio kwa ajili ya malipo ya kazi yatafanywa;

- Mteja ataitwa na kulipa huduma hiyo; na
- Mteja atapatiwa huduma husika.

Ifahamike kwamba (kama tutakavyofafanua hapo baadae), endapo katika kuunganishiwa umeme huo kutahitajika vifaa ambavyo kwa kipindi hicho Shirika halitakuwa navyo, basi mteja ataruhusiwa kununua katika maduka ambayo yamepewa kibali na Shirika kwa madhumuni hayo.

(b) Kwa Wateja wakubwa:

Kwa upande wa Wateja wakubwa, wao wanatakiwa kufuata utaratibu ufuatao :

- Waandike barua ya maombi kwa Meneja Mkuu;
- Watalipia fomu ya maombi (Kwa sasa ni Sh. 12,000/-);
- Eneo husika litapimwa;
- Makisio yanayohusika na malipo yake yatafanywa;
- Hatimae Mteja atatakiwa kulipa ; na
- Mteja atapatiwa huduma aliyoiomba.

Halikadhalika, endapo katika kuunganishwa huko kutahitajika baadhi ya vifaa ambavyo kwa wakati huo Shirika halitakuwa navyo, basi mteja ataruhusiwa kununua mwenyewe kwenye maduka kama yalivyoteuliwa na Shirika, hata hivyo kwa wateja wa aina hii hata kama vifaa hivyo watavitoa nje ya Nchi, basi inaruhusiwa kwani yawezekana mradi wake ni mkubwa au aina ya vifaa anavyovihitaji yeye si rahisi kupatikana Nchini kwa maana ya Zanzibar au Tanzania kwa ujumla, na maduka yenye ruhusa hiyo hayana vifaa hivyo kwa mujibu wa mahitaji ya mteja. Jambo la msingi ni kwa Shirika hulazimika kuvikagua vifaa hivyo na kuridhika kwamba viko katika kiwango kinacho hitajika kwa matumizi ya Zanzibar.

2.3.0 Maduka yaliyopewa Kibali:

Shirika kupitia Bodi yake ya Wakurugenzi limeandaa utaratibu mzuri wa kuyapa maduka au Kampuni za kuweza kuuza vifaa vya umeme na kamwe haikuwa holela kwa kila mmoja kuifanya biashara hii. Maduka yaliyopewa kibali hicho ni Amko

Store, Osaju General Supplier, Mwembeladu Store, SANA Express, Toyota Store, GECCO, Trade Links na M /M General Traders.

Maduka hayo ndiyo ambayo Kamati iliarifiwa kwamba yamepitishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Umeme, katika kikao chake cha 89 kilichofanyika Tarehe 9/07/2008, chini ya Waraka nam. 343 ambapo katika hatua za mwanzo, jumla ya Kampuni 7 zilitimiza masharti yaliyowekwa na Kampuni moja tu ya Amko Store ambayo ilikosa kutimiza vigezo, baada ya kukosekana usajili wa VAT. Hata hivyo iliweza kuwasilisha baadae.

Maduka/Kampuni zote hizo zilikuwa miongoni mwa washiriki 11 waliowasilisha maombi yao kwa Tenda Bodi ya Shirika na kujadiliwa katika kikao chake cha Tarehe 25/3/2008 kabla ya kuwasilishwa kwenye kikao cha Bodi ya Wakurugenzi.

2.4.0 Wateja waliotembelewa na Kamati:

Kamati katika kujiridhisha na kuona ukweli juu ya jambo hili linalohusu upotevu wa mapato ya Shirika katika eneo hili la utoaji wa huduma kwa njia ya uungwaji wa umeme na usumbufu wanaoupata wananchi wakati wa kuomba huduma hiyo, iliamua kufika katika maeneo ambayo huduma hii inapelekwa, yaani walimo Wateja haswa, na ilifanya hivyo ili kuhakikisha kwamba Shirika linazifata kikamilifu taratibu walizojipangia wenyewe, ambazo ndizo zitakazotoa hali halisi ya upatikanaji na udhibiti wa mapato yake. Kamati katika kulifanya kazi hili, iliwakagua baadhi ya Wateja wa Shirika katika Kisiwa cha Pemba na Unguja, na imeona ni vyema kutoa ufafanuzi ufuatao:

2.5.0 Wateja husika:

Kwa mujibu wa Ripoti hii, tunapozungumzia Wateja Wadogo maana yake ni wale watumiaji wa huduma ya umeme wa kawaida (Low Tension), ambao mara nyingi huwa unatumiwa kwenye majumba na sehemu za biashara ndogo ndogo na za kati. Hivyo, tunaanzia na maelezo yanayowahusu wateja hao wadogo walioko Kisiwani Pemba, lakini hata hivyo katika kuiweka sawa taarifa hii kwa upande huo tutakuwa na baadhi ya mifano ya wateja wakubwa.

2.5.1 Yaliyojitokeza

Kwa kutambua tafsiri ya uhalali wa mteja kwamba ni yule aliefuata utaratibu ulioelekezwa ambao unajenga mazingira ya kumtambua kila mmoja, alipo na aina ya huduma anayoipata lakini pia malipo aliyolipa kwa ajili ya huduma hiyo na anayoendelea kulipa wakati akiendelea kuitumia huduma hiyo, basi ni dhahir kwamba, anayekwenda kinyume na hivyo, maana yake ni kupoteza uaminifu wake kwa kutenda kosa hilo lakini pia anasababisha upotevu wa fedha nyingi kwa Shirika, kwani kwa kutokufuata taratibu hizo ndiko kunakosababisha kutokuwa na usahihi wa kujua idadi halisi ya wateja na hivyo kulifanya Shirika kutoa huduma kubwa kwa malipo yasiyolingana na huduma yenyewe.

Kwa vile utendaji wa makosa hayo kamwe hautokamilika bila ya uwepo wa ushiriki wa baadhi ya watendaji wa Shirika, kwa maana hiyo ni dhahir kusema kwa lugha nyepesi kwamba, Shirika lina baadhi ya wafanyakazi wasio waaminifu ambao wanalisababishia kupoteza mapato yake kwa kiasi kikubwa.

Kutokana na ukweli huo, Kamati imebaini kwamba kuna baadhi ya Wateja kwa kushirikiana na baadhi ya Watumishi wa Shirika hawafati taratibu katika upatikanaji na utumiaji wa huduma hiyo ya umeme, jambo ambalo ndilo linalosababisha upotevu mkubwa unaotokana na eneo hilo la mapato ambapo kuna mambo yafuatayo yamebainika kujitokeza:-

(a) Kuna tofauti ya malipo kwa kazi inayofanana, au wakati mwengine kazi kubwa kuwa na malipo madogo.
(b) Malipo halisi wanayolipa wateja kwa kazi hiyo ya kuungiwa umeme, hutofautiana na thamani iliyopo kwenye risiti wanazoandikiwa.
(c) Kuwepo kwa upendeleo unaosababishwa na baadhi ya Watendaji wa Shirika katika kuunga au kutoa huduma za umeme kunakosababisha Wateja kuchelewa kuipata huduma hiyo ama huwapelekea Wateja hao kukata tamaa na kuwajengea mazingira ya kutoa rushwa.
(d) Kuna Malipo yanayolipwa na baadhi ya Wateja bila ya kupewa risiti kabisa.
(e) Kazi kubwa ya kuunga umeme kwenye minara ya simu za mkononi kupewa Kampuni binafsi badala Shirika kuifanya kazi hiyo mwenyewe.

(f) Baadhi ya Wateja kutumia huduma hii bila ya kusajiliwa na hivyo kutumia umeme bure. (Hawamo katika orodha ya Wateja wa Shirika).

2.5.2 Ufafanuzi :

Baada ya kutaja maeneo yaliyobainika na Kamati kwa udhaifu wake mbali mbali, sasa ni vyema tukapata ufafanuzi wa maeneo hayo kama ifuatavyo :

(a) Tofauti ya malipo kwa kazi inayofanana, au wakati mwengine kazi kubwa kuwa na malipo madogo.

Katika suala hili Kamati kwanza imefanya ziara ya kuwakagua wateja wadogo wa Shirika waliyoko Pemba, kwa utaratibu wa kupita nyumba hadi nyumba kwa mujibu wa sampuli iliyojipangia kama tulivyoeleza mwanzo, na katika kufanya kazi hiyo mifano ifuatayo imepatikana:-

- Kuna Nyumba ya Bw. Juma Moh'd Dadi wa Chokocho ameunganishiwa umeme kwa masafa ya nguzo moja na 'Roof poll' moja ambapo vifaa vyote ni vya Shirika, ameunganishiwa Tarehe 22/2/2012 akiwa amelipia huduma hiyo kwa Sh. 442,593/-, wakati Bibi Zuhura Nassir Nassor wa Ngezi na yeye ameungiwa kwa hiyo hiyo nguzo moja na 'Roof Poll' moja kama alivyofanyiwa mwenzake, ametozwa jumla ya Sh.1,236,747.02 siku ya Tarehe 7/2/2012. Kazi hiyo imefanyika kwa mwezi huo huo mmoja. Halikadhalika nae Bibi Asha Ali Omar wa Madungu mwenye nguzo moja na Roof poll moja malipo yake ni Sh.442,593.22 ya Tarehe 2/3/2011. Kazi iliyofanyika mwezi mmoja tu baadae.

- Bw. Ussi Moh'd wa Michenzani yeye ameunganishiwa umeme kwa nguzo mbili na 'Roof poll' moja kwa Sh.194,000/- Tarehe 6/10/2008 wakati Ndg. Hamad Abdallah wa Matangatuani (Kifundi), ameungiwa kwa nguzo mbili na 'Roof poll' moja na malipo yake ni Sh.537,750/- kupitia risiti ya Tarehe 1/11/2011. Wakati Ndg.Khamis Ali Makame wa Tundauwa mwenye Akaunti namba DO 04015, ameungiwa umeme kwa kutumia nguzo mbili

za Shirika kwa gharama ya Tsh. 506,824.16 zilizolipwa kwa risiti nambari 00000866800 ya Tarehe 31/01/2011.

(b) Malipo wanayolipa Wateja kwa kazi ambapo hutofautiana na thamani ya malipo yaliyomo kwenye risiti zinazotolewa.

Kamati ilifanya mahojiano na baadhi ya Wateja wa Shirika ambao walilalamika juu ya kupewa risiti hizo zenye tofauti na bei, ijapokuwa wengine hawakujali kufanyiwa hivyo kwani kwao wao walichokitaka ni kuipata hiyo huduma ya umeme tu, bila ya kujali kupata huko ni kwa njia au ni kwa gharama gani.

Mifano ya Wateja waliopata kadhia hiyo ni:

- Bw. Moh'd Habibu Suleiman wa Kigongo (Wambaa) ameungiwa umeme kwa masafa ya nguzo kumi na mbili na amethibitisha mbele ya Kamati kwamba amelipa Shilingi Milioni nane (8,000,000/-), wakati risiti aliyopewa na Shirika ni yenye thamani ya Sh.167,320/- tu**.**

- Mteja mwengine Ndg. Khamis Makame wa Tundauwa, Pemba, mwenye Akaunti Namba DO04015, ameungiwa umeme kwa kutumia nguzo mbili za Shirika, kwa gharama za Tsh. 506,824.16/- zilizolipwa kwa risiti namba 00000866800 ya tarehe 31/01/2011 na kiwango alicholipa kina utata, kwani kinaonekana ni kidogo kuliko uhalisia wa kazi yenyewe ilivyo (Angalia Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani wa Shirika ya Januari-Machi, 2012**,** ambayo ni **Kiambatanisho Nam 2)**

- Pemba Misali (Bw. Amani Ibrahim Makungu) mwenye Akaunti Namba, Ac. D O 03220 ameungiwa umeme mkubwa *(Three Phase)* kwa masafa ya nguzo kumi na nne. Risiti ya malipo yake ni jumla ya Sh. 2,052,696/- ya Tarehe 19/5/2010 (005100519000034) na kwenye faili lake kuna risiti iliyoonesha kununuliwa kwa nguzo kumi na nne kutoka kwa mfanyabiashara mwenye jina la MOHD & BASHIR (TIN No. 105-251-777) ya Tarehe hiyo hiyo 19/5/2010 yenye nambari

000161 ikionesha thamani ya jumla ya Sh.1,680,000/-. **(Kiambatanisho Nam 3).**

(i) Maelezo ya Ziada

Katika faili la Mteja huyu (Bw. Ibrahim A. Makungu) kuna barua ya Tarehe 12/5/2010 yenye kumbukumbu nam. ZECOP/P/T/Vol. I/28 aliyopelekewa Bw. Amani Ibrahim Makungu wa Mkanjuni, Chake Chake, Pemba ikimuarifu juu ya makisio kwa ajili ya kuungiwa umeme katika Hoteli yake iliyopo Wesha Kwa Mfaki. Barua ambayo ilikuwa ni majibu ya barua ya Ndg Amani I. Makungu ya Tarehe 28/4/2010, ijapokuwa barua hiyo inayozungumzwa kuwa ni ya maombi haikuweza kuonekanwa na Kamati, kwa vile haikuwemo katika faili la Mteja na wala haikuonekana katika faili jengine au pahala pengine popote.

Hata hao watendaji wa Shirika nao wameitafuta bila ya mafanikio na hatimae Kamati ikakubaliana kwamba, barua hiyo haikuwapo isipokuwa kilichokuwepo ni kubuni katika kuhalalisha maombi hayo.

Pamoja na mambo mengine barua hiyo inayodaiwa eti imeijibu barua ya maombi ya mteja huyo, ya ZECO kwa mteja huyu imesisitiza malipo hayo ya Sh. 2,052,696/- kufanyika kwa Shirika la Umeme Afisi Kuu Pemba kwa ajili ya ujenzi wa Line na nguvu kazi tu, kama ambavyo fomu ya makisio ya kazi hiyo inavyoonekana **(Kiambatisho Nam 4).**

(ii) Malipo aliyoyafanya

Kamati ilibaini kwamba Ndg. Amani Ibrahim Makungu alituma fedha kwa ajili ya kazi yake hiyo, kwa kufuata maelekezo mengine kabisa aliyoyapata na si kwa ile barua anayodaiwa kupelekewa na ZECO ya Tarehe 28/4/2010. Jambo hilo ndilo lililoishangaza Kamati, kwamba barua ya Tarehe 28/4/2010 imeagiza kuwa malipo yake mteja huyu ayalipe Shirika la Umeme, Tawi la Pemba (Sh. 2,052,696/-) lakini cha ajabu kumbe kulikuwa na maelekezo mengine ambayo inaonekana hayakuwa ya maandishi na ndio maana Kamati haikuweza kuyaona . Kwa bahati maelezo hayo mengine nje ya barua hiyo, ndiyo ambayo Ndg. Amani Ibrahim Makungu aliyoyafata katika kufanya malipo hayo ya uungwaji wa umeme wake huo.

Maelekezo hayo ni kwamba, gharama ya kazi yake ni jumla ya Sh.37,720,000/- (na sio 2,052,696/- aliyoelekezwa rasmi na Shirika), na hivyo fedha hizo za malipo aziingize kwenye Akaunti ya mtu binafsi na si kwenye Shirika, tena mtu ambae ni mfanyakazi wa Shirika anayeshughulika na kufanya kazi ya makisio ya wateja na hata hayo makisio yake yeye ndie aliyekuwa muhusika. Nambari ya akaunti aliyopewa ni yenye kusomeka 2022500868 ikiwa inamilikwa na Ndg. Zakia Juma Azan iliyopo kwenye National Microfinance Bank (NMB) Tawi la Pemba. Nae Ndg. Amani Ibrahim aliziingiza fedha hizo kwa utaratibu ufuatao, ambao pia unathibitika katika **Kiambatanisho Nam 5** cha ripoti hii:

- Tarehe 17/5/2010 aliziingiza jumla ya Sh. 30,000,000/-
- Tarehe 28/7/2010 aliziingiza jumla ya Sh. 2,220,000/-
- Tarehe 23/8/2010 aliingiza jumla ya Sh. 1,600,000/-
- Tarehe 30/8/2010 aliingiza jumla ya Sh. 1,670,000/-
- Tarehe 1/9/2010 aliingiza jumla ya Sh. 2,430,000/-

Jumla kuu Sh. 37,720,000/-

Hata hivyo pamoja na utumaji huo wa fedha; ieleweke tu kwamba malipo yaliyoonekana katika faili la mteja huyu ni ya Sh. 2,052,696/- tu ambayo yameambatanishwa na risiti ya malipo ya nguzo zilizotumika kwa ajili ya kazi hiyo ambayo yana jumla ya Sh. 1,680,000/- zilizolipwa kwa risiti yenye kuonesha jina la MOHD & BASHIR, duka ambalo hata halimo katika orodha wa maduka/kampuni yaliyopewa kibali na Shirika cha kuuzia na kusambaza vifaa vya umeme zikiwemo hizo nguzo, na kwa kuwa kazi hiyo imefanyika bila ya kuonesha ushahidi mwengine wa manunuzi ya vifaa vyengine, maana yake ni kwamba, vifaa hivyo vilivyotumika ni vya Shirika na hasa ikizingatiwa kwamba muhusika hakuweza kupewa risiti nyengine ya matumizi yake halisi aliyoyafanya katika kuungiwa umeme huo na wala katika faili lake hakukuwa na risiti nyengine zenye kuonesha matumizi aliyoyafanya kwa ajili ya vifaa vyengine, ukiachia mbali hizo nguzo na gharama za kuungiwa kama zilivyooneshwa katika moja ya fomu ya makisio.

Katika kadhia hii, Kamati iligundua kwamba si tu kwamba kulikuwa na makisio madogo ambayo Mteja huyu alifanyiwa lakini kuna mambo mengine yaliyojitokeza. Kwanza ni kwamba kumbe kulikuwa na Fomu mbili za makisio. Fomu moja ilikuwa na jumla ya Tsh. 19,009,696/- na hayo makisio mengine madogo ndiyo yenye thamani ya Tsh. 2,052,696/- , makisio yote hayo yamefanyika Tarehe 13/5/2010. Jengine ni kwamba, kuna kudaiwa kulipwa kwa fedha hizo (Tsh. 2,052,696/- za makisio ya kazi yenyewe na Tsh. 1,680,000/- kwa ajili ya ununuzi wa nguzo), jambo ambalo si sahihi lakini pia ni namna ya malipo hayo mengine yalivyofanyika. Utata mwengine ni kuwa barua ya kudai malipo iliandikwa Tarehe 12/5/2010 wakati fomu za makisio hayo imetayarishwa tarehe 13/5/2010. Kamati ilikuwa na maswali mengi yaliyokosa majibu, na mojawapo ni kwanini barua ya kumjulisha juu ya malipo kutokana na makisio iwe mwanzo kabla ya makisio yenyewe hayajafanywa, lakini jambo jengine, iweje fedha za malipo hayo ya umeme aliyotakiwa kulipa yawe kinyume na yale yanayodaiwa kuwa ni makisio, na iweje malipo hayo yaingizwe kwenye akaunti ya mtu binafsi tena ni mfanyakazi wa Shirika anayehusika na utengenezaji wa makisio ya malipo ya wateja! Swali jengine ni kwanini mteja mmoja na eneo moja la mahitaji atengenezewe fomu mbili zenye makisio tafauti.

Lakini kama hayo hayatoshi wakati wa mahojiano na wafanyakazi hasa wale mafundi walioshughulika na uingizaji wa umeme wa mteja huyu, imedhihirika wazi kwamba, vifaa walivyotumia waliagizwa kuchukua kwenye ghala ya Shirika na bila ya wao kujua mambo mengine yaliyojitokeza kama hayo ya malipo tuliyoyaeleza kwenye ripoti hii. Maelezo hayo yalitolewa na Fundi Salum Saad Khamis (Fundi Sadi) na wakati huo huo mfanyakazi aliyeingiziwa fedha hizo kwenye Akaunti binafsi Ndg. Zakia Juma Azan, alikiri kupokea fedha hizo na kudai kwamba alizitumia kwa madhumuni hayo ya uungwaji wa umeme.

Ijapokuwa hakuweza kuijibu Kamati ni kwanini fedha hizo zisiingizwe kwenye akaunti za Shirika na itumike ya kwake yeye. Wakati kuna barua inayohimiza kwamba malipo hayo yafanyike kupitia Afisi Kuu ya Shirika la Umeme Pemba. Aidha alishindwa kuithibitishia Kamati uhusiano uliopo kati yake na Mteja huyu zaidi ya kuwa yeye ni Mteja sawa na wateja wengine wa Shirika. Jambo ambalo labda lingekuwa na angalau hoja ya yeye kuweza kuwa msimamizi wa kazi hiyo.

Lakini vile vile kama kweli fedha hizo zote Nd. Zakia amezitumia kwa matumizi ya huduma hiyo ya kuunga basi mbona hakuna ushahidi wa matumizi ya fedha hizo kwenye Shirika?

Sasa unapoendelea kupinga kwamba, Shirika halipotezi mapato yake kutokana na baadhi ya wafanyakazi wake kukosa uaminifu, unakusudia nini wakati ushahidi huu unamfanya kila muungwana kukiri kwamba, pamoja na mambo mengine, kamwe Shirika hili halitaweza kujiendesha kwa faida na ufanisi wa huduma wanazozihitaji wananchi wa nchi hii, zitaendelea kuwa ndoto zilizokosa kalima!. Hebu fikiria, huyu ni mteja mmoja tu, kati ya wateja wengi wa Shirika hili anaeungiwa umeme bila ya taratibu za kisheria, huku fedha za malipo zikiingia katika Akaunti ya mfanyakazi binafsi wa Shirika. Kama alitakiwa kwa mujibu wa makisio halisi ya umeme, kulipa hizo Tsh. 37,720,000/- zilizoingia mkononi mwa Ndg Zakia, na hatimae kalipa Tsh. 2,052,696/-tu kwenye Shirika, ni wazi kwamba, Mfanyakazi huyu amenufaika kwa fedha za Umma Tsh.35,667,304/- na katika wateja 100 tu wanaoungiwa umeme kwa utaratibu huu, ni wazi kwamba Shirika hupoteza Tsh. 3,566,730,400/-, fedha ambazo ni nyingi na zingelisaidia zaidi ya Bajeti za Wizara 2 za Serikali hii tukufu, ya Mapinduzi ya Zanzibar! Tunaamini kwamba hili haliwezi kufanywa na kukamilika kwa kusimamiwa na mtu mmoja. Hapana shaka kuna mtandao mkubwa.

- Mfano wa Mteja mwengine ambao Kamati iliupata ni wa NMB Bank Chake Chake (Munawar House) ambae nae aliungiwa umeme huo uliotoka Posta Madungu kwa masafa ya nguzo kumi na moja (11) Ukiwa na waya wa 50mm ‘bunch cable’ na malipo yake yalikuwa ni Sh. 3,718,903.58 risiti ya Tarehe 18/11/2010 (Nam. 011101018000141 inahusika na katika ripoti hii ni **Kiambatanisho Nam 6**), wakati katika makisio ya gharama hizo yaliyofanywa Tarehe 13/10/2010 yalionesha aina na wingi wa vifaa vilivyotumika pamoja na bei zake, ikiwa ni pamoja na nguvukazi iliyotumika *(Labour Charge*) usafiri, malipo ya kodi ya thamani (VAT) na gharama za kiutawala (6%). Hata hivyo baadhi ya vifaa vilivyotumika havikuoneshwa bei zake na Kamati ilitaka kujua hasa ikizingatiwa kwamba vifaa hivyo vilitoka kwenye Ghala ya Shirika. Pamoja na kwamba kulikuwa na maelezo yasiyothibitishwa kwamba Mteja huyu vifaa hivyo alivinunua

mwenyewe na kuwekewa kwenye Ghala la Shirika, hakukuwa na ushahidi wowote wa kuitetea hoja hiyo kwani hata kitabu cha kupokelea vifaa hivyo hakioneshi ile karatasi ya kupokelea vifaa kwenye Ghala (*Delivery Note*), wala hakukuwa na risiti ya ununuzi wake iliyoonekana. Wakati wateja wengine wakinunua vifaa vyao kumbukumbu ya ununuzi huo (Risiti) huhifadhiwa kwenye faili lake.

Aidha idadi ya nguzo zilizoainishwa katika fomu ya malipo hayo ni tatu tu, moja ikiwa na urefu wa mita 11 na nyengine mbili zenye urefu wa mita tisa kila moja. Wakati katika uhalisia ni kwamba, idadi ya nguzo zilizotumika ni kumi na moja. Kamati ilibaini hilo wakati ilipofika katika eneo husika. Lakini hili pia linathibitishwa na hata akili ya kawaida tu ya binaadamu, kwani haiwezekani kabisa urefu wa waya wa mita 2,016 uungwe kwa nguzo tatu tu!. Au hivi ni kweli eneo lenye masafa ya mita 480 liungwe umeme kwa nguzo tatu tu!.

Hata hivyo, Kamati ilipata nakala nyengine ya makisio ya kuungiwa umeme kwa Mteja huyu ya tarehe 1/9/2010 ambayo ina thamani ya Sh. 14,889,047. Hapa kwa mara nyengine tena Kamati ilipata utata na kujiuliza ni kwanini Shirika lifanye makisio hayo mara mbili kwa Mteja mmoja. (Inashangaza kuona kwamba fomu yenye makisio makubwa huwa haiwekwi saini na aliyeitayarisha.) Hata hivyo, kilichoonekana na Kamati ni kwamba, tafauti inayowekwa baina ya makisio hayo mawili huwa ni kubwa mno, kwa mfano wa fomu hii kuna tafauti ya Sh. 11,170,146.42/-, ukilinganisha na yale makisio ya mwanzo ya Sh. 3,718,903.58.

Vifaa vyenye utata na ambavyo ununuzi wake haukuthibitishwa mbele ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

- U/G Cable 35mm wenye urefu wa mita 15 ambapo bei yake ni Sh. 18,000 kwa mita na kwa maana hiyo kutokana na urefu huo thamani yake ni Sh. 270,000/-
- PVC –Al-Wire1x100mm wenye urefu wa mita 2,016 ukiwa na bei ya Sh.1,800/- kwa mita na thamani yake halisi ni Sh.3,628,800/-
- Nguzo nane nazo zenye thamani ya Sh. 1,420,000/- ambapo kwa kila nguzo moja ina thamani ya Sh.165,000/- ikiwa na urefu wa mita tisa.

(Kiambatisho Nam 7)

Kwa ujumla, thamani ya vifaa vinavyodaiwa kwamba vimenunuliwa na Mteja mwenyewe, jambo ambalo halikutolewa ushahidi wa maandishi yoyote isipokuwa maelezo ya mdomo tu kutoka kwa Watendaji wa Shirika, vina thamani ya jumla ya Sh.5,518,800/- ukiyatoa makisio yenye kutoa tafauti ya makisio ya mara ya pili (Sh.11,170,146.42) bado kuna bakaa ya Sh. 5,851,346.42, kwa maana hiyo Kamati imepata mashaka kwamba wakati mwengine Watendaji wa Shirika huyatengeneza mazingira yenye kuonesha makisio makubwa kwa makusudi, ili Mteja atishike na hatimae wamfanyie makisio mengine madogo ambayo huambatana na hujuma ya mapato ya Shirika kama ambavyo yameonekana katika mfano huu.

Na hili pia huwa sehemu kubwa ya usumbufu kwa wananchi wanaohitaji kupatiwa huduma ya umeme, huku hujuma hizo zinapofanyika, wanaonufaika ni wafanyakazi wachache wa Shirika, lakini kwa nini Shirika lisichukue hatua dhidi yao ? Ni suala ambalo linatafsiri nyingi, ikiwa ni pamoja na njama na hujuma hizi pia huwahusisha watendaji wakuu wa Shirika.

- Mteja mwengine ni Bw. Nassor Omar Abdalla wa Mgogoni – Mpakani ambae nae amelipa gharama za nguzo moja kwa thamani ya Shs. 150,000/-, waya kwa thamani ya shs. 280,000/- gharama za kuungiwa umeme shs. 442,595/- na shs. 8,000/- ikiwa ni gharama za fomu ya maombi jumla ya malipo hayo aliyofanya ni Shs. 880,593/- wakati risiti alizopewa ni mbili, No. 28388 ya tarehe 19/4/2012 yenye kuonesha malipo ya shs. 442,593/- kama gharama za kuungiwa umeme na risiti No. 27043 yenye kuonesha malipo ya shs. 8,000/- ikiwa ni gharama za fomu za maombi. Kwa mahesabu hiyo maana yake ni kwamba, jumla ya Shs. 430,000/- zilizobakia zikiwa ni gharama za nguzo na waya hazikutolewa risiti zake. Nguzo hiyo na waya huo ni mali ya Shirika !.

- Aidha Bw. Hemed Suleiman wa Konde nae amewekewa huduma hiyo ya umeme kwenye msikiti wa Msuka Mchikichini kwa kuunganishwa kwa nguzo saba. Kwa kazi hiyo alikiri kutoa shs. 3,000,000/- lakini risiti aliyopewa na Shirika ni shs. 213,000/-.

- Wakati mteja mwengine Bw. Nassor Hamad Fadhil wa Msuka Mchikichini, alilipia nguzo tatu kwa jumla ya shs. 390,000/-. Akalipa tena Sh. 1,780,000/- (Laki tano mara mbili hatimae Sh. 780,000/-) risiti aliyopewa na Shirika inaonesha thamani ya malipo ya Sh. 221,553/-. Hata hivyo baada ya kadhia yote hiyo umeme alicheleweshwa mno kuungiwa na laiti asingechukua hatua ya kutumia nguvu ya kudai chake, akitumia maneno yaliyoashiria kwamba asipoungiwa umeme huo aibu kubwa ingetoka nje, basi ni dhahir hata kwa kulanguliwa huko alikofanyiwa, asingeliupata umeme huo hadi leo.

- Nae Bw. Rashid Mbarouk wa Pandani ambae pamoja na kulipa Sh.442,593/- ambazo zilikuwa ni gharama za kuungiwa umeme tu, lakini alitoa fedha nyengine zaidi ambazo ni shs 500,000/- ikiwa ni madai ya nauli za mafundi waliyomuungia. Fedha hizo zilizodaiwa kuwa ni nauli za watumishi wa Shirika hazikuwa na risiti, dai ambalo lilidaiwa kwa nguvu kubwa na hatimae Mteja ambae ni mhitaji alizitoa. Madai haya ya Mteja yalitolewa mbele ya Kamati na Uongozi wa Shirika ukishuhudia, bila ya kupinga chochote.

- Katika mazingira hayahaya, Baobab Beach Bungalows/ Mr. Misali Kamati haikuweza kupata kitu chengine chochote zaidi ya risiti ya malipo yenye kuonesha malipo ya Sh. 2,164,050/- ikiwa ni kwa kazi ya kuunga umeme tu kwa madai ya kuwa vifaa ni vyake mwenyewe, lakini Kamati haikuweza kupata ushahidi wowote juu ya hilo zaidi ya barua ya mhusika yenye kutaja tu baadhi yake kama vile Transformers, H.T Poles, Cross Arms n.k. Kamati haikuweza kupata risiti za manunuzi yake wala vielelezo vyovyote vilivyonesha kuingia na kutoka kwa mali kwenye ghala **(Kiambatanisho Nam 8)**

- Kamati ilipata utata kwa mteja mwengine anayejulikana kama Mnarani Kigomasha wa Makangale, mwenye nambari ya akaunti DO 02748, ambaye utaratibu wake wa kufanyiwa makisio ulikuwa kama ifutavyo:-

  - Tarehe 30/10/2009 mteja huyu, Mnarani Kigomasha aliarifiwa kwa barua yenye nam. ZECOP/P/T/VOL/06 kwamba makisio yake yaliyohusiana na

maombi ya kuungiwa kwa umeme kwenye eneo lake (maombi aliyoyaomba kwa barua ya Tarehe 23/9/2009 yenye kumbukumbu nam. ZHL/ZECO/MK/10/09) kwamba yamekubaliwa na alitakiwa kwenda kulipa jumla ya Sh. 1,387,836/- ikwa ni jumla ya gharama zote zikiwa na mchanganuo wa High Tension Line Sh. 486,948/-, Transformer Station Cost Sh. 415,800/- na Low Voltage Sh. 485,088/-. Mteja huyu alilipa gharama hizo kwa Shirika kwa risiti nam. 005091102000313 ya Tarehe 2/11/2009. (Makisio haya yalifanywa na Ndg. A.S.Yussuf) **(Kiambatanisho Nam 9)**

- Tarehe 13/9/2010 alifanyiwa makisio na Ndg. Zakia Juma Azzan ya jumla ya 1,303,333.60.

- Tarehe 14/9/2010 Ndg. Zakia Juma Azzan aliyatengeneza makisio kwa kulinganisha baina ya makisio aliyoyaita ya nyuma (*Previous Estimate*) na makisio ya sasa aliyoyaita kama (*Current Estimate*) mlinganisho huo ulikuwa ni:

	Previous Estimate	***Current Estimate***
Tansformer Installation	415,800.00	415,800.00
Construction Of l. V. Line	485,088.00	485,800.00
Construction Of H.T. Line	486,948.00	1,303,333.60
TOTAL	**1,387,836.00**	**2,205,221.60**

Alimuwekea tafauti ya makisio hayo ambayo ni Sh. 817,385/-. Hesabu inapatikana kwa kutoa yale ya makisio ya sasa dhidi yale ya zamani **(Kiambatisho Nam 10)**

Kamati ilikuwa na maswala mengi ya kuuliza juu ya hilo lakini majibu yakakosekana. Utata wenyewe ni kwamba; kwanza kwanini makisio hayo ya mteja mmoja yafanywe mara mbili tena kwa wakati tafauti uliopishana kwa mwaka mzima. Kipi kilichozidi hasa kwa kuzingatia kwamba alipotakiwa kulipa tu

alifanya hivyo. Lakini hii tafauti ya Sh. 817,385.60 ililipwa? Jawabu likawa rahisi kwani hakuna risiti iliyoonesha malipo hayo maana yake haikulipwa. Sasa kuna haja gani ya kuoneshwa kuwa ni malipo halali anayodaiwa Mteja huyo!

Wasiwasi mwengine wa Kamati ni juu ya vifaa vilivyooneshwa kwenye fomu ya makisio kuwa ni vya mteja mwenyewe. Kama kawaida, hakuna ushahidi wa kuthibitisha hilo zaidi ya maneno ya mdomo tu yaliyotolewa na watendaji wa Shirika. Kwani ilipaswa vifaa hivyo vioneshe maduka vilivyonunuliwa.

c) Kuwepo kwa upendeleo unaosababishwa na watendaji wa Shirika katika kuunga au kutoa huduma za umeme kunakosababisha wateja ama kukata tamaa au kuwajengea mazingira ya kutoa rushwa.

Kuwepo kwa upendeleo huo husababisha Shirika kupoteza au kukosa mapato kwani idadi ya wateja haiongezeki kwa kasi halisi kwani baadhi yao wanakaa muda mrefu bila ya kupata huduma, lakini wengine wanakuwa wazito kuomba huduma hiyo kutokana na kuona usumbufu wanaoupata wenzao. Wanapoamua basi hujilazimisha kutoa chochote ili waepukane na usumbufu huo. Kwa mnasaba huo na wale ambao huomba na kukamilisha taratibu za kisheria na kukaa tu huku wakisubiri majaaliwa ya Shirika maana yake ni kwamba, kwa muda wote huo wa kusubiri ambao walikuwa tayari wawe wateja wa Shirika, hufanya Shirika hili kuwa limejipotezea mapato yake kwa makusudi kama wao wanavyowakosesha huduma wananchi hao.

Kamati ingeridhika kama ingekuwa uchelewashaji huu una sababu maalum kama vile upungufu wa vifaa, hali ya hewa au miundombinu, lakini imebaini kwamba wala hakukuwa na sababu za msingi zinazopelekea matokeo hayo. Maana yake ni kwamba hayo hutokea kwa utashi tu. Kwa lugha nyepesi ni kusema kwamba hili hufanywa kwa makusudi.

Mfano wa ucheleweshwaji huo ni:-

- Bw. Salum Makame Juma wa Mgagadu amejaza fomu na kulipa gharama zote zilizohitajika ambazo ni Sh. 554,729/- kwa risiti ya Tarehe 30/12/2011. Hadi Kamati inamtembelea Tarehe 3/5/2012 alikuwa hajapatiwa huduma hiyo, wakati Bw. Rashid Mbarouk Rashid wa Pandani mwenye mita No. 07101423916, ameomba Tarehe 18/1/2012 na kupatiwa huduma hiyo tarehe

23/1/2012 (Ndani ya siku tano) akiwa amelipia Sh. 442,593/- tena malipo aliyafanya Tarehe 24/1/2012. Yaani hata hayo malipo ya kuungiwa umeme huo, ameyafanya siku moja baada ya kupewa huduma hiyo. Mazingira hayo yamedhihirisha wazi kwamba Ndg. Salum Makame amecheleweshwa kwa makusudi.

Kamati ilishangaa sana kuona kwamba Ndg. Salum ameomba kupatiwa huduma hiyo mwanzo (Mwishoni mwa mwezi Disemba, 2011) wakati Ndg. Rashid ameomba mwisho (Mwishoni mwa Mwezi Januari, 2012) kukiwa na tafauti ya mwezi mmoja tu, lakini alieomba mwisho amepata kabla ya wiki kwisha na yule wa mwanzo miezi mitano imepita hajapatiwa huduma hiyo.

Hivi kwanini tusiseme kwamba huduma hiyo inatolewa kwa upendeleo? Na kwa mazingira haya ni kiasi gani cha mapato ambayo Shirika linapoteza kwa kukosa kuongeza idadi ya wateja. Sasa hebu kwa mfano, chukua malipo ya Tsh. 554,729/ anayotakiwa alipe mteja wa kawaida kwa lengo la kupatiwa umeme, kama alivyotakiwa Ndg. Salum Makame Juma, ambae hakupatiwa huduma hiyo, ukifanya kwa wateja 100 wanaohitaji kupatiwa huduma kama mwananchi huyu, ni wazi kwamba Shirika linapoteza Tsh.55,472,900/- kwa mwezi ama zaidi, huku Shirika hili likiendelea kupiga kelele za kukosa uwezo wa kulipa umeme kwa TANESCO ama kuendesha majenereta ya 32 ya dharura, kwa dai la kukosa fedha!

d) Malipo yanayolipwa bila ya wateja kupewa risiti kabisa:

Pamoja na kuunga umeme, bado Shirika linaendelea kuwa na dhima nyengine ya kutoa huduma kwa wateja hasa pale ambapo huduma zile zinakosekana kwa uharibifu au maharibiko ya aina yoyote yasiyosababishwa na mteja. Mfano kuanguka kwa nguzo au kukatika kwa waya kwenye njia kuu za umeme na mambo mengine yanayolingana na hayo.

Mfano wa matukio haya ni: -

- Bw. Moh'd Habibu Suleiman wa Kigongo kwenye njia ya umeme unaoendea kwake nguzo mbili zilianguka kwa sababu ya ubovu, pamoja na kuliarifu Shirika kwa muda mrefu juu ya tukio hilo, lakini Shirika halikuchukua hatua za mara moja na hatimae watu waliojitambulisha kuwa

ni wafanyakazi wa Shirika, walimuomba akanunue mwenyewe nguzo na wao watamaliza kazi ya kuunga (ufundi) kwa niaba ya Shirika. Aliamini hivyo kwa vile katika maelezo yao walimueleza kwamba, wametumwa kuifanya kazi hiyo baada ya kuagizwa na Shirika. Bwana Moh'd hakuwa na mashaka nao kwa sababu hapo awali alishatoa taarifa hiyo kwenye Shirika, lakini pia watu hao walionesha vitambulisho vyao vya kazi.

Jambo ambalo lilibainika kwamba, kumbe waliofanya kazi ile hawakuagizwa na Shirika isipokuwa walichukua nafasi hiyo baada ya Shirika lenyewe kutokuchukua hatua yoyote wakati lilipoarifiwa juu ya tatizo hilo. Kazi hiyo iliongozwa na Fundi Abeid (Punda) ambae kwa wakati huo alikuwa si mfanyakazi tena wa Shirika na alishirikiana na baadhi ya mafundi wengine wa Shirika ijapokuwa Bw. Mohd hakuweza kuyafahamu majina yao.

Hata hivyo Bw. Moh'd alinunua nguzo hizo mbili zenye thamani ya shs. 340,000/- na kazi ya ufundi ikatozwa shs. 170,000. Hizi shs. 340,000/- hakurejeshewa na Shirika ambalo ndilo lenye wajibu wake *(maintenance),* lakini pamoja na hayo yote hizo shs. 170,000/- za malipo ya kazi yenyewe, nazo hazikuandikiwa risiti ikiwa angalau uwe ushahidi wa malipo ya huduma iliyotolewa na Shirika. Nguzo hizo alizinunua katika kampuni ya SANA EXPRESS SUPPLY kwa risiti ya Tarehe 5/2/2012 pamoja na matumizi ya Sh.80,000/- zikiwa ni gharama za usafirishaji wa nguzo hizo **(Kiambatanisho Nam 11)**

Kwa mfano wa mwananchi huyu, Ndg. Mohd, alielipa Tsh. 170,000/- bila ya kupewa risiti, ni mfano wa mtu mmoja tu (ukiachia mbali hizo 340,000/- alizonunua nguzo na Tsh. 80,000/- za uchukuzi) kati ya zaidi ya watu 100 wanaopatiwa huduma kinyume na taratibu. Ni sawa na kusema, kwa kuzingatia uwezo wa Shirika kutoa huduma hii kwa zaidi ya watu 100 kwa mwezi Unguja na Pemba, Shirika hili linapoteza zaidi ya Tsh. 17,000,000/- zinazoingia mifukoni mwa baadhi ya watendaji wake wasio waaminifu, huku usumbufu wanaoupata wananchi wa kawaida ni mkubwa mno!

Aidha, Kamati iliikuta kadhia kama hiyo huko kwenye Msikiti wa Mwambe – Chaleni ambapo waumini wa Msikiti huo walitoa jumla ya SH.150,000/- ambazo alikabidhiwa Ndg Abeid (Punda) nae aliwaingizia umeme kwenye msikiti wao

huo. Hata hivyo baada ya mwezi watendaji wa Shirika walikuja kuukata umeme huo.

Kwa bahati, hili ililbainika mapema na kuchukuliwa hatua na Shirika, bila ya shaka mifano ya aina hii, hautakuwa huu tu uliyobainika. Maana yake ni kwamba kwa mle ambamo bado hamjabainika, Shirika linatoa huduma zisizotia mapato na tija hiyo inakwenda kwa wajanja wachache. Mazingira na jiografia ya Zanzibar si tata kiasi hicho, ni eneo dogo tunaishi pamoja na tena kwa kujuana. Shirika lina mtandao wa usambazaji wa umeme unaotambulika na ulio wazi. Jambo ambalo halisumbui hata kidogo kutambua line mpya inayoungwa. Kwa maana hiyo wale wachache wanaofahamu ndio wanaoficha kwa faida na masalahi yao.

e) Kazi kubwa ya kuunga umeme kwenye minara ya simu za mkononi kupewa Kampuni binafsi:

Kamati ilitarajia sana kwamba Shirika lingeingia mkataba wa uunganishaji wa umeme kwenye minara ya simu za mkononi, ambapo Shirika lingefanya biashara kubwa na kuingiza fedha nyingi, lakini matokeo yake biashara hizo hupewa kampuni nyengine huku kampuni hizo hutumia rasilimali za Shirika kama vile wafanyakazi na magari. Kamati imepewa taarifa na Shirika kwamba Pemba, kuna jumla ya minara ya simu 49 kati ya jumla hiyo, minara 40 ni ya kampuni ya simu ya Zantel, minara minne ni ya Kampuni ya simu ya TIGO, minara mitatu ni ya AIRTEL na minara miwili ni ya VODACOM**.**

Kati ya minara hiyo ya kampuni ya simu ya Zantel ambayo ni jumla ya 40 kwa wakati huo ambao Kamati inafanya kazi, ni minara mitatu tu iliyoungwa umeme na Shirika la Umeme (ZECO), huku minara iliyobakia (yote 37) kazi hiyo ilifanywa na kampuni ya GECCO. Na kwa upande mwengine wa minara ya kampuni zilizobakia, (Minara 9 iliyosailia) minara ya mitatu (3) ilifanyiwa kazi hiyo na kampuni binafsi ya POMY na iliyobaki ilikuwa ni kazi ya GECCO.

Sasa tuendelee kutoa ufafanuzi wa hii minara mitatu ya Kampuni ya Zantel, iliyopatiwa huduma ya umeme na Shirika, kwamba kati ya hiyo mitatu, Mnara mmoja uliopo Kifumbikai, Wete umelipiwa Tsh.792,379.80 zikiwa ni gharama za nguvu kazi tu *(Labour Cost)* kwa ajili ya kuweka umeme kwenye mnara huo,

ambapo gharama nyengine za vifaa husika zinazofikia jumla ya Shs.3,247,400, hazikulipwa kwa Shirika, **(Kimbatanisho Nam 12)** na Kamati imepata maelezo ya kuridhisha kwamba, vifaa hivyo huuzwa na Kampuni binafsi ya GECCO wakati hata Shirika lingeliweza kuuza pamoja na kuvifunga vifaa hivyo. Ingawaje bado kuna haja ya kujiridhisha iwapo vifaa hivyo vimenunuliwa na Kampuni husika ya Zantel na havikutoka katika mikono na umiliki wa Shirika. Suala hili lilihitaji ushahidi wa kina, ingawaje Kamati ilipatiwa majibu ya mdomo tu, huku ushahidi mwengine ukikosekana.

Sasa tuchukue hizo gharama za Vifaa Tsh. 3,247,400/- tukijumlisha na gharama za nguvu kazi Tsh. 792,379.80/- ni sawa na Tsh. 4,039,779.80/- kwa mnara mmoja tu. Sasa ukizidisha minara 46 iliyofanyiwa kazi na Kampuni nyengine binafsi, ni sawa na kusema kwamba, Shirika limepoteza jumla ya Tsh. 185,829,870.80/- kwa minara 46 iliyoungiwa umeme na Kampuni binafsi.! Kama huu sio upotevu wa mapato ya Shirika, basi hakuna lugha nyengine yoyote ya kukidhi majibu sahihi ya hoja hii?

Tukiendelea zaidi inafahamika wazi kwamba, Kibiashara kazi kama hizo zingelichukuliwa na ZECCO (SHIRIKA) basi fedha nyingi zingelipatikana. Lakini fedha nyingi zinakosekana kutokana na maamuzi hayo yasiyozingatia uwepo wa mapato zaidi ya Shirika, kwa madai eti halina uwezo wa kununua vifaa kwa ajili ya kazi hizo. Lakini dai jengine ni muda ambao mteja angetaka kukamilika kwa kazi yake ni jambo gumu kutokana na majukumu ya Shirika yalivyo.

Kamati imepata mashaka juu ya maamuzi hayo ambapo yanaonekana kuelekea mno kutawaliwa na tamaa binafsi kuliko uhalisia wenyewe. Hasa ikizingatiwa kwamba wanaofanya kazi hizo za GECCO ni wafanyakazi wa ZECO. Muda upi wanautumia kwa ajili ya hayo majukumu ya ZECO na muda upi wanautumia kwaajili ya kazi za GECCO, jambo ambalo linaiwezesha GECCO kukamilisha kazi hizo kwa wakati na mazingira hayo hayaliwezeshi Shirika kufanya kazi hiyo na kuweza kukidhi muda unaotakiwa na wateja.

Hebu tuchukue mfano wa Ndg. Hamidu Saidan Ali mwenye hisa 20 na Ndg. Ali Abeid Haji mwenye hisa 15 ni wafanyakazi halali wa Shirika la Umeme, pamoja na umiliki na kufanya kazi Kampuni ya GECCO, sasa ni wakati gani wanawajibika kwa bosi mmoja kati ya hawa? Jawabu ni nyepesi mmno kwa anaetaka kuelewa.

Lakini hebu na tuzingatie ufafanuzi wa GECCO kuhusu Ndg. Habibu Moh'd Ali, mfanyakazi wa ZECO lakini hutumiwa na kulipwa fedha na Kampuni ya GECCO, pale wanapona wana haja ya kutumia vifaa ama huduma ya ZECO. Kubwa zaidi wanalofanya ni kumtumia mfanyakazi huyu kwa kuwasaidia kuwa kiunganishi bora katika majukumu yao.

Kwa hali hiyo isiyovumilika pia iliwashtua sana wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika, kwani katika uchunguzi wake Kamati ilipata nakala za Kumbukumbu za Kikao cha 110 cha Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika kilichofanyika Tarehe 20/01/2011, ambapo pamoja na mambo mengine ambayo Bodi imeyajadili katika kikao hicho, lakini pia ilizungumzia juu ya ushiriki wa baadhi ya wafanyakazi wa Shirika ambao pia ni wafanyakazi wa Kampuni ya GECCO, kwamba wanachanganya mambo mawili kwa wakati mmoja na matokeo yake ni kwamba kunakuwa na mgongano wa kimaslahi, jambo ambalo Bodi imesema kwamba limeanza kujitokeza na hivyo katika kikao hicho iliwataka watendaji wachague moja kati ya GECCO au ZECO.

Aidha katika kuonesha kwamba kampuni ya GECCO inachangia sana utendaji wake kupunguza mapato ya Shirika kutokana na ushiriki wa baadhi ya watendaji hao wa Shirika wanaofanya kazi pia kwenye GECCO, Bodi hiyo ya Wakurugenzi iliagiza kufutwa mara moja kibali cha uuzaji wa Transfoma unaofanywa na Kampuni ya GECCO. Hiyo ni moja ya biashara kubwa ambayo bila ya shaka Shirika lenyewe linaweza kuifanya, lakini kutokana na kile ambacho Bodi imekisema **mgongano wa kimaslahi** basi bila ya shaka ndicho hicho hicho Kamati ilichokiona kwenye suala zima la uwekaji wa huduma ya umeme kwenye minara ya simu za mkononi, kwamba linaendana na utaratibu huo huo wa maslahi binafsi. Kwa bahati Shirika la Umeme lilitimiza agizo hilo la Bodi linalohusu wafanyakazi na lile la ufutaji wa kibali cha uuzaji wa Transfoma na limeiandikia kwa maana ya kuiarifu Kampuni hiyo ya GECCO, kwa barua ya Tarehe 28/2/2011 yenye nambari ya kumbukumbu ZECO/TENDER/09/VOL.1 **(Kiambatanisho Nam 13)**.

Pamoja na yote hayo Kamati ilipata mshangao kuona karatasi ya kupokelea mali *(Delivery Note)* ya Tarehe 30/04/2012 Nam. 1155 iliyotoka GECCO kwenda ZECO Pemba, yenye kuonesha mapokezi ya Transforma tatu, bidhaa hizo kwa

mujibu wa karatasi hizo zinaonesha kuwa zimesafirishwa kwa Meli ya M V SERENGETI. Kabla ya hapo mnamo Tarehe 19/04/2012 *Delivery Note* yenye Nam. 1154 ilipelekwa kwa Ndg. Habibu Mohamed wa ZECO, Pemba yenye vifaa mbalimbali vya umeme **(Kiambatanisho Nam 14)**.

Jambo la kujiuliza ni GECCO ipi iliyozuiwa kufanya biashara ya uuzaji wa Transforma kwa maana ya kufutiwa kibali hicho na ZECO, Tarehe 28/2/2011, na GECCO ipi ambayo inaendelea na biashara hiyo?. Kamati haikupata barua nyegine iliyotoa tena kibali hicho. Hilo nalo likawa ni sehemu ya ubabaishaji unaofanywa na Shirika katika kung'ang'ania kuzipa Kampuni binafsi kazi kubwa hata kama Shirika lenyewe linaweza kuzifanya.

f) Baadhi ya wateja kutokuwemo kwenye orodha wa mafail ya wateja wa Shirika.

Kamati ilipata orodha ya watu/wananchi ambao wanatumia huduma hiyo ya umeme bila ya kusajiliwa rasmi kwenye mtandao wa wateja kwenye Shirika. Katika kutafuta ukweli juu ya jambo hili, Kamati iliarifiwa na Shirika lenyewe Tawi la Pemba, kwa kukiri kwamba kuna Wateja ambao taratibu za uungwaji wa umeme wao zilikuwa na utata. Utata wao ulibainika wakati wa ukaguzi wa nyumba kwa nyumba uliofanywa na Shirika na kugundua Wateja Ishirini na Tatu (23) wanatumia umeme bila ya kulipia, lakini vilevile hawamo kabisa katika mfumo wa malipo ya Wateja wa Shirika. Orodha ya Wateja ambao Kamati imekabidhiwa na Shirika kwamba wana utata ni kama wafuatao:-

1.Ndg Abdallah Ali Khamis	-	Vitongoji
2. Ndg Rashid Abdalah Ali	-	Vitongoji
3. Ndg Said Hassan Abdallah	-	Vitongoji
4. NdgGhania Abdi Nassor	-	Wete –Baghani
5. Ndg Hassan Mjaka Juma	-	Tondooni-Makangale
6. Ndg Haroub Suleiman Said	-	Bandari Kuu –Konde

7.Ndg Makame Faki Haji - Tondooni-Makangale

8. Ndg Juma Haji Makame - Wete

9. Ndg Ali Asaa Sheha - Konde

10. Ndg Mohamed Zahor - Konde

11. Ndg Bakar Mohamed Bakar - Tondooni –Makangale

12. Ndg. Salim Hamad Salim - Chanjaani – Konde

13. Ndg. Juma Khamis Juma - Bule

14. Ndg. Hamad Shaibu - Chimba

15. Ndg. Said Mbwana Ali - Chimba

16. Ndg. Abdallah Salim Said - Bule

17. Ndg. Mohamed Shaibu Mohamed - Mkoani

18. Ndg. Sharif Shaaban Mwalim - Mkoani

19. Ndg. Bakar Hamad Seif - Gombani

20. Ndg. Ali Khamis Juma - Gombani

21. Ndg. Asha Khamis Juma - Gombani

22. Ndg. Sumaiya Said Ali - Gombani

23. Msikiti wa Sebinyemi - Matale

Orodha hiyo bila ya shaka inaonekana dhahir kwamba ni wananchi wale tu waliokaguliwa tena kwa baadhi ya wale walioko Pemba tu, lakini kwa sababu si nyumba zote zilizokaguliwa, maana yake ni kwamba upotevu huo wa mapato ni mkubwa kwa uhalisia wake kuliko vile unavyoonekana sasa. Kwani Kamati inaamini kuna zaidi ya wateja hao walioainishwa ambao uungwaji wa umeme wao haukufata taratibu.

Hata hivyo kama kuna wateja wa aina hii ambao uungwaji wa umeme wao haukufata taratibu maana yake ni kuwa, Shirika limekuwa likipoteza mapato yake kila siku kwani wateja wa aina hii si tu wamekuwa wakilikosesha Shirika mapato yanayohusiana na gharama za uungwaji tu, bali hata yale mapato yanayotokana na malipo ya kila mwezi.

Sasa hebu tujikumbushe kiasi gani zinazopotea kwa Shirika kwa mfano wa wananchi tuliowataja hapo juu, huku tukijua kwamba, hiyo ni idadi ndogo sana ya wananchi wa aina hii. Na tutoe mfano wa mwananchi mmoja angelilipa Tsh. 8,000/- za Fomu ya maombi na malipo ya kuungiwa umeme kwa nguzo 1 tu na 'Roof Poll, ambapo malipo yake ni Tsh. 442,593/-, Jumla ya malipo kwa mtu mmoja ni Tsh. 450,593/-. Sasa iwe kwa watu wote 23, ni sawa na kusema Shirika lingelipata malipo ya Tsh. 10,363,639/-. Ukiachilia mbali huduma hiyo ya malipo ya Fomu na Kuungiwa Umeme, lakini pia kuna malipo mengine yanayotokana na malipo ya kila mwezi kwa ajili ya huduma ya umeme yanakosekana.

Kwa mfano kila mmoja kati ya wateja hao angelikuwa analipia kiwango cha chini sana cha malipo, Tsh.5000 kwa kila mwezi, basi Shirika lingelipata zaidi ya Tsh. 115,000/- kwa mwezi, ni sawa na kupoteza Tsh. 1,380,000/- kwa mwaka, ingawaje ifahamike wazi kwamba, kiwango tulichokisia hapa ni kidogo sana cha Tsh. 5000 kwa mwezi, wakati kwa kawaida wananchi wengi hulipia zaidi ya Tsh. 20,000/- kwa mwezi.

1.6.0 WATEJA WALIOTEMBELEWA UNGUJA:

Kwa upande wa Unguja Kamati ilikabidhiwa idadi ya Wateja Wakubwa wa Shirika, wenye Mahoteli na Kampuni mbali mbali wafikao 160, **(Kiambatanisho Nam. 15),** na upande wa Wateja wa Minara ya Simu wanne, ambapo Zantel pekee inamiliki vituo vya Minara vifikavyo 48, TTCL vituo 27, TIGO vituo 17 na Celtel 14 **(Kiambatanisho Nam. 16).** Kwa kuzingatia wingi wa wateja hao, na muda mdogo uliokabidhiwa kwa Kamati, Kamati ilifanya mifano yao (sampling) kwa kutembelea Wateja 21 wa Makampuni ya Mahoteli, huku mijadala kuhusiana na Minara ya Simu, ikijadiliwa kwenye vikao tofauti baina ya Kamati na Uongozi wa Shirika na mara nyengine Kampuni ya GECCO, ambao kama tulivyokwishaona upande wa Pemba, pia walihusika na utoaji wa huduma ya umeme kwa Kampuni hizo.

Aidha, Kamati ilitumia siku 3 za ziara kwa kuwatembelea wateja hao 21 na hatimae, imejiridhisha zaidi kwa kupata ufafanuzi wa baadhi yao kama ifuatavyo:

1. **Sea Rock:**

Kamati kwanza ilitembelea eneo liliopo Hoteli hii, na kugundua kwamba imeungwa umeme bila ya taratibu. Kamati ilipata pia maelezo ya Uongozi wa Shirika kwamba, wao waligundua zamani kwamba 'Sea Rock' wameunga umeme bila ya ridhaa zao na kinyume na taratibu zilizopo, kwani kilichogundulikana umeme wa mteja huyu umeungwa na Kampuni kutoka Tanzania Bara, ambapo umeme huo ulichukuliwa kutoka ulipokuwepo ambapo ni masafa ya nguzo kumi hadi hotelini vifaa vilivyotumika kama vile waya nguzo pamoja na Transforma vyote havikuhakikiwa na Shirika.

Kamati ilipohoji juu ya hatua zilizochukuliwa na Shirika kutokana na kufahamu hali hiyo, Uongozi huo ulieleza kwamba, waliwaita na kufanya makisio mapya na hatimae wakawapiga faini kutokana na kukiuka taratibu za uungaji wa umeme. Pamoja na hali hiyo, wakati Kamati inaendelea na mahojiano na Uongozi wa Shirika kuhusu Hoteli hii, ilielezwa kwamba, mwanzo walipeleka maombi yao kwa Shirika kupitia barua ya tarehe 07/09/2009 **(Kiambatanisho Nam 17).**

Pamoja na maelezo hayo, barua hiyo aliyoieleleza Meneja Mkuu kwamba ndio ya maombi, inahusiana na 'Ubadilishaji wa njia ya line ya Umeme ya H.T', na wala haihusiani na maombi ya kuungiwa umeme. Yaani, kwanza yalifanyika maombi ya kuungiwa umeme, na ndio baada ya hatua hiyo, Mkurugenzi Mkaazi wa Kampuni ya 'Sea Rock', aliomba kubadilishiwa line ya awali kwa kuwekewa line mpya. Kwa maana hii, Kamati iliendelea kutia shaka juu ya taratibu za maombi na kuruhusiwa kwa Kampuni hii, kama taratibu zinavyostahiki kufuatwa kuhusiana na suala hili.

Hata hivyo, Kamati ilitaka kupatiwa fomu ya maombi ambayo, baada ya Mteja Mkubwa kupeleka barua yake ya maombi, huijaza, na kupewa 'FORM:01' ambayo kwa ujumla haina saini yoyote ya Mteja huyo **(Kiambatanisho Nam 18).** Aidha, kama utafanya tena rejea ya fomu ya maombi ya umeme inayotambulikana kama FORM B iliyomo katika Kielelezo tunachokizungumizia, utaona katika sehemu ya maelezo, kuna neno 'ILLEGAL', ikimaanisha kwamba Mteja huyu amejiungia

umeme mwenyewe kabla ya kuwasiliana na Shirika, na hana haki ya kisheria ya kupewa huduma aliyoiomba. Aidha, maelezo hayo yana maana kwamba, Shirika kwa kuzingatia tabia aliyoionesha Mteja huyu, imekataa kumpatia huduma ya umeme. Hii inatokana na ukweli kwamba, Mteja huyu tokea mwanzo alikwishajiungia umeme kinyume na taratibu.

Aidha, pamoja na makosa aliyoyafanya, na hoja ya Shirika kuipiga faini Kampuni hii, mnamo tarehe 25/03/2010, Shirika lilipokea barua kutoka kwa 'Sea Rock', kutaka kuunganishiwa 'Transforma' ya umeme Mkubwa wa KvA 315, kupita line ya KV 33. Hata hivyo, Shirika limeshindwa kuthibitisha iwapo kweli walitoza faini kwa Sea Rock, na hatimae malipo yaliyothibitika kulipwa na Kampuni hii ni ya Tsh. 12,132,760/- yanayotokana na kuungiwa Transforma husika, na kufanywa mwaka 2010 **(Kiambatanisho Nam 19)**.

Tunachotaka kuweka wazi katika ufafanuzi wa mteja huyu ni kwamba, Shirika halifahamu inachokifanya. Kama Mteja amevunja sheria kwa kujiungia umeme kinyume na taratibu, ni wajibu wa Shirika kusimamia Sheria zake na sio kumbembeleza mteja. Sasa kama mteja huyu anaachiwa, eti kwa kisingizio cha kuwapiga faini, ambayo imeshindwa kuthibitishwa na Kamati kwa kukosekana kielelelezo kinachothibitisha, kama vile pia ilivyoshindikana kuthibitisha uwezo wa Shirika kisheria kutoza faini, kitu ambacho kwa mujibu wa kifungu cha 39(1) cha Sheria Nam.3 ya 2006, pamoja na kutajwa adhabu ya faini kwa anaeiba umeme ama kufanya makosa yanayowiyana, basi uwezo wa kutoa adhabu hiyo kwa mujibu wa Sheria ni wa Mahakama na sio Shirika hili!.

Kwa lugha nyengine, Kamati imejiridhisha kwamba, kuna upotevu mkubwa wa mapato ya Shirika, na pia husababishwa na uzembe na usimamizi mbovu wa dhamana za watendaji wa Shirika, waliokabidhiwa dhamana husika. Hebu kwa mfano tuchukulie mteja huyu pamoja na umeme mkubwa aliotumia, pamoja na wingi wa vifaa vilivyotumika na mambo mengine, fedha yake ya kupewa huduma iliyoingia katika Shirika ni Tsh. 12,132,760/- pekee ya gharama za nguvu kazi pekee, huku hata fedha ya malipo ya fomu, Tsh. 12,000/- zikishindikana kuthibitishwa kwamba zimelipwa.

2. Ras Kichanga:

Mteja mwengine ambae Kamati imepata nafasi ya kuhojiana na Uongozi wa Shirika, ni kuhusiana na hoteli ya Ras Kichanga, iliyopo Michamvi, Mkoa wa Kusini Unguja. Wakati Kamati inafanya ziara katika eneo hilo, iligundua kwamba, kuna 'Transforma' ambayo ni mali ya Hoteli, nguzo 2, huku umeme katika hoteli hii unaaminika kwamba umeungwa mwaka 2004. Kuhusiana na utaratibu wa maombi kwa Mteja huyu, Kamati imeshindwa kupata uthibitisho wa barua yoyote ya maombi na hivyo imeshindwa kupata uthibitisho wa kujazwa kwa fomu ya maombi ya Mteja huyu. Kwa lugha nyengine taratibu za kuungiwa umeme kwa mteja huyu zimekiukwa.

Tatizo liliojitokeza kuhusiana na suala hili ni kukosekana kwa faili lenye vielelezo vilivyohitajika. Kosa kubwa la Shirika ni kupoteza kumbukumbu za wateja wake, kama tutakavyoeleza suala hili hapo baadae.

3. Mwamba Investment:

Hoteli hii pia iko Michamvi na imepatiwa huduma ya umeme. Kiasi ya nguzo 15 zimetumika kuutoa umeme katika sehemu moja hadi katika eneo la hoteli, huku Mteja huyu akitumia 'Transforma' yake mwenyewe, kama vile Kamati ilivyoelezwa kwamba, wateja wote wakubwa huwa wananunua transforma zao wenyewe kupitia Shirika la Umeme. Kampuni hii imepeleka maombi yake tarehe 14/09/2009, na kujaza fomu ya maombi tarehe 15/10/2010, na hatimae imenunua vifaa pamoja na kufanya malipo kama inavyotakiwa **(Kiambatanisho Nam 20)**. Kamati imejiridhisha kwamba, Kampuni hii imejitahidi sana kufuata taratibu zilizowekwa na Shirika, na hata malipo yake yamefanyika bila ya shaka yoyote.

4. Atlas Hotel:

Kampuni ya Atlas Michamvi Resort Ltd, yenye hoteli ya Atlas Hoteli, imeandika barua ya maombi ya kuungiwa umeme tarehe 01/03/2011 na kujaza fomu ya maombi kwa ajili ya huduma hiyo, tarehe 17/11/2011 na hatimae kukubaliwa mnamo tarehe 25/11/2011. Wakati Kamati inapitia faili la Mteja huyu, imejiridhisha kwamba vielelezo vyote vilivyotakiwa na taratibu zilizohitajika zimefuatwa, ingawaje imetia wasi wasi kwa Kampuni vilikonunuliwa vifaa vya umeme vilivyohitajika, ambayo ni Sun General Supply, kwamba haimo katika

orodha ya Kampuni zilizoruhusiwa na Shirika, kutoa huduma ya kuuza vifaa vya umeme.

Aidha, baada ya kupitia Kumbu kumbu ya kikao cha 89 cha Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika, Kamati ilithibitisha kwamba, kikao hicho kiliruhusu Wafanyabiashara 7 tu, ambao ni Toyota Store; Trade Links; M/M General Traders; Mwembeladu Store; GECCO; OSAJU na SANA Epress. Kwa hiyo ni wazi kwamba, Kampuni ya Sun General Supply, haijapewa kibali cha kuuza vifaa vya umeme, na jambo la kushangaza zaidi, Uongozi wa Shirika umeshindwa kulisema ama kulichukulia hatua tatizo hili. Ni wazi basi, kwamba, katika kasoro kubwa za Uongozi wa Shirika ni pamoja na kutofuata maelekezo na miongozo halali ya Bodi ya Wakurugenzi.

Aidha, wakati Kamati inakagua risiti zilizoambatanishwa katika faili hilo na kuwa **Kiambatanisho Nam 21**, gharama ama manunuzi ya nguzo hayakuonekana. Kamati ilipotaka maelezo ilielezwa kwamba, Shirika ndilo lililowauzia Kampuni hii, nguzo, na ndio maana hazikuonekana katika risiti ya vifaa vilivyonunuliwa na Kampuni. Pamoja na maelezo haya, Kamati ilitaka kuthibitishiwa na zaidi kutaka kuona nani aliyelipwa gharama za ubebaji wake, nguzo ambazo kwa kawaida hubebwa kwa gari maalum ambazo humilikiwa na Shirika. Hata hivyo, Uongozi wa Shirika ulisema kwamba, Kampuni imetumia usafiri wake wa hoteli, ingawaje wameshindwa kuthibitisha juu ya hili.

Sasa hebu rejesha tena kumbukumbu zako katika Kampuni iliyouza vifaa hivyo kwa mteja huyu, kwamba haimo katika zilizoruhusiwa, wakati huo huo sio vifaa vyote vyote vilivyotumika katika kupelekewa umeme vikawa vimeorodheshwa katika risiti, ni wazi kwamba, akili yako itatafakari mengi tu, kwamba inawezekana sana kukawa na mchezo mchafu wa baadhi ya watendaji kutumia nguzo na vifaa vyengine vya Shirika kwa wateja bila ya malipo ya vifaa hivyo kuingia katika Akaunti ya Shirika. Huku ni kupotezewa mapato ya Shirika, kwa makusudi kabisa!

5. Kae Funk Sunset Beach:

Hii inahusika na Bungalow inayomilikiwa na Ndg. Eddie T. Mattar. Kamati ilipofika eneo liliopo Bungalow hii, Uongozi wa Shirika ulishangaa na kusema kwamba, mteja huyu hayumo katika orodha ya wateja wao. Kwa lugha nyengine, mteja huyu amejiungia umeme kinyume na taratibu. Aidha, Kamati imeshuhudia zaidi ya nguzo 30 feki, (Haziko katika kiwango, ni nyembamba, fupi na zimechakaa) zimetumika kusambazia umeme katika Bungalow hii. Hata hivyo, wakati Kamati ilipofanya mahojiano na Uongozi wa Shirika kuhusiana na Mteja huyu, walikiri kwamba ni mteja wao halali mwenye nambari ya hesabu D 36888, ingawaje wameshindwa kuthibitisha maombi yake, na namna alivyoruhusiwa kupatiwa huduma ya umeme.

Kwa ufupi tuseme kwamba, huyu ni mteja feki wa Shirika, aliejiungia umeme bila ya kufuata taratibu zilizowekwa lakini pia amepoteza mapato ya Shirika, ingawaje Shirika lenyewe baada ya kumchukulia hatua za kisheria, bado linaendelea kumbembeleza na hatimae kufuga wizi wa meme, huku wanachokilipa mara nyingi huingia katika mifuko ya watendaji wachache wa Shirika.

Unataka kusema kwamba, Shirika pia limeshindwa kusimamia Sheria yake Nam. 3 ya mwaka 2006 msisitizo kwa hili ukiwekwa katika makosa yaliyoorodheshwa katika sehemu ya VII ya Sheria hiyo. Au labda Shirika líseme kwamba, wakati mteja huyu anajiungia umeme kinyume na sheria, sheria zinazosimamia uhalifu wa aina hii hazikuwepo. Basi la kushangaza zaidi, wakati Kamati inafika katika eneo la tukio, ilielezwa kwamba mteja huyu hajawahi kupelekewa 'Bill' ya malipo inayotakiwa kutolewa na Shirika kwa kila mwezi, kama Kanuni ya 10 ya Kanuni za Shirika la Umeme zinavyoelekeza, kama tunavyonukuu:

> "Bills shall be rendered monthly and be paid on the date specified in the bill at designated locations, failure to reveice the bill shall not exempt customers from payment"

Jee, Uongozi wa Shirika umeghafilika kutekeleza hata kanuni zake, au Shirika limegeuka shamba la bibi, kwamba kila mtu anavuna anachotaka na anavyotaka! Sasa wananchi wanyonge wa nchi hii wataacha kweli kulalamika, wakati Shirika hili hili huwa wakali dhidi yao. Hukatiwa umeme hata kama wanadaiwa Tsh.10,000/- wakati wenye biashara zao, tokea walipopata huduma ya umeme

kinyume na sheria, hakuna malipo yoyote wanayolipa zaidi ya miaka mitatu. Na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi yao, zaidi ya Viongozi hawa kujifanya wanashangaa namna watu wanavyoiba umeme.

6. The Residence (The Hotel Property):

Kamati imeshindwa kupata barua ya maombi ya Kampuni hii, ingawaje ilipatiwa Form 01 pamoja na FORM B, zinazohusiana na ujazaji wa maombi ya mteja mpya **(Kiambatanisho Nam 22)**, ingawaje malipo ya maombi Tsh. 12,000/- zimeshindikana kuthibitishwa kulipwa kwake, kwa kukosekana risiti ya malipo ya fomu za maombi hayo. Kampuni hii inayomiliki hoteli kubwa ya kitalii eneo la Kizimkazi Mchangamle, imeungiwa umeme kwa thamani ya Tsh. 2,311,733/- (Rejea Kiambatanisho Nam 22), wakati imevuta umeme kwa kutumia takriban nguzo 46. Shirika la Umeme katika kulijibu hili, ilieleza kwamba, wao kama Shirika wamehusika na malipo ya 'labour charge' tu, kutokana na mteja huyu kutaka kuungiwa transfoma, na ndizo gharama za fedha hizo, tulizoziainisha kabla.

Aidha, Shirika limesema huduma ya kuvuta umeme kwa nguzo hizo takriban 46 imefanywa na Kampuni ya CRJE na wala sio wao. Maelezo haya hata hivyo, yanakiuka kifungu cha 4(a) cha Sheria ya Shirika la Umeme, Namba 3 ya Mwaka 2006, inayoeleza kwamba, Shirika hili ndilo pamoja na kazi nyengine, litasambaza umeme huo kwa Mtumiaji ama Mteja yoyote hapa Zanzibar. Aidha, pamoja na Shirika kusema kwamba, Transfoma ni milki ya Kampuni, kwa kuwa wao Shirika ndio wenye dhamana ya kuwaungia umeme, na kuhakikisha kwamba, vifaa vyote vinavyonunuliwa na Mteja viko katika kiwango kinachotakiwa, kwa kawaida pia hujiridhisha kwa uhalali wa ununuzi wa transfoma na kiwango chake.

Kwa Kamati, hili pamoja na vifaa vyengine vilivyofungwa kwa mteja huyu, imeshindwa kupata risiti za manunuzi yake wala kielelezo chengine cha vifaa hivyo, tofauti na Kampuni nyengine ambazo huweka kumbu kumbu ya risiti na vielelezo hivyo.

7. Kendwa Beach Resort:

Barua ya maombi ya mteja huyu haikupatikana wakati wa ukaguzi wa Kamati. Aidha, kilichoweza kupatikana ni fomu ya maombi ya kuungiwa umeme, FORM 01, huku fomu ya masharti ya usambazaji (Conditions of Supply), ikishindwa

kutiwa saini wala kujazwa chochote **(Kiambatanisho Nam 23)**. Aidha, FORM B imeonekana, lakini hakuna uthibitisho wowote wa malipo yaliyofanyika kwa mteja huyu, kulipia maombi hayo. Mnamo tarehe 24/10/2011 ilipokelewa barua ya mteja huyu akiomba kubadilishiwa transfoma, huku malipo halisi ya mabadiliko hayo ni Tsh. 1,488,452/- kama inavyothibitika katika Kielelezo kinachohusika na hoja hii.

8. Docrim Hotel:

Na Hoteli hii nayo imeunga umeme bila ya kupeleka maombi ya kufanya hivyo. Hata hivyo, kwa kigezo cha kujaza fomu, Hoteli hii pia haijajaza fomu hizo kisheria. Kwa maana fomu ya usaili, FORM 01, haina saini yoyote ya kuthibitisha imejazwa kisheria. Aidha, fomu inayohusiana na masharti ya kuungiwa umeme, ndio haijajazwa kabisa. Hata hivyo, FORM B ndiyo iliyojazwa huku ikikosa saini za Mkuu wa Upimaji na Mkuu wa Sehemu ya Mita na badala yake imepata kibali cha Mkuu wa Mains na Msimamizi wa kazi za uvutaji wa 'Main Service line'. Aidha, fomu hiyo inaonesha makisio ya kuungiwa umeme huo ni Tsh. 14,171,564/- ambazo ni nyingi sana ukilinganisha na wateja wengine, kama vile The Redisence ama 'The Hotel Property', wakati mteja huyu ameungiwa umeme kwa takariban nguzo 15 za Shirika.

9. Shumbana Amani Karume:

Katika Wateja waliosababisha kuwepo kwa majibizano makali na mjadala mrefu ni mteja huyu, Ndg. Shumbana Amani Karume anaemiliki nyumba ya kupumzikia iliyopo Matemwe Zanzibar. Shirika katika kumtetea mteja huyu lilieleza Kamati kwamba, ni mteja Mkubwa lakini ni muekezaji hivyo walimpatia upendeleo na kumzingatia kama Waekezaji wengine. Kamati kwa upande wake haikuridhika kwamba, ni muekezaji kwa sababu anamiliki nyumba ya kupumzikia na haendi ila mara chache tu kwa kitambo cha miezi, huku nyumba hiyo haitumiki na yeyote zaidi ya kuwepo walinzi wa kumlindia.

Baada ya mjadala mrefu, ilikubalika kwamba, Ndg. Shumbana Karume ni Mteja Mkubwa, mwenye tranfoma ya 50 kVA. Wakati Kamati inahoji juu ya uhalali wa transfoma hiyo, ilielezwa kuwa ni ya Ndg. Shumbana, ingawaje hakuna uthibitisho wa aliponunua transfoma hiyo, na ni wazi kwamba, Kamati inaamini ni mali ya Shirika.

Vile vile, barua ya maombi iliyopokelewa na Shirika kutoka kwa Mteja huyu, haikuweza kuthibitishwa ingawaje kuna uthibitisho wa maombi ya Mteja kupitia FORM 01 na FORM B, zinazothibitisha kwamba, Ndg. Shumbana amelipia Tsh. 4,259,787 kwa kazi ya ukaguzi (Surveying Work), huduma za waya (Service Line), ufungaji wa mita (installation of metre), fomu ya maombi (Application Form) na gharama za usafiri **(Kiambatanisho Nam 24)**, huku gharama ama malipo ya fomu ya kujiunga kama mteja mpya, yakishindwa kuthibitishwa.

Jambo la kushangaza ni kwamba, mteja huyu ametumia nguzo zaidi ya 31 kwa umbali unaokisiwa kuwa zaidi ya kilomita 2.5, huku hakuna uthibitisho uliowasilishwa kwa Kamati, kwamba nguzo hizo ni mali ya mteja, kama vile pia ilivyoshindwa kuthibitishwa kuuzwa na Shirika. Kwa lugha nyengine, gharama za nguzo hazihusiki na malipo yaliyofanywa na mteja, huku gharama alizolipa mteja huyu kwa ujumla wake ni ndogo ukilinganisha na huduma aliyopewa.

10. The Seyyida Hotel:

Kampuni hii nayo imepata huduma ya umeme kutoka Shirika la Umeme Zanzibar, kupitia maombi iliyoyafanya tarehe 01/09/2009 **(Kiambatanisho Nam 25)**. Maombi ya mmiliki wa hoteli hii yanaonekana kupitia FORM 01 na FORM B, ambazo hazina uthibitisho wa saini ya Mkuu wa sehemu ya Mita wala Mkuu wa Mains; hivyo ni sawa na kusema fomu hizi hazina uthibitisho wa kisheria. Hata hivyo jumla ya Tsh. 3,373,157.44 zimelipwa kwa kazi ya kufunga mita ya umeme pamoja na gharama nyengine zinazohusika. Kama ilivyo kwa wateja wengine, transfoma ya mteja huyu ni milki yake, ingawa wapi ameinunua na vipi Shirika halikuweza kuthibitisha, ni jambo linaloendelea kuhitaji uthibitisho kwa sababu, Kamati haikupatiwa uthibitisho huo.

Pamoja na kutakiwa kulipa 3,373,157.44 uthibitisho uliowasilishwa kwa Kamati unahusiana na makisio tu ya gharama zilizohitajika, huku uthibitisho wa wapi yalilipwa na kupokelewa, umeshindwa kuthibitishwa kwa Kamati. Vile vile, mteja huyu amesamehewa Kodi ya VAT, huku Kamati ikishindwa kupatiwa utaratibu uliotumika hadi akasamehewa na hii ina maana, pamoja na makisio yake kuwa kima tulichokwisha kieleza hapo juu, fedha hizo hazijalipwa kama zilivyokisiwa, ikiwa ni pamoja na kusamehewa VAT. Hata hivyo, kwa kuwa kima cha VAT cha

18% sawa na Tsh. 514,549.44/- kimeagizwa kutolewa, inawezekana ikawa fedha zilizolipwa ni Tsh. 2,858,608/-.

11. The Leisure Hotel:

Hakuna utaratibu wowote wa maombi ya umeme kwa mteja huyu, kama vile ilivyoweza kuthibitika fomu moja tu 'FORM B' inayoonesha angalau taarifa kadhaa na nia ya kuungiwa kwa umeme kwa mteja huyu. Makisio aliyofanyiwa ni Tsh. 1,387,752/- ingawaje hazihusiani na manunuzi ya vifaa, huku pia Kamati ikishindwa kukabidhiwa uthibitisho wa wapi vifaa hivyo vimenunuliwa.

12. Larosa Deivent:

Hakuna barua yoyote ya maombi ya mteja huyu, huku pia hata fomu za kuungiwa umeme zilizomo katika taarifa zake, hazina saini yoyote wala taarifa zilizohitajika. Kwa lugha nyepesi, kuungiwa umeme kwa mteja huyu hakujafuata taratibu zilizohitajika. Makisio yaliyohusika na kazi hii ikiwa ni pamoja na ghama za baadhi ya vifaa bila ya kuhusisha Transfoma ni Tsh. 2,601,605/-. Tatizo linaendelea kuwa lile lile la kawaida, wapi imepatikana transfoma, kwa ushahidi upi, lakini jee Shirika liliikagua na kujiridhisha kufaa kwake? Vi masuala yaliyokosa jawabu mbele ya Kamati.

13.One Stop Company:

Mteja mwengine wa Shirika ni Kampuni hii ya 'One Stop' iliyopo Forodhani, ambapo pamoja na kukosekana kwa barua yao ya maombi ya huduma ya umeme, wamejaza fomu zilizohusika kwa kazi hii na kupatiwa makisio ya gharama za umeme. Tatizo moja sugu ambalo hatukulieleza kabla ingawaje limeonekana sana ni makisio hayo kukosa saini ya 'Operation Manager' na badala yake ni 'Planning Engineer' pekee wa Shirika huandaa makisio hayo na kuyasaini, huku yakiwa hayajapata ithibati inayostahiki ya 'Operation Engineer'.

Makisio hayo yaliyogharimu Tsh. 6,341,556/- yamethibitishwa kulipwa kwa Shirika. Aidha, Kamati kwa mara ya kwanza katika wateja wote tuliowataja hapo juu, imejiridhisha kwa mteja huyu kuwa na ripoti ya majaribio ya ufungwaji wa umeme huyu (Consumer Installation Test Report), ambayo kwa ujumla wake

inaonesha ni kwa kiasi gani Shirika lilivyotakiwa kufanya hivyo kwa kila mteja wake mkubwa, jambo ambalo wengine wamekosa kufanyiwa.

1.7.0 Mafaili ya Wateja Wakubwa yaliyokosekana kukaguliwa na Kamati:

Ukiacha mbali taarifa za wateja tuliowazungumza hapo juu, na kwa mnasaba wa orodha ya wateja wakubwa tuliyoifanya Kiambatanisho cha ripoti hii, taarifa za wateja takriban 147 zimekosekana kwa kukaguliwa na Kamati, kwa maelezo kwamba, mafaili yaliyokuwa yanahifadhi taarifa hizo, yamerowa kwa mvua katika ofisi kongwe ya Shirika Mwanakwerekwe, kwa sababu bati la ofisi hiyo ni bovu na lilikuwa linavuja, pale inaponyesha mvua. Aidha, maelezo haya yametolewa, bila ya kujali uzito wa umuhimu wa taarifa za wateja hao, na hata kujali kwamba, taarifa hizo sio mali ya mtendaji binafsi wa Shirika, bali ni sawa na mali ya Serikali.

Na unapofanya rejea ya Sheria zinazohusiana na nyaraka za Serikali, suala hili halitakuwa geni kwako na ingelistahili kwa Uongozi wa Shirika, kufahamu madhara wa wanachokifanya, ikiwa kwa makusudi kwa lengo la kuipotosha Kamati ama kuficha ukweli uliohusika ama kwa uzembe uliopelekea mafaili ya wateja kupotea. Hebu pia tukumbuke kwamba, kifungu cha 9 cha Sheria Namba 5 ya mwaka 1983, Sheria ya Usalama wa Taifa na Siri za Seriakali (The National Security and Official Secrets Act), pamoja na mambo mengine, kinakemea tabia hii ya Uongozi wa Shirika kupoteza taarifa za Serikali, ikiwa ni pamoja na uzembe uliofanyika hupelekea taarifa hizo kupatikana na watu wengine wasiohusika.

Katika hali ya kawaida huwezi kuamini kwamba Shirika kubwa lenye hadhi kama hili la Umeme, kwamba linashindwa kutengeneza Ofisi yake kwa tatizo eti la kuvuja wakati Shirika hilo linatumia fedha nyingi tu kwa mambo mengine ambayo wala si muhimu sana.

1.8.0 ZANZIBAR DATA COM LTD:

Miongoni mwa wateja wakubwa wa Shirika la Umeme ni Kampuni ya Zanzibar Data Com, yenye mahusinao na Shirika kupita mnara wa Shirika uliopo Mtoni

ambao umekodiwa na Kampuni hii. Suala hili lilianza kufahamika mara tu Kamati ilipoanza ziara ya kutembelea eneo la majenereta Mtoni, ambapo ilipohoji juu ya mnara uliopo pembeni mwa eneo hilo, iliambiwa ni mali ya Shirika, lakini umekodishwa kwa Kampuni hii. Kufuatia hili, Kamati ilitaka kuhoji juu ya umeme unaotumiwa na Kampuni hii, ambapo ilifahamishwa kwamba, Kampuni ya Zanzibar Data Com imekodishwa mnara kwa kuweka vifaa vyake vya matangazo, na kwa kuwa inatumia huduma ya umeme wa Shirika, ilipaswa kulipa na kuungiwa umeme huo kama wateja wengine. Ili kufahamu vyema kuhusiana na mteja huyu, ni vyema ukafuata utaratibu ufuatao:

1.8.1 Mkataba baina ya Shirika na Kampuni ya Zanzibar Data Com Ltd:

Ukitaka kufahamu juu ya uhusiano wa kibiashara baina ya taasisi hii na mtu ama Kampuni yoyote, akili yako kwanza itaanza kuulizia kuhusiana na Mkataba wowote wa kisheria uliopo baina yao. Ni kweli kwamba, uhusiano wa kibiashara baina ya Shirika ya kutoa huduma ya umeme kwa Kampuni ya Zanzibar Data Com ama huduma ya mnara inafuangamanishwa na Mkataba ulioingiwa kisheria tarehe 1/07/2009 **(Kiambatanisho Nam 26)**, ambapo katika Masharti ya kodi, Mkodishwaji ambae ni Zanzibr Data Com imekodi mnara huo wa Mtoni, ukiwa ni mali ya Shirika la Umeme kwa mnasaba wa masharti ya Mkataba na kulazimishwa kulipa kodi kwa kila mwezi.

Tunapenda tusisitize kwamba, kilichokodishwa kwa mnasaba wa Mkataba huu ni Mnara, hii ni kwa sababu wakati Kamati inafanya majadiliano na Uongozi wa Shirika, haikuwa rahisi kwa Uongozi huo kukiri kilichokodishwa, kwa mfano, Mwanasheria wa Shirika, Ndg. Abass Juma Faki alieleza zaidi ya mara moja kabla ya kuletwa Mkataba husika, kwamba wamekodisha huduma ya kuweka Mitambo tu ya mawasiliano ya Kampuni hii, bali si mnara uliokodishwa, kitu ambacho kwa kawaida huwa ni sehemu ya kuidanganya Kamati. Hebu na tujikumbushe maneno ya Mwanasheria huyo alipokuwa akitoa ufafanuzi husika kama ifuatavyo:

> *"Ule Mnara haujakodishwa ila Zanzibar Data Com kapewa 'access' ya kueka vyombo vyake na kwa hali hii, kaingia Mkataba na Shirika la Umeme kuweka vyombo hivyo"*

Kitu cha msingi katika Mkataba huo ni maslahi ya ukodishaji (*consideration*), ambapo kwa mujibu wa kifungu cha 2, Zanzibar Data Com inalazimika kulipia jumla ya USD 300, sawa na Tsh. 480,000 kwa mwezi na ni sawa na kulipia Tsh.

5,760,000/- kwa mwaka. Hata hivyo, kodi hii ilipaswa kubadilishwa kwa mnasaba wa mabadiliko ya soko na wakati husika, kwa kila baada ya miaka miwili, kwa makubaliano baina ya pande zote mbili, huku kiwango cha kodi husika, pia chaweza kubadilishwa kila mwaka. Na kwa sharti la kifungu cha 6 cha Mkataba husika, iwapo Mkodishwaji hatolipa kodi husika, Shirika litatoa taarifa kwake (notice) inayoelekeza malipo kufanyika (mara moja) na baada ya taarifa hiyo, Zanzibar Data Com inaposhindwa kulipa, Mkataba huu utakoma hapo.

1.8.2 Ukweli kuhusu Malipo:

Pamoja na masharti ya Mkataba kuelekeza hivyo, Kamati imethibitishiwa kwamba, Kampuni ya Zanzibar Data Com, haijawahi kulipia Mnara iliyokodishwa kwake tangu ulipoanza kukodishwa, na ni sawa na kusema kwamba, pamoja na Kamati kutakiwa zaidi kuangalia upotevu wa Upotevu wa fedha za Shirika unaotokana na uungwaji wa umeme unaofanywa na watendaji wasio waaminifu, katika suala hili, imejiridhisha kueleza wazi kwamba, Shirika hili limekuwa likipoteza mapato mbali mbali kwa kutosimamia ipasavyo majukumu yake kwa mnasaba wa Sheria na Mikataba mbali mbali inayoingia.

1.8.3 Hatua zilizochukuliwa dhidi ya deni linaotokana na kodi ya Mnara:

Jambo linalotarajiwa kwa Kampuni hii kutokana na tabia yake ya kutolipia kodi ya Mnara kwa Shirika, ni kuchukuliwa hatua za kisheria. Suala hili lilipoelekezwa kwa Uongozi wa Shirika wakati wa mahojiano na Kamati, Meneja Fedha, Ndg. Riziki Faki Hamad aliithibitishia Kamati kupitia barua ya tarehe 18/10/2011 yenye kumbu kumbu namba ZECO11/AC/VOL.I/10/08 ambayo katika ripoti hii tunaifanya **Kiambatanisho Nam 27,** aliimuandikia Meneja Utawala wa Shirika, kumtaka afuatilie deni hilo kwa kuchukua hatua kama zilizoelezwa na Mkataba wa ukodishwaji.

Katika barua yake, Meneja Fedha alilianisha deni kwa kuzingatia muda na uthibitisho wa Ankara ya kodi (Tax Invoice) (ambayo kwa wakati huo tarehe 18/10/2011 ilikuwa ni Tsh. 10,836,000/-)na namna gani Idara yake ilifanya juhudi za awali za kuwasiliana na Mkurugenzi Mtendaji wa Zanzibar Data Com, Afisa Mkuu wa Uendeshaji na hata Idara ya Fedha ya Kampuni, bila ya mafanikio yoyote. Na kwa hatua hii ya pili ya kulikabidhi deni hilo kwa Meneja Utawala wa

Shirika, ni dhamira ya wazi kwamba yeye sasa limemshinda na ni wajibu wa Meneja huyu wa Utawala kulisimamia kwa hatua yoyote ya kisheria.

Kwa hatua ya pili, Kamati ilitaka ufafanuzi iwapo kuna hatua nyengine yoyote iliyochukuliwa dhidi ya Kampuni hii na ndipo ilipobahatika kupewa barua ya tarehe 31/10/2011 yenye kumbu kumbu namba ZECO/CONF.5/VOL.111/483 aliyoiandika Meneja Mkuu wa Shirika kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Zanzibar Data Com, kumhimiza kulipa madeni yake kuanzia mwaka 2010 huku barua hiyo pia ikitumia kifungu cha 6 cha Mkataba kuwa ni taarifa (notice) (ingawaje kitendo cha taarifa hiyo kutolewa kwa kipindi cha siku saba, hakizuii matakwa ya Mkataba kuhusiana na kuweza kutolewa kwa wiki tatu) na kuwa ni dalili njema ya kuchukuliwa hatua za kisheria kwanza kwa kuanzia na masharti yaliyoelezwa katika Mkataba husika **(Kiambatanisho Nam 28).**

Hata hivyo, pamoja na barua hiyo, hakuna malipo yoyote yaliyofanyika, wala hatua zozote za kisheria zilizochukuliwa dhidi ya Kampuni hii, bila ya kujali hasara iliyokuwa inapata Shirika kwa kutoa huduma ya mnara bure huku na umeme nao ukiendelea kutumiwa na Kampuni hii, wakati kwa mwananchi mwengine mnyonge, ujeuri huu asingekuwa nao, kwa maana, Shirika huwa linasimamia taratibu zake dhidi ya wananchi wanyonge, huku Makampuni ya vigogo ama jamaa zao ama matajiri, zikiendelea kutumia huduma bure za Shirika.

1.8.4 Matumizi ya Umeme katika Mnara uliokodishwa:

Suala jengine muhimu kwa mnasaba wa Hadidu rejea iliyokabidhiwa Kamati na kwa maslahi ya ukodishwaji wa Mnara huu, ni huduma ya umeme inayotolewa kwa Kampuni kutoka Shirika la Umeme kama Mteja mwengine yoyote wa Shirika. Kwa lugha nyengine, ili kutoa huduma ya mawasiliano na kuvifanya vyombo vya Kampuni vilivyofungwa katika Mnara viweze kufanya kazi, Kampuni ya Zanzibar Data Com imeungiwa umeme katika Mnara huo iliokodishwa na Shirika na kwa kuzingatia hili, Kamati ilihitaji kujiridhisha kwamba taratibu zipi zilizotumika hadi Kampuni hii kuuingiwa umeme. Na kwa hili, ilielezwa kwamba, kama utaratibu ulivyo kwa wateja wengine, Kampuni hii iliomba kupatiwa huduma hiyo na taratibu zilifuatwa hadi kupata huduma. Hata hivyo, Kamati haikuweza kuthibitishiwa kwa maandishi, yaani, haikuweza kupatiwa taarifa za maombi, wala taarifa nyengine zinazohusika na kuuingiwa kwa umeme, na ni sawa na kusema,

faili la Kampuni hii litakalothibitisha uhalali wa njia zilizopitwa hadi kupata huduma ya umeme, halikupatikana.

Hata hivyo, Kamati kwa upende wake imekwishajiridhisha tokea awali kwamba, ufungwaji wa umeme katika mnara huo sio halali na haukufuata taratibu za kisheria.

1.8.5 Malipo ya Umeme unaotumiwa katika Mnara wa Mtoni:

Ili kupata ukweli kuhusiana na hoja hii ya Upotevu wa fedha za Shirika unaotokana na uungwaji wa umeme unaofanywa na watendaji wasio waaminifu, na kwa kuwa tayari tumeshakubaliana kwamba, Kampuni ya Zanzibar Data Com ni mteja mmoja kati ya wateja wengi wa Shirika la Umeme la Zanzibar, ni vyema tukajiridhisha iwapo mteja huyu kweli anatekeleza wajibu wake wa kulipia huduma ya umeme kama inavyotakiwa kwa mteja mwengine yoyote. Wakati Kamati inahoji hili, ilipata tabu kupata ukweli wa suala hili kwa sababu katika kikao cha awali cha mahojiano ya hoja hii, Shirika lilikuwa linaendelea na kikao cha Bodi ya Wakurugenzi, na hivyo Meneja Mkuu alikuwa katika Kikao hicho, huku baadhi ya watendaji ndio walioendelea na kazi za Kamati. Kamati haikupata jibu la moja kwa moja na kuonekana kusita ama kubabaika kwa watendaji wengi, ikiwa ni pamoja na Wanasheria wa Shirika. Hata hivyo, kwa kupitia taratibu ilizojiekea, hatimae Kamati ilipata ukweli wa suala hili kwa udhati wake.

Kama tulivyoeleza katika Mkataba, kwamba Kampuni hii imeingia Mkataba na Shirika kwa kukodishwa mnara tarehe 01/07/2009 na pia ieleweke kwamba, huduma ya umeme nayo imeanza kutolewa kwa mteja huyu tarehe sawa na Mkataba na pia ithibitike kwamba, ingawaje uthibitisho wa malipo yaliyofanyika yamethibitika kwa miezi miwili baada ya kodi ya Mnara wenyewe, yaani tarehe 01/09/2009 kupitia Cheki Namba 799547 na kuthibitika kwa risiti ya malipo ya 31/08/2009 kama uthibitisho huu unavyosomeka kuwa **Kiambatanisho Nam 29** katika ripoti hii, pia inakuwa vigumu kufahamu iwapo malipo hayo ya miezi miwili ya awali, yalikuwa ni kwa ajili ya mnara pekee ama ni pamoja na huduma ya umeme, huku Kamati ikipatiwa majibu ya malipo hayo ya awali, kama ni uthibitisho wa malipo ya Umeme, wakati huo huo ni malipo ya kodi. Hata hivyo, pamoja na malipo hayo ambayo ni sawa na miezi miwili ya awali, lakini tokea mwezi wa Septemba 2009 hadi hivi leo tunawasilisha ripoti yetu, Kampuni hii

haijawahi kulipia huduma hiyo ya umeme, na ushahidi huu sio tu kwamba umethibitishwa na Uongozi wa Shirika pekee, lakini pia hakuna ushahidi wowote mwengine uliopatikana kwa Kamati, ulio kinyume na ufafanuzi wetu huu.

Kwa maana hii, ni sawa na kusema kuwa, kwa kuwa hakuna uthibitisho wa kufuatwa ipasavyo taratibu za kuungiwa kwa umeme kwa Kampuni hii na kwa kuwa Kampuni hii imesita kulipa deni lake la kila mwezi mbali na kutakiwa kulipa deni hilo na kwa kuwa bado Kampuni hii inaendelea kupata huduma za umeme kama wateja wengine wa Shirika, Kamati imejiridhisha kwamba kuna upotevu mkubwa wa fedha za Shirika ambao sio tu kwamba unaotokana na uungwaji wa umeme unaofanywa na wateja wasio waaminifu, lakini pia unasababishwa na upendeleo na kukiukwa kwa sheria zinazohusiana na masuala haya.

1.8.6 Utumiaji wa huduma ya umeme katika mnara wa kampuni ya Zanzibar Data com, Masingini-Unguja:

Mbali na kukodi mnara wa Mtoni kama tulivyoeleza hapo juu na malipo ya Umeme katika Mnara huo, Kampuni hii pia imekodi mnara katika maeneo ya Masingini, ingawaje mnara huu hauko katika milki ya Shirika, lakini huduma ya umeme inayopatikana kwa Kampuni hii katika kuendeshea mitambo yake ya intaneti katika mnara huo, inatolewa na Shirika. Ilielezwa Kamati kwamba, hapo kabla, Kampuni ilikuwa inatumia umeme wa ‘Three Phases’ umeme unaotumiwa na wateja wakubwa wa Shirika, lakini kutokana na tabia yake ya kutoulipia umeme huo, Shirika baadae liliamua kumpatia umeme wa ‘Single Phase’ unaotumiwa hata na wateja wadogo wa Shirika.

Tunataka kwanza ifahamike kwamba, Mteja huyu mbali na kupatiwa umeme huo, hakua akilipa ipasavyo, na kwa hali hii, lile deni lake alilokuwa anadaiwa katika matumizi ya umeme mkubwa (Three Phases), lilihamishiwa katika huduma mpya ya Single Phases. Pamoja na juhudi hizi, zikiwa ni sawa na kumkumbusha wajibu wake wa kulipia huduma ya umeme, Kampuni hii haikuona haja ya kulipia, mbali na kuendelea kupatiwa huduma hiyo, na ilipofikia deni kuwa kubwa, Shirika liliamua kukata huduma ya umeme kwa Kampuni.

Baada ya hatua hii, Kamati ilielezwa kwamba, Uongozi wa Kampuni uliomba kupatiwa umeme kutoka katika minara ya jirani, ikiwa ni pamoja na Mnara

uliokodishwa kwa Kampuni ya Mawasiliano ya Tigo, lakini ilikataliwa kwa sababu Kampuni hii ya Tigo ilikuwa inajua wajibu wake kisheria kwamba, wao kwa kuwa wateja wa Shirika la Umeme la Zanzibar, hawana uwezo wa kumruhusu mtu ama taasisi wala Kampuni yoyote kutumia umeme kinyume na taratibu zilizowekwa. Jambo la kushangaza wakati Kamati inafanya ziara katika eneo la tukio, ilikuta Kampuni hii inatumia umeme kutoka Mnara wa Shirika la Utangazaji la Zanzibar(kama ilivyokuwa inafahamika kwa jina la TVZ), Shirika ambalo bajeti yake inapitishwa kupitia pesa za walipa kodi na kuidhinishwa Baraza la Wawakilishi. Tena basi, Taasisi hii ni ya Serikali iliyokubali kutoa huduma ya umeme kwa Kampuni binafsi, kinyume na taratibu za kisheria na taratibu za Shirika la Umeme.

Kwa kufahamu hili na kupewa maelezo na Shirika juu ya tabia ya mteja huyu, na kwa kuwa umeme huo alioungiwa na Shirika la Utangazaji la Zanzibar (TVZ) unatokana na waya uliotoka katika Mnara wa Kampuni hii hadi katika plagi ya kibanda cha Mnara wa Shirika la Utangazaji(TVZ), Kamati iliagiza kukatwa kwa waya huo kwa lengo la kusitisha huduma ya wizi iliyokuwa inaendelea, huku Shirika la Umeme likijitazimia kwa muda mrefu bila ya kuchukua hatua zozote muwafaka.

Jambo lililoshangaza, siku ya pili ama ya tatu, mteja huyu karejeshewa huduma ya umeme, huku Kamati ilipokutana na Uongozi wa Shirika la Umeme ilielezwa kwamba, amefungiwa mita ya TUKUZA na deni lake limehamishiwa katika mita hiyo. Hali hii, ilileta masuala mengi kwa Kamati, juu ya nani alieruhusu kurejeshewa umeme, lakini kabla ya kufanya uchunguzi wake kwa kina, iliona busara kwanza kumwita Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji la Zanzibar, kwa ajili ya kufanya mahojiano nae, kwa nini airuhusu Kampuni binafsi kutumia huduma ya umeme bure huku gharama za malipo hayo zikilipwa na Taasisi yake ya Serikali kupitia fedha za walipa kodi wanyonge wa nchi hii.

Kwa bahati mbaya, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji hakuweza kuhudhuria katika kikao hicho kutokana na dharura ya safari ya kikazi na hatimae aliwakilishwa na Kaimu Mkurugenzi, Ndg. Rafii ambae alikiri kulifahamu tatizo hilo na alieleza kwamba, kwa mujibu wa taarifa za mafundi wao, tatizo hilo lilianza tokea January 2012, ingawaje yeye alilitambua tatizo hilo kuanzia tarehe

09/05/2012, baada ya Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Mhe. Said Ali Mbarouk, kutembelea eneo hilo ambapo nae pia kama ilivyofanya Kamati, aliagiza kukatwa kwa huduma hii ya wizi, kinyume na taratibu dhidi ya Kampuni ya Zanzibar Data com. Hata hivyo, Kamati ilijuilishwa na Uongozi wa Shirika la Utangazaji kwamba, hawakuukata umeme huo kama Waziri wao alivyoagiza, kutokana na kuona ipo haja ya kumshauri kwanza kuangalia taratibu za kisheria juu ya suala hilo.

Wakati Kamati inafanya mahojiano na Fundi wa Shirika la Utangazaji, aliefuatana na Kaimu Mkurugenzi na watendaji wengine, aliieleza Kamati kwamba, alilifahamu tatizo hilo tokea Januari 2012 kwani Uongozi wa Kampuni ya Zanzibar Data Com, kwanza ulimfuata yeye na kumtaka awaungie, ingawaje aliwaeleza kwamba yeye hana mamlaka ya kufanya hivyo, na hatimae Kampuni hii ulimfuata Mkurugenzi wa Shirika la Utangazaji na kumuomba kuwasaidia kutekeleza azma yao. Kamati iliona haja iutambue Mkataba wowote ulioingiwa baina ya Kampuni hii na Shirika la Utangazaji kuhusu kuungwa kwa umeme huo, lakini ilithibitishiwa kwamba, hakuna Mkataba wowote uliopo, ingawaje ilielezwa kwamba, ruhusa hiyo ambayo inakiuka taratibu za kisheria na wizi wa mapato ya Serikali, ilitolewa kwa meizi mitatu tu, kuanzia Januari hadi Machi, 2012, ingawaje hadi Kamati inafika tarehe 14/05/2012, bado Kampuni inaendelea kujipatia huduma hiyo bila ya malipo.

Wakati Kamati inahoji angalau makisio ya kawaida ya matumizi ya umeme huo kuanzia January, ilielezwa kwamba, kwa kila siku Kampuni hii ilikuwa inatumia baina ya Units 10 hadi 250, na makisio ya Tsh. 375,000/- zilipaswa kulipwa ambazo zimeshapotea bila ya uwezo wa kulipwa kwake kwa Shirika la Umeme. Kwa mnasaba huu, Kamati ilendelea kuhoji juu ya sababu zilizopelekea kurejeshewa umeme kwa Kampuni hii, na kupewa barua iliyotoka kwa aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Umeme, Ndg. Moh'd Hashim Ismail, ya tarehe 11/04/2012[2], na kupokelewa tarehe 11/05/2012 iliyoagiza la kurudishiwa huduma ya umeme kwa Kampuni ya Zanzibar Data Com **(Kiambatanisho Nam 30)**.

[2] Tarehe ya barua hii imekosewa, kwani ilitakiwa iwe 11/05/2012, badala ya mwezi wa April, kama inavyosomeka.

Kufuatia hatua hii, Kamati ilimwita aliyekuwa Mwenyekiti huyo wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika na kumtaka aote ufafanuzi juu ya uwezo alionao kisheria kuagiza kurudishiwa kwa huduma ya umeme kwa Kampuni iliyokuwa hailipi umeme huo na kuupata kupitia njia za wizi. Aidha, Kamati ilimtaka aeleze sababu zipi zilizompelekea kuamuru ama kutoa agizo hilo na yeye alikiri kwamba ameagiza kwa njia ya barua na kueleza sababu kubwa eti ni kipaumbele kinachotakiwa kupewa kwa wawekezaji, yaani Kampuni ya Zanzibar Data Com ni mwekezaji na akipatiwa umeme, na kwa kutumia umeme asioulipia mapato ya Serikali yataongezeka. Ni kichekesho, lakini ni aibu kwa maneno hayo kutamkwa na mtu kama yeyé mwenye dhamana kubwa ya kuwa msimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya Nchi. Ukiachilia mbali dhamana ya uenyekiti wa Bodi ya Shirika la Umma (Serikali).

Hoja hizi zote hazina mashiko mbele ya Kamati, kwanza Kamati inaamini Mwenyekiti huyu hana mamlaka ya kuagiza kurejeshewa umeme mteje yoyote anaekiuka taratibu za Sheria. Wala maamuzi aliyoyatoa ama agizo halina uhalali kisheria. Tunasema hivi kwa sababu Mwenyekiti alipotoa agizo hilo, alilitoa kama yeye (in persona) wala hajalitoa kwa kupitia Bodi ya Wakurugenzi, na hata kama angelipita kwa Bodi, ingekuwa ni sawa na kutumia mamlaka isiyopewa kisheria. Aidha, hoja ya kuongeza mapato ya Serikali kwa kutumia mgongo wa cheo alichokuwa nacho cha Kamishna, Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), kwa makusudi na kuruhusu kupotea kwa mapato ya Shirika la Umeme, ambayo pia ni mapato ya Serikali, ni suala lisilo kubalika na linaonesha wazi kwamba, Ndg. Moh'd Hashim hakuwa na mapenzi ya dhati ya Shirika na alikitumia cheo chake cha Uenyekiti kwa manufaa yake binafsi na manufaa ya Makampuni machache ya kibiashara, huku Shirika likiendelea kukosa mapato na kuwa katika hali mbaya ya kiuchumi na kupoteza imani yake kwa wananchi.

Unaweza sasa kujiuliza, jee hilo deni lililokuwa linadaiwa kwa Kampuni ya Zanzibar Data Com iliyojiungia umeme kinyume na taratibu za Sheria za Shirika na kubebwa na Viongozi wa juu wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika, jee limekwenda wapi? suala hili lilijibiwa kwamba, baada ya kutoka kwa agizo la aliekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Uongozi wa Shirika ulimrejeshea Kampuni ya Zanzibar Data Com huduma hiyo kwa kumuungia mita ya TUKUZA

na kumhamishia deni lake alilokuwa anadaiwa hapo awali, katika mita hiyo mpya na kumtaka kulipa kila mwezi pamoja na deni lake la awali.

Pamoja na uzuri wa maelezo haya, Kamati imejiridhisha kwamba, hatua hii iliyochukuliwa kwa Kampuni hii ni upendeleo ulio wazi na haina imani kwamba deni hilo litalipwa kwa muda mfupi, ukizingatia tabia ya Kampuni hii kutolipa katika madeni yote inayodaiwa na Shirika.

1.9.0 Wateja wa Minara ya Simu:

Kama tulivyokwisha eleza awali kwamba, miongoni mwa wateja wakubwa wa Shirika ni pamoja na Kampuni za minara ya simu, ikiwa ni pamoja na Zantel, Tigo, TTCL na Celtel. Pamoja na ukweli kwamba, Kampuni hizo ni chache, kwa upande wa kila Kampuni inamiliki vituo kadhaa vya minara, na kila mnara unatakiwa kuwa na umeme wake unaojitegemea. Hivyo, kwa tafsiri hii, kila mnara ni sawa na mteja halisi, mwenye kuhitaji umeme kwa kutumia mita yake, nguzo zake na hata transfoma ya kwake pekee.

Hivyo basi, katika idadi kamili iliyowasilishwa kwa Kamati, jumla ya vituo vyote vilikuwa ni 106, vilivyomilikiwa na Makampuni hayo tofauti tuliyokwishayaeleza, ingawaje Kamati imepata taarifa ya mafaili yasiyozidi 10 tu ya vituo vyote hivyo, huku jawabu ni ile ile kwamba yamerowa kwa mvua. Tunachotaka kusema kwa ujumla wake katika kipengele hiki ni kwamba, wateja hawa wanafanana sana na Makampuni ya Mahoteli tuliyoyaeleza hapo juu, huku taratibu za maombi na hatimae kupatiwa huduma ya umeme ni hizo hizo.

Tumeona vyema na kutayataja mapungufu yaliyomo kwa ujumla wake, bila ya kulazimika kutaja Kampuni ama kituo kimoja kwa kingine. Na hivyo, ni sawa kufahamu kwamba, kazi hii kwa mujibu wa taarifa zilizofika kwa Kamati, hufanywa na Shirika la Umeme, lakini pia na Kampuni binafsi ikiwa ni pamoja na Kampuni ya GECCO. Yaani, pamoja na Sheria kuwataka Shirika pekee kuhusika na kazi ya ufikishaji wa huduma ya umeme kwa wananchi, kazi hizo zimekuwa zikifanywa pia na Kampuni binafsi kinyume na sheria.

Mara nyengine hutokea Kampuni husika kuomba kibali hicho kwa Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme, (kama ilivyofanyika kwa Kampuni ya Pomy Engineering Company Ltd, **Kiambatanisho Nam 31**), jambo ambalo sio tu linakiuka Sheria,

lakini pia hupoteza mapato ya Shirika na kama kazi hizi zingelikuwa zinafanywa na Shirika pekee, kama maelekezo ya Sheria Nam. 3 ya mwaka 2006, basi lingeliweza sana kutotekeleza majukumu yake kwa udhati wa maslahi na ustawi wa wananchi.

Mfano halisi unaweza kuupata kwa kufanya rejea ya Kituo cha Zantel kilichopo Mpendae ambacho hata Akaunti yake haionekani katika tarifa zilizomo kwenye FORM B, pamoja na kwamba hakuna maombi yoyote yaliyofanywa na Kampuni ya Zanteli katika kupatiwa huduma ya umeme kwa matumizi ya umeme wa kituo hicho, na pamoja na ukweli kwamba, fomu ya Usajili iliyomo katika taarifa za mteja huyu haijajazwa taarifa kamili wala hazina uthibitisho wa saini kuthibitisha kweli maombi yalifanywa ama malipo husika **(Kiambatanisho Nam 32),** bado mteja huyu ameweza kulipia Tsh. 1,096,184.16 kwa ajili ya kuweka Transfoma na kujenga laini ya phase 3 na kazi nyengine zinazohusika ikiwa ni pamoja na malipo ya kazi.

Sasa chukua mfano huu tu kwa vituo vyote 106 vya Minara ya Simu Unguja pekee, ni sawa na kusema kwamba Shirika lingeliweza kuingiza jumla ya Tsh. 116,195,520.96 kwa wateja wanne tu wa Kampuni za Simu, mbali na wateja wengine. Lakini kwa kuwa kazi hii hufanywa pia na Makampuni binafsi, tena msisitizo ukiwekwa kwa Kampuni ya GECCO ambayo wamiliki wake na wafanyakazi wake ni wafanyakazi wa Shirika, ni sawa na kusema, upotevu huu wa makusudi utaendelea kuwepo, kwa sababu ya mgongano wa kimaslahi uliopo.

1.10.0 Akaunti za Shirika upande wa Tawi la Pemba vipi zinahusika na upotevu wa fedha za Shirika:

Katika kupata uthibitisho zaidi wa vipi fedha za Shirika zinapotea, Kamati imeona ni vyema kuangalia kwa kina kuhusiana na ‘Accounts’ za Shirika, na imeonekana mfano mzuri wa kuzungumzia suala hili, ni ‘Accounts’ za Shirika, upande wa Tawi la Pemba. Kuhusiana na idadi ya ‘Accounts’ za Tawi la Pemba, Kamati imeelezwa kwamba, Shirika lina idadi ya ‘Accounts’ 3. ‘Account’ namba 162 inahusiana na Mishahara ya Wafanyakazi wa Shirika, Tawi la Pemba. ‘Account’ hii huingiziwa fedha zake kutoka Makao Makuu ya Shirika, Unguja, na huiwezesha Afisi ya Pemba kujiendesha kwa kuwalipa wafanyakazi wake mishahara yao ya kila mwezi.

Aidha, ‘Account’ ya 2 ni Namba 163, hii hutumiwa kwa kulipia malipo ya TANESCO kwa umeme unaotumiwa, Pemba. Na ‘Accout’ ya 3 ni Namba 173 ambayo inahusika na Matumizi Mengineyo (Other Charges), na kwa ufupi, shughuli za kila siku kwa upande wa Pemba fedha zake hutokana na ‘Account’ hii Namba, 173. Baada ya kupata maelezo hayo, Kamati ilihitaji kupewa utaratibu wa vipi fedha za ‘Account’ hii zinapatikana na kuelezwa kwamba, mara tu baada ya mauzo ya umeme kupitia utaratibu wa kawaida (Post Paid), na fedha hizo kupokelewa na Muuzaji (Cashier), kupitia Makao Makuu ya Shirika, na baadae, pamoja na kufanya migawanyo mengine, ‘Account’ hii nayo huingizwa fedha kwa ajili ya matumizi ya Pemba.

Kwa kawaida, kabla ya mwaka 2010, utaratibu uliokuwa unatumika ni wa ‘Petty Cash’ yaani fedha hizo hupelekwa Pemba kwa njia ya ‘Cheque’ ya matumizi madogo madogo, zilizokuwa hazizidi 500,000/- na baada ya Tawi la Pemba kufanya matumizi ya fedha hizo, vilelezo vya matumizi hayo hurejeshwa Makao Makuu ya Shirika, Unguja. Hata hivyo, sababu kubwa iliyotajwa ya kulifanya Shirika hili Pemba kupokea fedha hizo kwa njia ya ‘Petty Cash’ ilikuwa ni kukosekana kwa Mhasibu wa Shirika, upande wa Pemba, na hatimae kuanzia mwaka 2010, baada ya kuajiriwa kwa Mhasibu huyo, fedha hizo ndio zimefunguliwa ‘Account’ Namba 173. Mara tu baada ya kufunguliwa kwake, mnamo mwezi wa Agosti, 2010 jumla ya Tsh. 5,000,000 zimeingizwa katika ‘Account’ hii.

Hata hivyo, kuanzia Tarehe 25/08/2010, ‘Account’ hii imeendelea kuingiziwa Tsh. 1,000,000/- kwa kila siku, utaratibu ambao umeendelea hadi tarehe 02/03/2011 ndipo ilipoanza kuingiziwa Tsh.2,000,000/- kwa kila siku ya mauzo. Jambo kubwa lililosisitizwa kwa Kamati, ni kufahamu hali halisi ya mauzo, kwamba fedha hizo zinaweza kushuka chini ya kiwango hicho cha kila siku, pale ambapo mauzo ya umeme hayakuwa mazuri. Ila ifahamike pia kwamba, makusanyo ya fedha hizo kwa utaratibu huu, ni tofauti na utaratibu wa awali wa ‘Petty Cash’, ambapo matumizi ya fedha hizi baada ya kufunguliwa ‘Account’ yake, yalitakiwa yakaguliwe na Mkaguzi wa Ndani, pamoja na Mkaguzi wa Nje.

Jambo la kusikitisha, matumizi ya fedha hizo hayajakaguliwa na Mkaguzi wa Ndani, na Kamati ilipohoji suala hili ilielezwa kwamba, Shirika la Umeme kwa

muda mrefu lina Mdhibiti mmoja tu wa Ndani, nae yupo Makao Makuu ya Shirika, Unguja na huenda Pemba mara moja angalau kwa miezi mitatu. Pamoja na melezo hayo, Kamati imejiridhisha kwamba, matumizi ya fedha hizo hayajakaguliwa hata mara moja na Mdhibiti wa Ndani, jambo ambalo linapelekea upotevu wa fedha husika.

Lakini unafahamu kilichomsibu Mkaguzi wa Ndani wa Shirika ambae kabla ya Kamati hii kuanza kazi zake, alikwisha sibiwa na uhamisho usio na sababu za msingi, eti tu ameshauri ipasavyo juu ya matumizi halisi ya Shirika kwa mnasaba wa Sheria? Basi ni vyema ukapata ufafanuzi huu:

> "Ndg. Mohammed Khamis Juma (Kilindi), ni Mfanyakazi wa Shirika aliekuwa akifanya kazi za Ukaguzi wa Hesabu za Ndani (Internal Auditor) Tawi la Shirika Pemba. Mnamo tarehe 14/04/2012 alilishauri Shirika kuwa na utaratibu mzuri wa matumizi ya fedha zake, huku akionesha mapungufu kadhaa katika ripoti yake hiyo. Alimuandikia Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme na nakla ya ripoti hiyo ambayo hapa tunaifanya ni **Kiambatanisho Nam 33**, alitoa ushauri wa kina kupitia Idara zote za Shirika, ikiwa ni pamoja na Idara ya Fedha, Biashara, Utawala na Uendeshaji, kwa lengo la kuboresha utendaji wa Shirika, katika suala zima la matumizi ya rasilimali fedha za Shirika"

Jee, unajua kilichompata Mfanyakazi huyu, Kamati imethibitishiwa kwamba Meneja Mkuu wa Shirika, badala ya kuupokea na kuufanyia kazi ushauri wa kitaalamu wenye ukweli na nia safi ya kuendeleza Shirika, alichoamua yeyé na Menejimenti yake ni kumpa uhamisho wa kumleta Unguja, bila ya kumpangia kazi yoyote ya maana yenye kuendana na ujuzi wake, huku akiacha nafasi ya Mkaguzi wa Ndani Pemba, ikiwa tupu bila ya kujali umuhimu wa nafasi hiyo katika suala zima la kutunza rasilimali za Shirika. Kwa hali hii, nani atakaepinga kwamba, Meneja huyu badala ya kuwa na mawazo ya kuliendeleza Shirika, yeyé badala yake anajenga mazingira ya kulibomoa na kuendeleza matumizi holela ya fedha za Umma.

Kamati imeendelea kuelezwa kwamba, kwa matumizi yanayofanywa kupitia 'Account' hii hayazidi Tsh. 5,000,000/ kwa Vocha moja, na ikitokea matumizi hayo yanazidi fedha hizo, ni lazima Meneja wa Tawi Pemba, aombe idhini kutoka

kwa Meneja Mkuu wa Shirika, Unguja. Uongozi wa Shirika, umeendelea kutetea haja ya kuwepo kwa 'Account' hii kwa kueleza kwamba, hapo kabla ya kuanzishwa kwake, mapungufu ya fedha kupitia 'Petty Cash' yalikuwa yanaonekana wazi na udhibiti wa fedha hizo ulikuwa mdogo zaidi. Kwa mfano, ilielezwa pia kwamba, matumizi hayo yalikuwa shaghla baghla, mara saini ya matumizi yake yanafanywa na aliekuwa Afisa Tawala, Ndg. Shaibu Kaduara, Bi Msufe na wengineo.

1.10.1 Uchunguzi wa 'Account' Namba 173:

Pamoja na maelezo mazuri na yakusifu yaliyotolewa na Uongozi wa Shirika, Kamati ilitaka kujiridhisha namna matumizi ya 'Account' hii yanavyodhibitiwa na hatimae imefanya uteuzi wa miezi mitatu tu tokea kuanzishwa kwake, yaani kuanzia August, Septemba na Octoba 2010. Vile vile imechagua baadhi tu ya hati za malipo, ili kufanya 'Sampling' ya namna gani matumizi ya 'Account' hiyo yanavyofanyika na iwapo yanafuata taratibu za Sheria za Fedha.

1.10.2 Uchunguzi wa Hesabu kwa mwezi wa Agosti hadi Oktoba, 2010:

Kamati ilielezwa kwamba, wakati Mhasibu wa Shirika, Tawi la Pemba Ndg. Salma Juma Said, alipoajiriwa, kwanza alilazimika kubakia Makao Makuu Unguja kwa mwaka mmoja, akipewa uzoefu wa kazi zake, kwa hoja kwamba, mbali na kuajiriwa kama Mhasibu wa Shirika kwa kuzingatiwa elimu yake, Mhasibu huyu alikuwa hana uzoefu wowote wa kazi (Fresh from School) na kwa kuwa Shirika lina utaratibu wake wa masuala ya fedha, Mhasibu alibakishwa Unguja kwa kupewa mafunzo madogo madogo na uzoefu wa kazi.

Wakati Mhasibu huyu alipohamishiwa Pemba, kama ilivyokusudiwa tokea mwanzo wa kuajiriwa kwake, alikabidhiwa Tsh. 470,541.25 zilizokuwemo katika Account hiyo na kuanzia tarehe 26 hadi 31/08/2010, 'Account' hiyo ilikuwa na Tsh. 7,470,541.25 na baada ya maelezo haya, Kamati ilitaka kujiridhisha juu ya matumizi ya Tsh. 7,470,541.25 na ilielezwa kwamba, matumizi halisi ya fedha hizo kwa mwezi huo, ilikuwa ni Tsh. 6,357,400/- **(Kiambatanisho Nam 34)**, huku kukiwa na bakaa la Tsh. 1,113,141.25/-. Aidha, katika uchunguzi wake, Kamati imeangalia namna gani taratibu hizo za fedha zinafuatwa kwa kuchukua mfano wa baadhi ya Hati za Malipo (Payment Vouchers), ili kujiridhisha iwapo huandaliwa

kwa taratibu za sheria, lakini pia kwa kuangalia vielelezo vyake kama vimekamilika ama laa, ili kujiridhisha kwa kiasi gani Sheria za Fedha na Kanuni zake zinavyoelekezwa ipasavyo.

Katika kupitia hati za malipo zinazohusiana na Ulinzi wa kituo cha Umeme cha Mnyanjani, Tanga, Kamati imepitia Hati ya malipo ya tarehe 28/09/2010 ambapo Shirika limekubaliana na Kampuni binafsi ya ulinzi ya 'Sunshine General Security Services' kupatiwa huduma ya ulinzi katika kituo chake cha umeme kilichopo Tanga, na Kamati imejiridhisha kuwemo kwa barua ya maombi, 'invoice' pamoja na 'Chaque' ya malipo hayo kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar. Hata hivyo, Kamati imeshindwa kupata risiti za mapokezi ya malipo yaliyofanywa na ni sawa pia kwamba imekosa kupata maelezo ya Benki (Bank Statement).

Jambo kubwa zaidi ambalo halivumiliki, ni kukosekana kwa Mkataba ulioingiwa baina ya Shirika na Kampuni hii ya ulinzi. Kwa maana nyengine, mbali na Mkataba kuwa kielelezo muhimu cha kuthibitisha malipo yaliyofanyika, katika hati hii umekosekana na Uongozi wa Shirika umekiri kutokuwepo kwa Mkataba Pemba, na ukasema yawezekana upo Unguja, lakini mpaka tunaandika ripoti hii, Uongozi wa Shirika umeshindwa kuithibitishia Kamati kuwepo kwa Mkataba huo **(Kiambatanisho Nam 35).**

Katika kuendelea na ukaguzi wa baadhi ya Hati za Malipo, Kamati imeikagua Hati namba 30 ya tarehe 20/09/2010 inayohusu nauli ya siku 2 kwa ajili ya safari ya Unguja **(Kiambatanisho Nam 36)**. Kwa mujibu wa hati hiyo ya malipo na maelezo yaliyotolewa kwa Kamati, Ndg. Ali Nassor Moh'd, Mfanyakazi wa Shirika la Umeme, Tawi la Pemba, alipata safari ya kikazi, kwenda Unguja kwa muda wa siku 2, na hivyo, aliombewa posho la safari na nauli ya kwenda na kurudi Pemba, jumla ya Tsh. 340,000/-, Nauli ikiwa ni Tsh. 80,000 na posho la kujikimu ni Tsh. 260,000/-. Pamoja na hali hii, kwa kawaida, inatarajiwa kuwepo kwa vielelezo vya kuthibitisha matumizi ya fedha hizo. Moja kati ya kosa lililofanyika ni kutokuwepo kwa hati yoyote inayoonesha kupokelewa kwa posho la siku 2. Vile vile vielelezo vya tiketi za kusafiria ni vya udanganyifu. Kwa mfano, Uongozi uliieleza Kamati kwamba, Ndg. Ali Nassor Moh'd alitumia Meli ya Mv. Maendeleo kwenda Unguja. Hata hivyo, Tiketi hiyo yenye namba 72442 ina jina la Msafiri Ndg. Rahma Abdalla na sio ya Mfanyakazi huyu.

Aidha, Tarehe ya kusafiri iliyomo katika tiketi hiyo ya MV Maendeleo ni 16/10/2010 wakati barua ya maombi ya safari yenyewe ilikuwa ni Tarehe 17/09/2010 na Tarehe ya malipo kwa mujibu wa vocha hiyo ni 20/09/2010. Kwa namna yoyote ile iwayo, tiketi hii ni ya udanganyifu. Sambamba na hilo, Kamati ilielezwa kwamba, Ndg. Ali Nassor Moh'd alisafiri kwa Boti ya Mv.Sepideh akitokea Unguja na kurudi Kisiwani Pemba. Hata hivyo, kwa mujibu wa tiketi hiyo, Boti hiyo ilisafiri kutoka Zanzibar hadi Dar es Salaam na sio Pemba kama ilivyoelezwa. Mbali na hayo, Kamati pia imegundua kwamba, tiketi hiyo ni ya Tarehe 3/09/2010, ikiwa ni tofauti kubwa na Tarehe ya maombi ya fedha zenyewe. Kibaya zaidi, tiketi hiyo ya kutoka Unguja kwenda Pemba, imekatwa Pemba badala ya Unguja.

Pamoja na kasoro hizo, jambo lililoishangaza Kamati hii ni kukuta wino wa rangi ya kijani, wenye ishara kwamba, tayari vocha hizo zimeshakaguliwa na Ofisa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Suala hili linatia mashaka sana na linahitajiuchunguzi wa kina zaidi. Kwa bahati mbaya, Kamati haikufanikiwa kukutana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ili kujiridhisha iwapo alama hizo zina maana ya kukaguliwa na yeye ama Ofisi yake au laa.

Aidha, Kamati imepitia Vocha Namba 15 ya Tarehe 08/09/2010 inayohusu malipo ya fedha kwa ajili ya Wasafishaji kwa mwezi wa Julai na Agost, 2010. Malipo ya Vocha hiyo ya Tsh. 711,000/- yamelipwa kwa Wasafishaji kwa miezi ya Julai na Agost, 2010, ambao ni Ndg Hamisa Subeit Kamna; Ndg Mashavu Mwalim Bilal; Ndg Ali Makame Ali ; Ndg Bimkubwa Ramadhan ; Ndg Raya Kombo Suwedi na Ndg Omar Salim Omar **(Kiambatanisho Nam 37)**. Maombi pekee yanayohusika kwao ni kuhusu malipo ambapo barua zao zimeandikwa na Ndg. Sufe M.Nassor, Mwangalizi wa Ofisi ya Shirika, Tawi la Pemba kumuomba Meneja wa Tawi kufanya malipo husika kwa kila Msafishaji. Ilitarajiwa katika vocha hii, kuwemo barua ya maombi ya wasafishaji husika, kitu ambacho kimekosekana. Aidha, hakuna ushahidi wa kimaandishi wa kupokelewa kwa fedha hizo, jambo ambalo linapokosekana, huleta utata mwingi wa kisheria.

Kwa maana nyengine, Kamati imekosa vielelezo vya kuthibitisha iwapo watu hao wamelipwa, lakini pia imekosa kujiridhisha namna yao walivyopatikana na

hatimae kupewa kazi hizo ambazo kwa kawaida za taratibu za Kiserikali, wanaotaka kazi hizo hupeleka maombi yao kwa Taasisi inayohusika.

Kamati pia ilifanya ukaguzi wa Vocha Namba 47A ya tarehe 27/10/2010[3] inayohusiana na malipo ya fedha kwa ajili ya ulinzi wa vituo vya Umeme vilivyopo Pemba, kwa mwezi wa Oktoba, 2010 **(Kiambatanisho Nam 38)**. Kwa ujumla katika Vocha hii, imeambatanishwa na 'Invoice' pamoja na risiti za malipo, walizolipwa Kikosi cha Valantia cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikifuatiwa na barua ya maombi ya fedha Tsh. 2,550,000/- kutoka kwa Ndg. Shaib H. Kaduara. Wakati Kamati inaipitia Vocha hii, kwanza imeshindwa kuthibitisha uhalali wa maombi ya fedha hizo, ingawa zimefanyiwa maombi. Yaani, aliyomba na kuidhinisha fedha hizo ni mtu mmoja, yaani Meneja wa Tawi, Pemba.

Tunakusudia kusema, barua hiyo ya maombi ya fedha imeombwa kwa niaba ya Meneja wa Tawi, na aliyeombwa ni huyo Meneja wa Tawi, jambo ambalo kihesabu na taratibu zake, huleta mashaka kadhaa.

Mbali na hilo, tatizo kubwa ambalo Kamati inaliona katika uhalali wa malipo yanayofanyika, ni risiti za mapokezi ya fedha hizo zinazotolewa na Kikosi cha Valantia (Rejea Kiambatanisho hiki). Kikosi cha Valantia, kikiwa ni kimoja kati ya Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kinapaswa kutoa risiti za Serikali ili kuthibitisha mapokezi ya fedha juu ya huduma za ulinzi wanazozitoa, lakini pia kuthibitisha uhalali wa mapato hayo kuingia katika Mfuko wa Serikali, kama zilivyo taratibu. Kwa kuwa Kikosi hiki hutoa risiti sawa na zile zinazopatikana kwa wauzaji wadogo wadogo wa mchele mitaani, Kamati imeshindwa kujiridhisha iwapo kuna uhalali wa malipo yaliyofanyika, lakini picha inayojengeka ni kuvuja kwa mapato hayo.

Mbali na hayo,Kamati ilitaka kujiridhisha iwapo kuna Mkataba wa kisheria ulioingiwa baina ya Kikosi cha Valantia na Shirika la Umeme. Na kwa bahati njema, ilikabidhiwa Mkataba huo wa miezi 6 na kusainiwa tarehe 09/10/2010, ingawaje Mkataba huo umeanza tarehe 01/10/2010. Aidha, Kamati pia ilipatiwa Mkataba mwengine uliotiwa saini Tarehe 31/03/2011, ingawa umeanza Tarehe 01/05/2010, kwa lengo la kubadilisha kiwango cha malipo ya kutoka kile cha awali

[3] Tarehe ya Vocha hii imekosewa, yaani imeandikwa 27/06/2010, wakati inahusika na mwezi wa October, 2010.

cha Tsh. 85,000/- kwa mwezi kwa kila mlinzi kati ya walinzi watano waliohusika, na badala yake kuwa Tsh.120,000/- kwa masharti hayo hayo. Pamoja na kuwepo kwa Mkataba huo uliohitajika na Kamati, Kamati imekuwa na wasi wasi na usahihi wa Mikataba hiyo kisheria, kwa kile kinachoelezwa kutiwa saini na Meneja wa Tawi, Pemba, ikiwa ni yeye mwenyewe ama Ofisa mwengine kwa niaba yake, jambo ambalo kisheria halikupaswa kufanywa isipokuwa na Meneja Mkuu wa Shirika hili, ambae yuko Unguja.

Vocha nyengine iliyoangaliwa na Kamati ni hii ya Tarehe 27/10/2010[4] inayohusu posho la wiki mbili kwa ajili ya kushiriki mafunzo, Unguja, ambalo walilipwa Ndg Ali Moh'd Ali na Ali Nassor Ali, wafanyakazi wa Shirika la Umeme, Pemba. Wafanyakazi hawa walilipwa Tsh. 3,800,000/- ikiwa ni posho la Tsh. 1,900,000/ kwa kila mtu, huku gharama za usafiri zikiwa ni Tsh. 160,000/-. Kamati imegundua kwamba, matumizi ya fedha hizo hayakuwa sahihi kwa sababu ya kupatikana kwa vielelezo vya udanganyifu vilivyoambatanishwa na vocha hiyo. Kwa mfano, wakati Kamati inakagua tiketi za safari, ili kujiridhisha iwapo wafanyakazi hao wamesafiri ama laa, imegundua tiketi ya Dr. Moh'd Jape, Daktari dhamana wa Hospitali ya Mkoani na sio jina la mfanykazi yoyote kati ya wawili hao waliohusika na malipo **(Kiambatanisho Nam 39).**

Aidha, tiketi hiyo inaonesha imetumiwa Tarehe 04/10/2010, wakati maombi ya safari hiyo yaliombwa baina ya Tarehe 20/10/2010, na kuidhinishwa Tarehe 27/10/2010. Sambamba na hili, vielelezo vyote vya tiketi za safari kwa Ndg. Ali Moh'd Ali, vinaeleza kwamba ametoka Zanzibar kwenda Pemba, kinyume na ukweli halisi.

Pamoja na kuangalia Vocha za mwaka 2010, Kamati pia ilivutika kuangalia Vocha ya mwaka 2011, inayohusiana na malipo ya posho ya safari na nauli ya siku 2 kwa ajili ya kwenda Unguja kuhudhuria kikao cha Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Umeme. Malipo hayo alilipwa Meneja wa Tawi la Pemba, Ndg. Salim M. Saleh, kwa posho la Tsh. 300,000/- na Nauli Tsh. 180,000/- . Pamoja na Meneja huyu kulipwa fedha hizo, na pamoja na kwamba yeye ndie anaestahiki kusimamia matumizi bora ya fedha kwa upande wa Pemba, kwa bahati mbaya yeye

[4] Vocha hii nayo imekosewa kitarehe kwa kuandikwa 27/06/2010, wakati tarehe sahihi ni 27/10/2010.

mwenyewe ndie anaevunja taratibu hizo. Kwa mfano, iwapo utapitia vocha hii ya Tarehe 26/07/2011 **(Kiambatanisho Nam 40)**, unatarajia sana upate uthibitisho wa kupokelewa kwa fedha hizo, lakini pia unatarajia upate marejesho ya fedha hizo, hususan nauli ya safari. Kwa bahati mbaya sana, hakuna vielelezo hivyo katika vocha hii tunayoizungumzia.

Kwa kuzingatia maelezo haya, inajenga khofu na wasi wasi kwamba, matumizi ya 'Account' hii yamegeuka sawa na chaka la kufichia maovu ya baadhi ya watendaji wasiokuwa waaminifu. Kwani hata wewe unapata picha gani unapofahamu kwamba, akaunti hii hukusanya 2,000,000/- kwa siku, huku haina mkaguzi wa ndani wa kuikagua, wakati huo huo unafahamu pia kwamba, wakaguzi wake walifanyiwa vitendo vya makusudi kutoendelezwa kielimu ama kupata misuko suko kadhaa ya kikazi ambayo haina ulazima wowote, na kwa kuzingatia ukweli kwamba hata matumizi yake hayafuati ipasavyo taratibu za sheria zinazohusika, ni wazi na utakubaliana nasi kwamba, Akaunti hii imegeuka kuwa chaka la watendaji wasiokuwa waaminifu na hata wakubwa wa Shirika, kutumia fedha zake watakavyo wao.

1.11.0 Muhtasari wa Mambo yaliyobainika na Kamati kufuatia Uchunguzi wake wa Hadidu hii Rejea:

i. Baadhi ya Wafanyakazi wa Shirika, mfano ukitolewa kwa Ndg. Zakia Juma Azan, wanahusika na upotevu wa fedha na mali za Shirika.

ii. Shirika linapoteza fedha nyingi kutokana na udhaifu wa huduma zake pamoja na kuibiwa na baadhi ya wafanyakazi wake wasio waaminifu.

iii. Wateja wengi wa Shirika wanapata usumbufu mkubwa ikiwa ni pamoja na kuibiwa ama kulanguliwa fedha zao, pale wanapohitaji huduma ya umeme kwa Shirika.

iv. Uongozi wa Shirika unakiuka maagizo ya Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika, kwa kuruhusu Kampuni binafsi ya GECCO kufanya kazi na kutoa huduma ambazo tayari Bodi imeshakataza kufanywa na Kampuni hiyo.

v. Shirika limepoteza taarifa muhimu za wateja wake, na upotevu huo umesababishwa na uzembe pamoja na Uongozi kutojali umuhimu wa taarifa hizo.

vi. Viongozi wa Shirika badala ya kusimamia matumizi ya fedha za Serikali kama inavyotakiwa na Sheria za Fedha, wao hugeuka wa kwanza kukiuka masharti ya Sheria hizo.

vii. Kuna upendeleo na usumbufu dhidi ya wananchi wa kawaida na Makampuni ama watu uwezo katika kupata huduma za kuungiwa umeme kutoka Shirika la Umeme la Zanzibar.

HADIDU REJEA YA TATU:

TARATIBU ZA AJIRA KATIKA SHIRIKA ZINAZODAIWA KUWA ZA UPENDELEO, UNGUJA NA PEMBA:

3.0.0 Maelezo ya Hadidu Rejea:

Katika hadidu hii, Kamati ilitakiwa kuchunguza ukweli wa madai kwamba Shirika la Umeme, kwa upande wa Unguja na Pemba limefanya uajiri wa wafanyakazi wake kwa misingi ya upendeleo, yaani kuajiri kinyume na taratibu za kisheria

lakini pia kwa misingi isiyo ya haki na upendeleo ama wa udugu au ubaguzi wa aina nyengine yoyote.

Katika uchambuzi wa Hadidu hii rejea, Kamati imeona ni vyema ikaifafanua kwa kutumia mitindo miwili inayotofautiana. Wa kwanza ni kuchambua taarifa za Mfanyakazi mmoja mmoja kwa mujibu wa mwaka walioajiriwa, ambapo kazi hii imefanywa katika Uajiri wa mwaka 2008, kwa upande wa Pemba. Lakini kwa kuzingatia haja ya kufupisha ripoti hii (vyenginevyo, kurasa pekee za hadidu hii zisingelipungua 200 kwa sababu waajiriwa hao ni wengi), Kamati imeona ni vyema kwa kuanzia mwaka 2009 hadi 2012, kuzingatia mambo yaliyojitokeza kwa ujumla wake juu ya suala zima la Uajiri, kwani kwa kufanya hivyo, kunarahisisha wepesi wa msomaji kufahamu mambo hayo, kwa kuzingatia ukweli kwamba, takriban yanawiyana na yale yaliyofafanuliwa kwa mfanyakazi mmoja mmoja kwa mwaka 2008 katika Tawi la Shirika, Pemba.

Hivyo basi, katika kuifanyia kazi hoja hii, Kamati ilianza kukutana na Uongozi wote wa Shirika siku ya kwanza ya kazi, Tarehe 30/04/2012 katika Afisi za Shirika, kikao ambacho kilitoa fursa kwa kila mfanyakazi mwenye maoni juu ya utendaji wa Shirika, aeleze bila ya woga namna Shirika linavyotekeleza majukumu yake kwa mnasaba wa Hadidu rejea zilizokabidhiwa kwa Kamati, hali iliyopelekea Kamati kupata mwanzo mzuri wa uchunguzi wake, kufuatia wafanyakazi hao kutoa ushirikiao mzuri na wa aina yake. Baada ya kikao hicho, Kamati ilikutana na Uongozi wa Shirika, kwa ajili ya kupata ufafanuzi wa hoja hii, na ilihitaji Uajiri ulioanzia mwaka 2008 hadi 2012 na kwa hali hii, Kamati inaona ni vyema kutoa ufafanuzi wake kama ifuatavyo :

3.1.0 Uhalali wa Uajiri na Taratibu zinazofaa kufuatwa na Shirika la Umeme katika kufanya Uajiri :

Kwa kawaida, suala la Uajiri wa Wafanyakazi wa Serikali huratibiwa na Wizara inayohusiana na Utumishi wa Umma, na kwa hali hii, mtu yoyote ambae hajui mamlaka ya Shirika la Umeme na nafasi yake, angefikiria kwamba, uajiri wa wafanyakazi wa Shirika, ungestahiki ufanywe na Wizara hii kwa niaba ya Serikali, kwa maana Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Fikira hii, ingelihusika pia kwa zile Taasisi zinazojitemea, ambazo mbali na kupewa Mamlaka ya Uajiri, lakini taratibu za uajiri huo, huongozwa na Sheria Namba 2 ya

mwaka 2011 na Kanuni zinazohusika na Utumishi. Ama mtu huyu huyu kama hakupatiwa ufafanuzi mzuri, angeona ni vyema Uajiri wa Wafanyakazi hawa, utokane na Tume za Utumishi za Serikali, kama zilivyoanzishwa na kifungu cha 117 cha Katiba ya Zanzibar na kifungu cha 33 cha Sheria Namba 2 ya mwaka 2011.

Fikira zote hizi zinatofauatiana na uhalisia wa Shirika hili, kwa sababu, Sheria Namba 3 ya mwaka 2006 iliyoanzisha Shirika la Umeme la Zanzibar, imetoa mamlaka ya Uajiri na malipo ya stahili za wafanyakazi hao kupitia Bodi ya Wakurugenzi, iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha Sheria hiyo. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 10(b) cha Sheria hii, Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika, ina jukumu la kuthibitisha Muundo wa Shirika na taratibu za kazi na kufanya maamuzi juu ya masharti na maelekezo ya Utumishi, Mishahara pamoja na stahiki nyengine zinazohusika za Wafanyakazi wa Shirika la Umeme.

Vile vile, Shirika linatumia muongozo mkuu wa uajiri kupitia Kanuni za Utumishi za Shirika la Mafuta na Nguvu za Umeme, Zanzibar **(Kiambatanisho Nam 41)**, zilizoidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika, na kuanzia kutumika tarehe 01/07/2005. Kanuni hizi tayari zimeshafanyiwa marekebisho (First Draft) na Uongozi wa Shirika mnamo mwaka 2011, isipokuwa Kamati imefahamishwa kwamba, bado marekebisho hayo hayajapitishwa na Bodi ya Wakurugenzi, na kwa maana hii, Kamati pia haiwezi kuzitumia kwa sababu, bado hazijapata nguvu ya kisheria, ispokuwa ieleweke kwamba, kwa kuwa bado Kanuni za Utumishi za Shirika za mwaka 2005 zipo, itafahamika kwamba, hata katika ripoti yetu hii ndio tutakayoitumia kama ni muongozo sahihi unaoonesha taratibu zote za Uajiri katika Shirika.

Baada ya kufahamu hivyo, na baada ya siku ya kwanza ya kukutana na wafanyakazi wote wa Shirika tawi la Pemba, Kamati iliamua kuifuatilia hadidu hii, kwa kufanya mahojiano na Uongozi wa Shirika, pamoja na kuwafanyia uhakiki wafanyakazi waliohusika na hatimae kufahamu mambo kadhaa, ambayo tutayaeleza mwisho wa hoja hii. Ni vyema sasa tufahamu namna wafanyakazi hawa walivyoajiriwa, kwa kupata ufafanuzi ufuatao:

3.2.0 UTARATIBU WA AJIRA, SHIRIKA LA UMEME:

Kabla ya kupata maelezo ya wafanyakazi binafsi, ni vizuri tukafahamu utaratibu wa ajira katika Shirika la Umeme. Hali hii itatusaidia pia kufahamu kiini cha hoja hii na itakuwa ni rahisi kuelewa, iwapo kweli Shirika limekiuka taratibu hizo kwa uajiri ulioanzia mwaka 2008 hadi 2012, ama laa. Basi, na tuanze kwa kufahamu kwamba, maamuzi ya uajiri ni lazima yafanywe na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika, na hii ina maana kwamba, iwapo Uongozi wa Shirika chini ya Meneja Mkuu, utaona ipo haja ya kuajiri, ni lazima mapendekezo hayo yapelekwe kwenye Bodi ili iamue kukubali au kukataa ajira mpya. Na baada ya kutoa kibali, ni lazima nafasi hizo zitangazwe katika vyombo vya habari ili watu wenye sifa waweze kuomba. Aidha, baada ya matangazo kutoka, maombi yote ya nafasi za kazi katika Shirika, yanatakiwa yawasilishwe kwa Meneja Mkuu, ambapo baadae, waombaji wanaoonekana wana sifa, huitwa kwa ajili ya usaili na hatimae kupatikana wenye sifa nzuri zaidi zilizohitajika na waliofaulu usaili huo.

Baada ya hatua hii, waombaji waliofaulu kabla ya kuitwa kwa ajili ya kuajiriwa, taarifa zao hupelekwa G.S.O kwa ajili ya Uhakiki wa Kiusalama (Vetting) na baadae wale wataoonekana hawana matatizo ya kiusalama, huitwa na kutakiwa kufanyiwa Uchunguzi wa Kidaktari (Medical Checking) na ndipo wasiokuwa na matatizo ya kiafya, huajiriwa kwa kuingia Mikataba na Shirika ikiwa ni pamoja na kujaza Fomu za Ardhihali ya Kuingia Kazini. Hatua hii inapokamilika, Uajiri huwa umefuata taratibu zilizokubalika kisheria. Baada ya kufahamu hali hii, ni vyema sasa tuendelee na Uajiri wa wafanyakazi hao kwa Upande wa Pemba kwa mwaka 2008 na hatimae tumalizie kwa kuangalia Uajiri wa Unguja na Pemba kwa mwaka 2009 hadi 2012, kama ifuatavyo :

3.3.0 UAJIRI WA WAFANYAKAZI WA SHIRIKA-PEMBA (MWAKA 2008):

Kwa kawaida, Shirika la Umeme kwa upande wa Pemba, linaongozwa na Meneja wa Tawi, ambapo wakati Kamati inafuatilia suala hili, Ndg. Salim Masoud Saleh ndie Meneja mhusika na hata maombi mengi ya waajiriwa kwa upande wa Pemba, hufanywa kwake, kama tutakavyoona katika taaarifa za wafanyakazi hao. Hata

hivyo, suala hili linapingana na Kanuni za Utumishi za Shirika, kwa sababu, kwa mujibu wa kifungu cha 3(1) cha Kanuni hizo za mwaka 2005, Shirika huwa linaongozwa na Meneja Mkuu anaeteuliwa na Rais, na Meneja wa Tawi, Pemba ni sawa na Meneja wa Idara anaepaswa kuteuliwa kwa mujibu wa fasili ya (5) na Kanuni ya 3 ya Kanuni za Utumishi za Shirika.

Jambo jengine la msingi, ni vyema tukafahamu haja ya uajiri wa wafanyakazi wapya kutoka Pemba hadi Makao Makuu na iwapo, Bodi ya Wakurugenzi waliidhinisha uajiri wa mwaka 2008 kwa upande wa Pemba. Kwa lugha nyengine, Kamati imehoji iwapo kuna ushahidi wowote (Written Evidence) wa ajira hizo za 2008, kupata baraka ya mamlaka inayohusika. Katika hili, Shirika lilitakiwa liithibitishie Kamati, kwamba baada ya kuwepo kwa nafasi tupu Pemba, Meneja aliomba kibali kutoka Bodi ya Wakurugenzi, kwa sababu ndio yenye uwezo wa kutoa kibali hicho.

Hata hivyo, Kamati haikuweza kupatiwa barua ya kuomba kibali hicho kama ilivyohitaji na badala yake, imepatiwa barua ya Tarehe 2/12/2008 yenye kumbu kumbu namba ZECO/MFU/VOL.1/09 kutoka Makao Makuu, Unguja kwenda kwa Meneja Tawi, Pemba kumruhusu kuajiri wafanyakazi wapya 16 katika makisio ya 2007/2008, ambayo hapa tunainukuu:

> “Shirika linapenda kukuarifu kwamba, ruhusa ya kufanya Uajiri kwa nafasi tupu imetolewa kama ulivyoomba. Aidha, kati ya nafasi hizo, tayari umeshafanyika Uajiri kwa Madereva watatu (3)”

Tunapenda ifahamike kwamba, barua hii inaijibu barua yenye namba ZECO/CONF.5/3/VOL.III/244, iliyotoka kwa Meneja Tawi, Pemba kuomba kibali cha Uajiri kwa Meneja Mkuu, Unguja. Kwa maana hii, Kamati imejiridhisha kwamba, pamoja na kukosekana kwa barua ya kuomba kibali, kwa mujibu wa barua hii tuliyoinukuu hapo juu na kuifanya **Kiambatanisho Nam 42,** imejiridhisha kwamba, ruhusa iliombwa kutoka Pemba kwenda Makao Makuu, ili Idara hii ya Pemba iweze kuajiri wafanyakazi wapya. Hata hivyo, bado kuna suala la kujiuliza, je ombi hilo la kibali baada ya kufika kwa Meneja Mkuu, ni nani aliyetoa idhini ya kuruhusiwa Uajiri huo?

Kwa mujibu wa kifungu cha 10(b) cha Sheria ya Shirika la Umeme, Namba 3 ya mwaka 2006, Bodi ya Wakurugenzi ndio iliyopewa dhima ya kuthibitisha Muundo wa Shirika na Taratibu za Ajira pamoja na kufanya maamuzi ya masharti ya Uajiri, Mshahara na maposho mengine ikiwa ni pamoja na stahiki nyenginezo za Waajiriwa wa Shirika. Hii ina maana, ni pamoja na kuthibitisha ama kuidhinisha Uajiri mpya wa Shirika. Na kwa lugha hii, ni lazima Shirika liithibitishie Kamati kwamba, idhini ya Uajiri wa nafasi tupu kwa upande wa Pemba kwa mwaka 2008 (na kila miaka mengine inayohusika), imetolewa na Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika na sio Meneja Mkuu wa Shirika wala chombo chengine chochote cha Utawala cha Shirika hili. Hivyo basi, Kamati inapenda ieleweke dhahiri kwamba, haikupata uthibitisho wa idhini kutoka Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika kuruhusu Uajiri huo na hivyo, Kamati imejiridhisha kwamba, hatua hii kwa mwaka huu wa 2008 haikufuatwa, na si sawa na kuthibitisha kwamba, tokea awali taratibu za Uajiri wa Shirika kwa mwaka huu 2008, zimekiukwa kisheria.

Kasoro nyengine inayoonekana katika barua hii tunayoendelea kuijadili hapa, ni udhati wa ombi la kibali hicho cha Uajiri kutoka Pemba kwenda Makao Makuu Unguja, ambapo hapo awali tulikiri kwamba, Kamati imejiridhisha kwamba ombi hilo limefanywa. Hata hivyo, tunataka tufahamike pia kwamba, ombi hilo la kibali limefanywa nje ya wakati. Yaani, wafanyakazi hawa tutakaowazungumza kwamba wameajiriwa mwaka 2008, wameingia mikataba ya Uajiri baina ya mwezi wa Juni hadi Oktoba 2008, wakati barua hiyo tunayoizungumzia imeandikwa Tarehe 2/12/2008. Yaani, Idara hii ya Shirika la Umeme chini ya Meneja Tawi Pemba, imefanya Uajiri kabla ya kuomba kibali cha kuwaruhusu kufanya Uajiri, na ni wazi kwamba, Idara hii imejibebesha dhima isizo zake na kufanya Uajiri bila ya kuomba kibali cha kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria.

Mbali na kasoro hizo, Kamati pia imepatiwa barua ya Tarehe 12/03/2008 yenye kumbu kumbu namba ZECO/U.2/VOL.1/11 iliyotoka kwa Meneja wa Tawi, Pemba kwenda kwa Meneja Mkuu, inayohusu Majina yaliyopendekezwa kwa Uajiri kufuatilia Usaili uliofanyika Tarehe 20/2/2008, barua ambayo tunaifanya **Kiambatanisho Nam 43,** ambayo Kamati imepatiwa kama uthibitisho wa Orodha ya Wafanyakazi walioajiriwa mwaka 2008, na kupitia barua hii ndio Uongozi huu wa Shirika, ukajenga hoja kwamba, wamefuata taratibu za Usaili na taratibu nyengine zinazohusika na Uajiri. Hata hivyo, tunachotaka kifahamike katika barua

hii na kwa mnasaba wa barua ile tuliyoijadili hapo kabla, ya tarehe 2/12/2008 ni kwamba, barua hizi mbili zinapingana dhamira yake. Yaani, barua hii ya tarehe 12/03/2008 inaonesha kwamba Idara ya Shirika, Pemba imefanya usaili na hatimae kuwateua wafanyakazi hao na kitendo cha kuipeleka Makao Makuu ni kwa ajili ya kuomba upekuzi kama maelelezo ya barua hii, tunavyoyanukuu hapa chini, wakati ile barua ya tarehe 2/12/2008, inaomba ruhusa ya awali ya kuajiriwa wafanyakazi hao. Hebu na tujikumbushe nukuu hiyo ya barua ya tarehe 12/03/2008:

> "Kufuatia usaili uliofanyika tarehe 20/2/2008 ili kujaza nafasi zilizowazi kwa Tawi la Pemba, wafuatao wanapendekezwa **kufanyiwa upekuzi** ili kupatiwa ajira kwa vitengo vifuatavyo……."[5]

Aidha, barua hii ya tarehe 12/03/2008 imeonesha kwamba idadi ya wafanyakazi walioajiriwa ni 10 tu, wakati ile ya tarehe 2/12/2008 ilikuwa inahusu ruhusa ya kufanya uajiri wa wafanyakazi wapya 16 katika Makisio ya mwaka 2007/2008. Katika hali hii, mtu yoyote anafahamu wazi kwamba barua hizi zinapingana sana.

Hata hivyo, pamoja na kasoro zote hizi, Kamati imehoji juu ya utaratibu wa ajira kwa wafanyakazi walioajiriwa mwaka 2008 na kupewa orodha ya wafanyakazi hao tutakaowaelezea taarifa zao kwa utaratibu ufuatao:

3.3.1 Ndg. Othman Faki Omar:

Wakati akihojiwa na Kamati, Ndg. Othman Faki Omar aliulizwa iwapo alipeleka maombi ya kazi, na yeye alisema aliomba kazi Pemba kwa kumuandikia barua,Meneja wa Tawi-Pemba. Na baabae aliitwa katika usaili na hatimae kupewa taarifa kwamba amefaulu. Hata hivyo, wakati Kamati inafanya uhakiki wa taarifa zake binafsi, Barua hiyo ya maombi haikuwemo katika faili lake na ni sawa na kusema kwamba, Kamati haina uwezo wa kuthibitisha kwamba maombi ya kazi ya mfanyakazi huyu yamefanyika. Aidha, hata kama yamefanyika, kwa mujibu wa maelezo yake kwamba, barua hiyo kaiandika na kuituma kwa Meneja wa Tawi, Pemba, ni kwenda kinyume na maelekezo ya Kanuni ya 3(7) (a) ya Kanuni za Utumishi za Shirika, ambapo hapa tunainukuu:

[5] Msisitizo ni wetu.

> “Maombi yote ya nafasi za kazi katika Shirika, yatawasilishwa kwa Meneja Mkuu kwa utaratibu uliowekwa”

Na kwa hali yoyote, maombi hayo hayana sifa ya kukubalika kisheria kwa sababu hayakufuata taratibu za sheria zinazoelekeza, na ni sawa na kusema kwamba, kitendo cha Meneja wa Tawi Pemba kuyashughulikia maombi hayo, ni kubeba dhamana zisizo zake kisheria.

Mbali na hali hii, Mfanyakazi huyu ameajiriwa Fundi (Technician) akiwa amemaliza Elimu ya Ufundi katika Chuo cha Ufundi Karume (Karume Technical College) mwaka 2006, na Kamati haikuwa na pingamizi juu ya sifa zake za kielimu. Jambo jengine la msingi, linahusiana na Uhakiki wa Kiusalama wa Mfanyakazi huyu. Kwa mujibu wa taratibu zilizopo, kabla ya mfanyakazi wa Serikali kuajiriwa katika Taasisi kama hii, hufanyiwa Uhakiki wa Kiusalama (Security Vetting), lakini kwa bahati mbaya sana uhakiki huo haukufanyika kwa mfanyakazi huyu.

Sambamba na hili, Kamati imepokea barua ya tarehe 12/03/2008 yenye kumbu kumbu namba ZECO/U.2/VOL.1/11, ambayo tulikwishaieleza awali kuhusika kwake na Majina yaliyopendekezwa kwa Uajiri kufuatia Usaili uliofanyika tarehe 20/02/2008, isipokuwa tunataka tusisitize kwamba, jina la Ndg. Othman Faki Omar, halimo katika orodha hiyo iliyofanyiwa usaili na hatimae kupendekezwa kwa Uajiri, na kwa hali hii ni sawa na kusema kwamba, pamoja na Mfanyakazi huyu kuijibu Kamati kwamba amepeleka maombi yake kwa Meneja wa Tawi, Pemba na baadae kufanyiwa usaili. Kwamba katika hoja hii, Kamati ilitakiwa kuchunguza utaratibu mzima wa ajira uliofanywa na Shirika la Umeme, kwa kuzingatia kwamba kuna madai kwamba linaajiri bila ya kufuata taratibu za kisheria na huajiri kwa upendeleo. Hivyo ni vigumu kwa mazingira haya kuthibitisha kinyume cha madai ya msingi ya hoja hii. Na ni wazi kwamba, Mfanyakazi huyu ameajiriwa bila ya kufuata taratibu zilizopo.

3.3.2 Ndg. Maimuna Ali Mbarouk:

Kwa mujibu wa Mkataba wa ajira baina ya Shirka la Umeme na Ndg. Maimuna Ali Mbarouk, Mfanyakazi huyu ameajiriwa Tarehe 01/08/2008 katika nafasi ya Fundi (Technician). Hata hivyo, kipengele cha 2 cha Mkataba huo kinahitajika

kuangaliwa kwa ukaribu, ambacho kinasema, "Mwajiri anamuajiri muajiriwa na mwajiriwa anakubali kutumikia mwajiri kama Technician katika Kampuni ya Mwajiriwa iliopo Zanzibar, kuanzia Tarehe 1/08/2008". Yaani, neno Kampuni lililotumika katika kifungu hiki linaleta utata, kwa sababu Shirika la Umeme la Zanzibar, ambalo ndilo Muajiri wa Mwajiriwa huyu, sio Kampuni bali ni Shirika, kama ilivyoelezwa na kifungu cha 3(1) cha Sheria Namba 3 ya mwaka 2006 ambacho kinasomeka ifuatavyo:

> "Kunaanzishwa Shirika la Umma litakalojuilikana kuwa ni Shirika la Umeme la Zanzibar au (ZECO) kama ufupisho wake, lakini likileta maana kuwa Shirika"[6]

Kasoro hii isiporekebishwa na ikaendelea kujitokeza katika Mikataba kama hii, italeta utata mkubwa wa kisheria na zaidi pale suala hili litakapofikishwa katika vyombo vya Sheria. Hata hivyo, tukirejea kwa Mfanyakazi huyu, jina lake limejitokeza katika majina yaliyotoka Pemba kwenda kwa Meneja Mkuu, Unguja yaliyopendekezwa kuajiriwa baada ya kufanyiwa usaili tarehe 20/02/2008. Hata hivyo, kama walivyo wafanyakazi wengine, Mfanyakazi huyu hakufanyiwa Ukakiki wa Kiusalama (Security Vetting).

3.3.3 Ndg. Zuwena Abdalla Ali:

Akiwa amemaliza elimu ya Ufundi katika Chuo cha Ufundi Karume mwezi May 2008, miezi mitatu baadae, Ndg. Zuwena Abdalla Ali aliajiriwa katika nafasi ya Ufundi (Technician) tarehe 01/08/2008, ambapo jina lake limejitokeza katika orodha ya majina yaliyopendekezwa kwa uajiri kufuatia Usaili ulioelezwa kufanyika tarehe 20/02/2008, iliyotoka kwa Meneja wa Tawi, Pemba kwenda kwa Meneja Mkuu, Unguja. Aidha, Kamati ilipofanya mahojiano na Mfanyakazi huyu, alieleza kwamba amepeleka maombi yake ya kazi kwa Meneja wa Tawi, Pemba barua ambayo imeandikwa tarehe 14/12/2007, ingawaje imepokelewa tarehe 8/01/2008, takriban wiki 3 baada ya kupelekwa **(Kiambatanisho Nam 44)**. Barua hii inasomeka kama ifuatavyo:

> "Mimi ni Msichana mwenye umri wa miaka 23, nimemaliza masomo katika Chuo cha Ufundi Karume mwaka 2007 katika Idara ya Umeme. Naomba unipatie ajira (nafasi ya kazi) katika Ofisi yako. Natumai ombi langu litazingatiwa na kufanyiwa kazi"

[6] Tafsiri ni yetu

Jambo kubwa la nukuu hii, ni kuthibitisha tu kwamba, Mfanyakazi huyu alipokuwa anaomba nafasi ya kazi, hakutaja nafasi aliyoomba kuajiriwa na badala yake ameomba nafasi ya kazi, yaani nafasi yoyote ya kazi, ilimradi tu aajiriwe. Kwa maelezo haya, inakuwa vigumu kuthibitisha kwamba, Shirika lilitoa matangazo ya kutaka kuajiri, kwani ingekuwa hivyo, wangelitaja nafasi mbali mbali walizotaka kuzijaza, sifa na utaratibu wa kuomba na hata tarehe ya mwisho ya kupokelewa kwa maombi hayo. Kama hii haitoshi, kwa kuwa Kamati ilihitaji kuondosha shaka hii na wasi wasi huu iliyonayo, ilikuwa ni jukumu la Shirika kuthibitisha kwamba wametangaza nafasi hizo na sifa za waombaji pamoja na aina ya nafasi walizohitaji kujaza, kuwemo katika uthibitisho ama tangazo hilo. Kwa bahati mbaya sana, Shirika limeshindwa kuthibitisha hili na ni wazi kwamba, hakukuwa na taratibu sahihi za ajira zilizofuatwa, huku kanuni ya 7(a) na 11(1)(2) za Kanuni za Utumishi wa Shirika za mwaka 2005, zikishindwa kusimamiwa na kutekelezwa ipasavyo.

Aidha, wakati wa mahojiano na Kamati, Mfanyakazi huyu alieleza kwamba, pamoja na kuajiriwa kama Fundi (Technician) baadae alihamishiwa kufanya kazi ya Cashier (Mhudumu Fedha). Maelezo haya yanakubaliana na ushahidi wa barua ya Tarehe 28/02/2011 iliyotoka kwa Afisa Utawala, Ndg. Shaib Hassan Kaduara na kumtaka Mfanyakazi huyu kutumikia kitengo hicho cha Huduma ya Fedha, TUKUZA kama Cashier. Pamoja na uwezo wa Shirika kumhamishia Mfanyakazi wake katika kitengo ama eneo lolote la kazi, tunapenda ifahamike wazi kwamba, kwa mwaka wa 2011, ambapo Shirika hili pia liliajiri wafanyakazi wa Cashier, miongoni mwa sifa walizozihitaji pamoja na mambo mengine, Muombaji awe na Cheti cha ‘Accounting’ yaani amesomea na kuhitimu Mafunzo ya Hesabu ama Uhasibu.

Tofauti iliyopo kwa Mfanyakazi huyu ni kwamba, yeye amesomea Ufundi na sio ‘Accounting’ na ni wazi kusema kwamba amepangiwa nafasi ya Cashier ambayo hakuisomea, hali inayoonesha wazi kwamba, inachangia kwa kiasi kikubwa kuzorotesha uwezo wa Shirika. Kama hii haitoshi, baada ya mwaka mmoja tu wa uhamisho wake huo wa nafasi ya ‘Cashier’ TUKUZA, mnamo Tarehe 01/03/2012 Mfanyakazi huhu huyu kapokea barua ya Uhamisho, kutoka nafasi hiyo ya Cashier na kupangiwa Kitengo cha ‘Marketing’ katika Idara ya Biashara, nafasi ambayo anaendelea nayo mpaka Kamati inafika katika Shirika hili, ingawaje nafasi hii

inahitaji elimu na uwezo mkubwa wa namna ya kulisaidia Shirika kuendelea kibiashara, huku Mfanyakazi huyu akiwa hajasomea masuala ya Biashara.

Kwa namna hii, utafahamu tu kwamba, Shirika halina utaratibu mzuri wa Uhamisho wa Wafanyakazi wake. Hali iliyopelekea pia kuwepo kwa malalamiko makubwa kutoka kwa wafanyakazi hayo, kama madai haya yalivyopokelewa na Kamati siku ya mwanzo ya kazi ya Kamati ilipokutana na Wafanyakazi wote na Viongozi wao, Pemba Tarehe 30/04/2012.

3.3.4 Ndg. Aisha Omar Khamis:

Mfanyakazi huyu ameajiriwa Mshika Fedha (Cashier) kuanzia Tarehe 01/06/2008. Mfanyakazi huyu amemaliza Kidato cha Sita, Skuli ya Sekondari ya Fidel Castro, mwaka 2006, huku akiwa hana kumbu kumbu zozote za kupasi somo la Hisabati, somo ambalo lingelimuwezesha vyema kutekeleza majukumu yake mapya ya nafasi ya ‘Cashier’ aliyoajiriwa kwayo. Aidha, Kamati haikupata ushahidi wa kutosha kwamba Mfanyakazi huyu amefanya Usaili na hatimae kuajiriwa kwa utaratibu uliowekwa kisheria.

Kwa kuwa hakuna ushahidi wowote uliwasilishwa kwa Kamati na Shirika la Umeme, unaoonesha Tangazo la Nafasi wanazotaka kuajiri, Orodha ya walioteuliwa kufanya Usaili (Short list), Idadi ya walioitwa kufanya Usaili wala Orodha ya waliopasi usaili huo na badala yake imepatiwa ushahidi wa Majina yaliyopendekezwa kwa Uajiri kufuatia Usaili unaodaiwa kufanywa Tarehe 20/02/2008. Kwa mujibu wa orodha hii yenye Idadi ya watu 10, ambao Kamati ndio ilioelezwa kuajiriwa kwa mwaka huu wa 2008, huku Mfanyakazi Mmoja, Ndg. Mussa Makame Haji, aliajiriwa bila ya kufuata taratibu walizopita wenzake. Tunaendelea kusisitiza kwamba, pamoja na Kamati kukabidhiwa barua hiyo ya Idadi ya Majina yaliyopendekezwa kwa Uajiri wa mwaka 2008, Mfanyakazi huyu hayumo katika orodha hiyo na ni wazi kwamba, hakufanyiwa usaili wala hakuna uthibitisho kwamba ameajiriwa kwa kufuata taratibu za Sheria kama zinavyoelekezwa na Sheria Namba 3 ya mwaka 2006 wala Kanuni za Utumishi za Shirika za mwaka 2005.

Mbali na hili, kuna tofauti kubwa baina ya tarehe ya kuajiriwa ya Mfanyakazi huyu ambayo ni 01/06/2008 na ile aliyoijaza katika Ardhihali yake 18/01/2008, tarehe

hii pia ndio aliyoijaza katika Fomu ya Upimaji wa Daktari (Medical Examination). Kwa kawaida vitu hivi huenda sambamba na mpishano wake huwa sio wa muda mrefu kama ulivyo katika taarifa za Mfanyakazi huyu. Aidha, kama utarejea barua ya Tarehe 12/03/2008 inayohusu Majina yaliyopendekezwa kwa Uajiri kufuatia Usaili unaodaiwa kufanyika Tarehe 20/02/2008, utafahamu kwa uwazi kwamba, Mfanyakazi huyu amesaini Ardhilhali ya Kuingia kazini pamoja na kufanya Uchunguzi wa Daktari, kabla hata ya muda unaosadikiwa kufanyika kwa Usaili husika. Hali hii inaleta shaka, na ndio maana Kamati inajiridhisha kwamba, Kuajiriwa kwa Mfanyakazi huyu, hakukufuata taratibu zilizowekwa kisheria **(Kiambatanisho Nam 45).** Vile vile jambo jengine linaloleta utata ni kwamba, Mfanyakazi huyu amejaza Makataba wa kazi Tarehe 01/06/2008, wakati ardhilhaji ya kuingia kazini inasema Mfanyakazi huyu ameingizwa kazini Tarehe 18/01/2008.

Yaani hapa kuna vitu vitatu vinachanganya. Moja ni kuingizwa kazini kwa mara ya kwanza ni mwezi Januari 2008, usaili unasadikiwa kufanyika mwezi Febuari 2008, Mkataba wa kazi unaonesha ameajiriwa Juni 2008, hapa kwa namna yoyote Kamati imejiridhisha kwamba pana ubabaishaji mkubwa katika ajira hii.

3.3.5 Ndg. Salum Mussa Alawy.

Mfanyakazi huyu ameajiriwa kama ‘Operator’ mnamo Tarehe 01/10/2008 baada ya maombi yake ya Tarehe 31/1/2008 aliyoyatuma kinyume na muongozo wa Kanuni za Utumishi za Shirika, kwa kumuandikia Meneja wa Tawi Shirika la Umeme Pemba, ambapo Kanuni ya 3(7)(a) ya Kanuni za Utumishi za Shirika, inaelekeza maombi hayo kuwasilishwa kwa Meneja Mkuu wa Shirika. **(Kiambatanisho Nam 46)**. Aidha, Mkataba wa Ajira wa Mfanyakazi huyu hauna athari yoyote kisheria kwa sababu umekosa ridhaa ya upande wa Muajiri, yaani saini ya Shirika.

Wakati akitoa ufafanuzi wa maombi yake ya kazi, Mfanyakazi huyu alikiri kwamba, wakati anaajiriwa, hakuambatanisha na cheti chake cha kuzaliwa kwa sababu kilipotea. Na kwa maana hii, maombi yake yamezingatiwa na kupokelewa bila ya kujuulikana uhakika wa umri wake. Pamoja na hali hii, katika Orodha ya Majina yaliyopendekezwa kuajiriwa baada ya usaili unaosemekana umefanyika Tarehe 20/02/2008, Mfanyakazi huyu yumo katika orodha hiyo.

Kwa mujibu wa kanuni ya 11(2) ya Kanuni za Utumishi za Shirika, kila muombaji wa kazi katika Shirika, analazimika kupimwa na daktari maalum atakaeamuliwa na Shirika na hawezi kuajiriwa mpaka upatikane uthibitisho wa maandishi kutoka kwa daktari huyo kuhusu kujiridhisha kwa hali ya afya ya mfanyakazi husika. Kwa kawaida, katika kupitia taarifa za kila mfanyakazi, Kamati hujiridhisha kwa kuziona fomu hizo za daktari zikiwa zimejazwa taarifa za Mfanyakazi husika, lakini kwa bahati mbaya, Mfanyakazi huyu hana taarifa hizo katika faili yake, na ni sawa na kusema kwamba, Kamati imekosa uthibitisho wa kufuatwa kwa maelekezo ya kanuni hii ambayo ni msingi wa kuonesha taratibu za kuajiriwa kwa mfanyakazi husika.

Hata hivyo, wakati akihojiwa, Mfanyakazi huyu alieleza kwamba amefanya uchunguzi wa daktari na kauli hii pia ilielezwa na Uongozi wa Shirika kwa madai kwamba, taarifa zake hizo zipo Unguja, Makao Makuu ya Shirika. Ingawaje, hata Kamati ilipofika Unguja haikuweza kupatiwa uthibitisho huo na ikajiridhisha kwamba, hakuna uthibitisho wa Mfanyakazi huyu kupimwa afya yake kabla ya kuajiriwa. Kama vile ulivyokosekana ushahidi wa Mfanyakazi huyu kufanyiwa uchunguzi wa kiusalama (Vetting) kabla ya kuajiriwa kwake.

3.3.6 Ndg. Haji Hamad Shaame:

Mfanyakazi huyu ameajiriwa kama Fundi (Technicia Plant), huku tarehe sahihi ya kuajiriwa kwake ikiwa na utata katika Mkataba wake wa kuajiriwa. Katika kifungu cha kwanza na cha Pili cha Mkataba huo, Ndg. Haji Hamad Shaame ameajiriwa Tarehe 01/10/2008, lakini katika sehemu ya saini ya Mkataba husika, Mwajiri akiwa ni Shirika ametia saini Tarehe 2/08/2008, huku Mwajiriwa akitia saini Tarehe 01/08/2008. Mfanyakazi huyu aliepata elimu yake ya Ufundi Chuo cha Ufundi Karume mwaka 2007, aliomba kazi hiyo kupitia barua yake ya Tarehe 09/08/2007 **(Kiambatanisho Nam 47)**, akimuandikia Meneja wa Tawi, Pemba na kuomba ajira asiyoifahamu, huku akitegemea zaidi elimu yake ya Ufundi mashine (Automative Engineering).

Hata hivyo, hakuna uthibitisho kwamba amefanyiwa Uchunguzi wa Kidaktari, kwa maelezo yale yale kwamba taarifa zao hazimo katika mafaili yao binafsi na badala yake yapo Unguja ambapo Kamati pia haikupatiwa uthibitisho wake. Sambamba na hili, hakuna uthibitisho kwamba, amefanyiwa Uchunguzi wa Kiusalama

(Security Vetting) kabla ya kuajiriwa kwake. Kwa ujumla, Kamati imejiridhisha kwamba, uajiri wa mfanyakazi huyu, haukufuata taratibu za kisheria kama zilivyowekwa. Hata hivyo, katika majina yaliyopelekwa Unguja kwa barua ya Tarehe 12/03/2008, Jina la Mfanyakazi huyu limo katika orodha hiyo.

3.3.7 Ndg. Said Juma Salum.

Mfanyakazi huyu ameajiriwa kama 'Operator' katika kituo cha Wesha kuanzia Tarehe 01/08/2008. Wakati akihojiwa namna gani alipeleka maombi yake ya kazi, alieleza kwamba, baada ya kuandika barua hiyo kwa mkono wake, aliipeleka kwa Meneja wa Tawi, Pemba. Na hatimae aliitwa kwa ajili ya Usaili na kuarifiwa kupata nafasi hiyo baada ya kupasi katika usaili husika. Hata hivyo, kama Kamati ilivyokosa uthibitisho wa zoezi zima la usaili wa wafanyakazi hawa, ndio pia kukosekana huko kunahusiana na Mfanyakazi huyu, ingawaje katika ile orodha ya majina yaliyopendekezwa kwa Uajiri baada ya kusadikiwa kufanyika usaili wa Tarehe 12/03/2008, Jina la Mfanyakazi huyu limo katika orodha hiyo.

Katika maelezo yake, Ndg. Said alieleza kwamba baada ya kupata taarifa za kufaulu kwake, alikwenda kufanya Uchunguzi wa Daktari na kujafa fomu zilizohusika. Hata hivyo, Kamati ilipokuwa inapitia taarifa binafsi za Mfanyakazi huyu katika faili lake, hakukuwa na fomu yoyote ya daktari kama vile ilivyokosekana barua yake ya maombi ya kazi, ingawa yeye alieleza kwamba, alipeleka barua hiyo kwa Meneja wa Tawi, Pemba. Mfanyakazi huyu amesomea Ufundi, Chuo cha Veta, Dar es Salaam na kumaliza Tarehe 15/03/2004 **(Kiambatanisho Nam 48)**, huku saini yake aliyoitia katika cheti hicho, ikitofautiana na saini alizotia katika Mkataba wake wa ajira na hata Kitambulisho chake cha Mzanzibari. Aidha, kwa muono wa Kamati, ni dhahiri kwamba, hati za Mfanyakazi huyu ni za udanganyifu.

Mbali na udhaifu huo, Mfanyakazi huyu aliwasilisha vyeti viwili vya J.K.U, kimoja ni cha Ufundi kinachosomeka kwamba amepata mafunzo ya miaka miwili kuanzia Januari 2002 na kumalizia Disemba 2003, huku cheti cha pili ni cha Ujenzi wa Taifa, alichokipata kuanzia Tarehe 6/1/2003 hadi Tarehe 16/2/2004 alichokitumikia katika Kikosi cha Mtoni. Aidha, udhaifu wa vyeti hivi viwili ni jambo lisilohitaji utaalamu mkubwa. Kwa mfano, inafahamika wazi kwamba, ndani ya mwaka mmoja, mwaka 2003, Mfanyakazi huyu kutumikia Mafunzo ya

Ufundi yaliyotolewa kwa miaka miwili na huku akitumikia Ujenzi wa Taifa kuanzia Tarehe 6/1/2003[7] hadi Tarehe 10/02/2004, kitu ambacho ni muhali, kwani ni mwaka huo huo akitumikia mafunzo ya Ufundi huku pia akitumikia Mafunzo ya Ujenzi wa Taifa. Aidha, wakati akihojiwa mbele ya Kamati, alieleza kwamba, mafunzo ya Ufundi aliyapata miaka miwili kwanza, yaani akisomea ufundi pekee bila ya kuchanganya na mafunzo mengine, na mwaka wa tatu ndio alitumikia Ujenzi wa Taifa.

Mbali na hali hiyo, Mfanyakazi huyu ameambatanisha na cheti chake cha Mafunzo ya VETA, aliyosomea Ufundi wa Magari, 'Grade Three' na kufanikiwa kupata cheti kilichotolewa Tarehe 15/03/2004. Hata hivyo, Cheti hichi nacho kina kasoro nyingi zilizotiliwa wasi wasi na Kamati. Kwa mfano, saini ya Mfanyakazi huyu kama mwenye cheti hicho, inatofautiana na saini aliyoitia katika Mkataba wake wa Uajiri wa Kudumu, kama vile inavyotofautiana katika Kitambulisho chake cha Mzanzibari. Aidha, mafunzo haya ya Ufundi wa Magari kupitia nadharia (theory) na Vitendo (Practical) katika chuo hicho cha VETA, Dar es Salaam, ameyapata ndani ya mwezi mmoja tu, yaani tokea alipomaliza kutumikia Ujenzi wa Taifa, J.K.U, Kikosi cha Mtoni Zanzibar, Tarehe 10/02/2004 huku cheti hicho cha VETA kinaonesha kwamba amekipata mwezi mmoja tu baadae, Tarehe 15/03/2004, kitu ambacho ni muhali kuwezekana.

3.3.8 Ndg. Khamis Abdalla Mselem.

Mfanyakazi huyu ameajiriwa Tarehe 1/10/2008 nafasi ya Fundi Umeme (Technician) kupitia Mkataba wake na Shirika, ambao tunaufanya ni **Kiambatanisho Nam 49**, ambapo katika Mkataba huo, tatizo lile lile la Shirika hili kujitambulisha kama Kampuni, limejirejea. Hii inathibitisha wazi kwamba, Shirika hili halikuwa makini katika Mikataba ya ajira iliyoingia na watumishi wake. Vile vile, katika barua ya kazi ya Mfanyakazi huyu aliyoiandika tarehe

[7] Ifahamike kwamba, mwezi ulioainishwa hapo juu hauonekani kwa uwazi wake, isipokuwa kwa kuwa hakuna utata kwamba mafunzo hayo ni ya mwaka mmoja, na kwa kuwa tarehe ya kumalizia mafunzo hayo inaonekana kwa uwazi, yaani tarehe 10/2/2004, ni wazi kwamba mafunzo hayo yameanza mwezi wa Januari, 2003.

17/1/2008, aliiandika kwa Meneja wa Tawi Pemba na sio kumuandikia Meneja Mkuu wa Shirika hili kama Sheria za Shirika zinavyoelekeza.

Kama tulivyoeleza kwamba, suala la kuthibitisha iwapo sifa za mfanyakazi huyu ndizo zilizohitajika kwa nafasi anayoajiriwa nayo, bado hakuna uthibitisho uliotolewa kwa Kamati kwa mwaka 2008 na hivyo, ni vigumu kuzithibitisha. Hata hivyo, katika nafasi hii kwa mwaka 2011 (ambapo ndipo Kamati imepatiwa sifa zilizotolewa katika nafasi ya maombi ya kazi), na kwa mnasaba wa nafasi aliyoajiriwa kwayo, bado inabaki ni kitu kisichoweza kulinganishwa. Hata hivyo, ni wazi kwamba, wakati wa mahojiano, Mfanyakazi huyu alikiri kwamba amemaliza Kidato cha Nne na hatimae amesomea Masomo ya Ufundi wa Umeme.

Pamoja na maelezo haya, Mfanyakazi huyu ameshindwa kuwasilisha mbele ya Kamati, cheti halisi ya Kidato cha Nne, sio halisi (original) wala Kopi yake (Certified Copy). Na hatimae, amekiri kwamba ameajiriwa akiwa na sifa ya kumaliza Kidato cha Pili (Form II) nae ameridhika kuajiriwa kwa kiwango hicho. Sababu kubwa ya hoja yake, aliieleza Kamati kwamba cheti chake hicho kimeharibika, jambo ambalo ni wazi hata kwa mtu wa kawaida halimuingii akilini. Kwa upande wa Kamati, haikubaliani na maelezo haya na inajiridhisha kwamba Mfanyakazi huyu ameajiriwa akiwa hana sifa.

Mbali na hayo, wakati Kamati inaendelea na uchunguzi wake, Mfanyakazi huyu aliieleza Kamati kwamba, hayo Mafunzo ya Ufundi Umeme, ya miaka miwili (kuanzia Januari 1998 hadi Decemba 1999)[8] alihitimu katika Chuo cha Ufundi 'Gulioni Technical School'. Na katika kuthibitisha kwake, alieleza kwamba somo la Ufundi 'Electrician' alipata kiwango cha 'A', yaani kiwango cha juu zaidi katika viwango vya elimu nchini Tanzania. Tatizo ni kwamba, katika orodha ya masomo yaliyomo katika cheti hicho, ambacho hapa ni Marejeo ya **Kiambatanisho Nam 50,** Somo la 'Electrician' halimo katika orodha ya masomo, na ni masomo yafuatayo tu na viwango vyake ndivyo vinavyothibitishwa; yaani somo la Physics amepata 'C'; Mathematics amepata 'C'; Tecnhical Drawing amepata 'B'; Theory amepata 'C' na somo la 'Practical' amepata 'B'. Tunachotaka tuthibishe hapa ni kwamba, Mfanyakazi huyu hana uhakika wa anachokithibisha mbele ya Kamati,

[8] Ingawaje ukifanya marejeo ya barua yake ya kazi, tuliyoiambatanisha na Kiambatanisho husika, Mfanyakazi huyu alikiri kwamba amemaliza masomo yake mwaka 2000, na sio 1999 kama ilivyo katika vyeti vyake.

na ni wazi kwamba sifa zake hizi zinatia mashaka na Kamati inaendelea kujiridhisha kwamba, hakuwa na sifa za kuajiriwa katika nafasi hii.

3.4.0 UAJIRI WA WAFANYAKAZI WA SHIRIKA UNGUJA NA PEMBA (MWAKA 2009):

Kwa mwaka wa 2009, Shirika liliajiri Wafanyakazi zaidi ya 30 kwa Unguja na Pemba. Kwa kuzingatia haja ya kufupisha ripoti hii, Kamati inaona ni vyema kutaja maeneo ambayo yameonekana ni sehemu ya mapungufu katika Uajiri huo, kwa mnasaba wa Hadidu hii kama ifuatavyo:

3.4.1 Kuendelea kukiukwa kwa masharti ya Uwasilishaji wa Maombi ya Ajira, Upande wa Pemba:

Kama tulivyokwishaeleza awali, kwamba Kanuni ya 3(7)(a) ya Kanuni za Utumishi za Shirika za mwaka 2005, Maombi ya nafasi za kazi katika Shirika, yanatakiwa yawasilishwe kwa Meneja Mkuu wa Shirika, kwa kuzingatia utaratibu ulioelezwa. Kwa bahati mbaya sana kwa upande wa Pemba, Kamati imejiridhisha kwamba, maombi yote ya mwaka huu kama ilivyotokea kwa miaka iliyofuata, yalielekezwa kwa Meneja wa Tawi, Pemba, ambae hana dhamana wala mamlaka haya kisheria. Ni sawa tu kisheria kusema kwamba, maombi haya hayakutumwa kisheria, na ni sawa pia kumalizia kwa kusema kwamba, hakukuwa na maombi ya kuomba kazi yaliyoeleza nia na haja ya muombaji, ambae ndie muajiriwa wa Shirika.

Aidha, Kamati ilipofanya mahojiano na waajiriwa wa Shirika Tawi la Pemba, kwa mwaka huu, walieleza kwamba, walisikia redioni tangazo la ajira katika Shirika. Jambo hili halilazimishwi kubishaniwa sana, lakini yapasa ieleweke kwamba, hakuna kielelezo chochote kilichothibitisha ukweli wa tangazo ama matangazo ya ajira kwa mwaka huu. Na kwa kuwa Kamati imezingatia ushahidi wa kimaandishi zaidi kuliko wa maneno matupu, imejiridhisha kwamba hakukua na utaratibu wa kutangazwa nafasi za kazi kupitia vyombo vya habari, na kutaja sifa za waajiriwa wanaohitajika katika mwaka huo. Utaratibu huo kwa upande wa Pemba ulikuwa ni mgeni na ulianza mwaka 2011.

3.4.2 Mikataba ya Ajira kutofuata masharti yote ya kisheria:

Jambo jengine ambalo pia ni maarufu kwa mikataba ya ajira iliyoingiwa baina ya Shirika na Wafanyakazi wake. Suala hili kwa namna yoyote ile inaifanya Mikataba hiyo kuwa na utata mkubwa kisheria. Labda Kamati iendelee kusisitiza hoja hii kwa kuangalia pia Mikataba ya wafanyakazi walioajiriwa kwa muda huu, na kwa suala hili, Kamati inapenda ufanyiwe rejea Mkataba wa Ndg. Salma Juma Said, Mhasibu wa Shirika Tawi la Pemba, aliejiriwa Tarehe 01/11/2009. Iwapo utaangalia sehemu ya kusainiwa Mkataba huu, ambao ni **Kiambatanisho Nam 51** cha ripoti hii, Utakubaliana nasi kwamba,hauna saini ya Meneja Mkuu wa Shirika na wala saini ya mtu yoyote isipokuwa ni umesainiwa na Mfanyakazi mwenyewe pekee.

Unaweza kujiuliza mara mbili mbili kwa Taasisi kama hii kubwa ya Serikali kufanya vitu adimu kufanywa katika Serikali, lakini uhalisia ndio huo ambao unaleta tafsiri tofauti inapogundulika suala hili. Ama ni uzembe wa Shirika, kutofahamu majukumu na uzito wa Mikataba ya ajira kisheria, kufanywa kwa makusudi kwa lengo la kutafuta njia ya kuwasumbua wafanyakazi wake na inapotokezea tatizo la kisheria, Mfanyakazi huyo akose haki zake ama maana nyengine yoyote ambayo hata kama sio sahihi, lakini kwa kitendo hiki itasadikiwa kuwa na maana.

Jambo la kushangaza zaidi baadhi ya Mikataba hiyo imekosa hata saini ya Mfanyakazi husika. Hili linashangaza sana kwa Taasisi kubwa yenye umuhimu wa kipekee Zanzibar. Kwa mfano Ndg. Ameir Omar Rajab, Mwajiriwa wa Shirika upande wa Unguja, aliaejiriwa Tarehe 03/03/2009, hajatia saini Mkataba wake wa ajira uliosainiwa kwa upande wa Mwajiri wake Tarehe 09/03/2009. Kwa maana hii, Mkataba huu hauko halali kisheira. Na ikitokezea tatizo lolote la kisheria, Mfanyakazi huyu anaweza kukosa haki zake kwa urahisi zaidi.

Aidha, kama ilivyo mikataba mingi iliyoingiwa na Shirika na waajiri wake, Mkataba huu pia umekosa saini ya Afisa wa kazi, alietarajiwa kutoka Wizara inayohusika na kazi Zanzibar. Jambo linaloshangaza ni kwamba, kwa kila Mkataba wa kudumu wa Shirika na Waajiriwa wake, huwa kuna sehemu ya kusaniwa na kuthibitishwa na Afisa huyo wa kazi. Kwa Mkataba huu, pamoja na Mikataba yote inayohusika na Uajiri wa Kudumu kwa mwaka 2009, hakuna saini ya Afisa huyo,

na ni sawa na kusema kwa maslahi ya Mkataba huu kwamba, Mkataba huu haujathibitishwa. Ni suala linaloendelea kuleta utata juu ya uhalali wa Mkataba huu kisheria.

Aidha, kwa upande wa Unguja nako kumethibitika tatizo kama hili, ambapo kwa ujumla Kamati imejiridhisha kwamba, Shirika halifuati ipasavyo masharti ya sheria katika suala zima la Mikatba yake inayoingia na Wafanyakazi wake. Mfano Ndg. Ameir Omar Rajab, Msomaji Mita alieajiriwa Tarehe 03/03/2009, Mkataba wake hauna saini ya Afisa wa kazi **(Kiambatanisho Nam 52)**, huku Kamati ikisisitiza kwamba, kama Shirika lilikuwa halioni umuhimu wa kuweka uthibitisho wa Afisa wa kazi, basi kulikuwa hakuna haja ya kuweka uthibitisho wake katika Mikataba ya Kudumu ya waajiriwa, wakati hakuna saini wala uthibitisho wowote unaofanywa juu ya Mikataba hiyo.

3.4.3 Uthibitishwaji wa Kazini kutofuata Masharti ya Kanuni za Utumishi za Shirika:

Kanuni ya 12 ya Kanuni za Utumishi za Shirika za mwakwa 2005, inazungumzia Muda wa Majaribio (Probation Period), ambao unafafanuliwa kwa masharti tofauti baina ya Mkataba wa Kudumu na Mkataba wa Muda. Kwa upande wa Mkataba wa Kudumu, masharti yake ni muda wa mwaka mmoja, kama inavyonukuliwa hapa chini na kifungu cha 12(1) cha Kanuni hizo:

> "Mtu anayeajiriwa kwa nafasi ya kudumu atalazimika kuwemo katika majaribio kwa muda wa miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya kuajiriwa"

Kwa maana hii, Mfanyakazi huyu Ndg. Salma Juma Said, alieajiriwa Tarehe 01/11/2009 kama inavyothibitika katika Mkataba wake wa ajira ya Kudumu, alitakiwa athibitishwe baada ya kumalizika mwaka mmoja wa majaribio ambao ni sawa na Tarehe 01/11/2010. Jambo la kushangaza Mfanyakazi huyu amethibitishwa miaka miwili na takriban miezi minne baada ya kuajiriwa. Yaani amethibitishwa kazini mnamo Tarehe 14/03/2012, kama inavyothibitika katika **Kiambatanisho Nam 53** cha taarifa hii. Kufanya hivi ni wazi kwamba kunakiuka masharti ya Kanuni ya 12(1) ya Kanuni za Utumishi tuliyoieleza na kuinukuu hapo juu.

Kichekesho ni kwamba, Mfanyakazi mmoja anathibitishwa mara mbili katika nafasi hiyo hiyo moja aliyoajiriwa. Kadhia hii inahusiana na Ndg. Mwadini Buzi Mwadini, alieajiriwa tarehe 01/07/2009 kama Dereva na akathibitishwa kazi mnamo tarehe 17/06/2010 kupitia barua namba ZECO/PF/M.206 na haijatosha, akathibitishwa tena tarehe 14/03/2012, siku ambayo takriban wafanyakazi wengi walipewa barua zao za kuthibitishwa **(Kiambatanisho Na 54)**. Suala hili linaifanya Kamati kuamini kwamba, pamoja na tafsiri nyengine, Shirika limejitutumua kuwapa barua wafanyakazi wake mnamo tarehe 14/03/2012 baada ya tetesi ya Mhe. Hija Hassan Hija, kuleta hoja binafsi dhidi ya Utendaji wa Shirika, ili angalau kuficha mapungufu mengi zaidi.

Aidha, unaweza ukadhani kwamba, kitendo hicho cha Mfanyakazi mmoja kuthibitishwa mara mbili, ama Mikataba yao kukosa saini za Mwajiriwa, kimetokea kimakosa. Dhana hii hubatilishwa kwa kule kufahamu kwamba, kasoro hizi zimejitokeza zaidi ya mara moja kwa wafanyakazi tofauti. Basi na Ndg. Abdul Moh'd Seif, aliajiriwa Tarehe 01/07/2009 kama Dereva, alithibitishwa mara ya kwanza kama wenzake walioajiriwa mwaka huu Unguja, mnamo Tarehe 30/06/2010 na akathibitishwa tena mnamo Tarehe 14/03/2012 kama inavyothibitika katika **Kiambatanisho Nam 55** cha ripoti hii. Aidha, Mfanyakazi huyu hata saini ya Mkataba wake wa ajira kuonesha ridhaa yake ya kazi, ameshindwa kuitia katika Mkataba huo.

3.5.0 UAJIRI WA WAFANYAKAZI UNGUJA NA PEMBA, KWA MWAKA 2010:

Kamati pia ilifanya ukaguzi kwa waajiriwa wa Kudumu wa Shirika, kwa mwaka 2010, kwa upande wa Unguja na Pemba. Katika kufanikisha suala hili, ilikutana na Uongozi wa Shirika na kuwaita wafanyakazi waliohusika na Uajiri huo. Aidha, Kamati inaona vyema kupata taarifa zao kama ifuatavyo:

3.5.1 Kutotangazwa kwa nafasi za Ajira kwa Wafanyakazi

Kama tulivyokwisha eleza awali, kwamba, pamoja na Uongozi wa Shirika kuona ipo haja ya kuajiri wafanyakazi wapya wa Kudumu, haja hiyo haipati uhalali wa kisheria, mpaka pale Bodi ya Shirika hilo itakapoidhinisha Uajiri huo. Na utaratibu wa kuombwa kwa idhini hiyo hutangulia kabla ya uajiri wenyewe. Kamati kwa

upande wake, ilitaka kujiridhisha iwapo kibali hicho kiliwahi kuombwa na matokeo yake Uajiri ukafuata taratibu zilizosalia. Jambo la kusikitisha ni kukosekana kwa uthibitisho wa kuombwa kwa kibali hicho kwa mwaka 2010, kwa Upande wa Unguja na Pemba. Na kufanya hivyo, ni sawa na kukiuka masharti ya kifungu cha 10(b) cha Sheria ya Shirika la Umeme, Namba 3 ya mwaka 2006.

Kamati haikupata tabu sana juu ya kujadiliana kuhusu suala hili, kwa kuwa tayari ilikwisha elezwa kwamba, kwa miaka yote hiyo, ukitoa mwaka 2011, Shirika na zaidi kwa upande wa Tawi la Pemba, halikufuata kikamilifu taratibu za ajira kama zilivyotakiwa, msisitizo ukiwekwa kwa upande wa idhini ya Bodi ama kutangazwa kwa uwazi wa nafasi pamoja na sifa zilizohitajika. Na kwa hali hii, Kamati ilipata tabu kujua sifa gani zilihitajika kwa wafanyakazi hawa, kwa kuwa hakukuwa na tangazo lililoainisha sifa hizo, wala uthibitisho kutoka katika Uongozi wa Shirika. Hata hivyo, pamoja na hali hii, Kamati iliendelea kugundua masuala yafuatayo:

3.5.2 Mikataba ya Ajira kukosa saini halisi ya Muajiri:

Wakati Kamati inapitia mikataba ya ajira kwa wafanyakazi walioajiriwa Pemba, mwaka 2010, ilijiridhisha kwamba, imekosa saini ya Muajiri,ambae ni Meneja Mkuu wa Shirika. Mikataba hiyo, badala yake imetiwa saini na Ndg. Shaibu Kaduara, Mfanyakazi wa Shirika Tawi la Pemba, na wakati huo alikuwa ni Afisa Utawala. Kitendo hiki kinaifanya Mikataba hiyo kukosa saini ya Meneja Mkuu wa Shirika ambae kwa mujibu wa Sheria Namba 3 ya mwaka 2006, kifungu cha 15(1), ndie Msimamizi Mkuu wa Masuala ya Utendaji wa Shirika (Ikiwa ni pamoja na kuingia katika Mikataba mbali mbali), na sio Afisa wa Kawaida. Uthibitisho wa saini hizo ni **(Kiambatanisho Nam 56).**

3.5.3 Udanganyifu wa Vyeti vya Kumalizia Masomo:

Pamoja na kasoro ya kuajiriwa wafanyakazi bila ya kutangazwa na kuomba kwa misingi ya sifa halisi na uwezo wao, Kamati pia ilipitia vyeti mbali mbali vya wafanyakazi hao vinavyothibitisha kumaliza na kuhitimu masomo yao. Katika zoezi hili, kama ilivyothibitika katika miaka iliyotangulia, kuna baadhi ya wafanyakazi wameshindwa kuwasilisha vyeti asili vya masomo (Original Certificates), lakini pia wapo walioghushi vyeti hivyo. Kwa kuzingatia ukubwa wa ripoti hii, Kamati inapenda kutoa mfano kwa Ndg. Omar Ali Juma, alieajiriwa

kama Fundi, kwamba ameshindwa kuwasilisha vyeti asili vya kumaliza masomo yake ya Sekondari katika Skuli ya Utaani, Pemba. Aidha, kadhia hii pia inahusika kwa Ndg. Moh'd Habib Iddi, aliewasilisha kopi ya Cheti cha Form III, bila ya kuwasilisha cheti halisi kilichohitajika na Kamati.

3.6.0 UAJIRI WA WAFANYAKAZI WA UNGUJA NA PEMBA KWA MWAKA 2011:

Katika mwaka wa 2011, Shirika lilifanya tena uajiri wa wafanyakazi wapya wa kudumu katika fani mbali mbali, Unguja na Pemba. Wafanyakazi hao ni 'Electrical Engineers' nafasi 4; 'Mechanical Engineers' nafasi 2; Computer/IT Engineer, nafasi 1; 'Mechanical Technicians' nafasi 2; 'Electrical Technicians, nafasi 20; 'Civil Technician' nafasi 1 na 'Procurement Officer', nafasi 1; 'Store Keepers' nafasi 4; Cashiers nafasi 3, Drivers nafasi 2, Meter Readers nafasi 3, na 'Secretaries' nafasi 2. Kama ilivyo utaratibu wa ajira, haja ya kuajiri wafanyakazi wapya, ilitangazwa katika vyombo vya habari, na kwa kupitia gazeti la Zanzibar Leo **(Kiambatanisho Nam 57)**, Kamati imepata taarifa za kutangazwa kwa nafasi hizo ambapo usaili baadae ulifuata na hatimae kuajiriwa kwa wafanyakazi hao. Pamoja na hali hiyo, kuna mambo kadhaa yamejitokeza katika uajiri wa wafanyakazi hao, ambapo Kamati inaona ni vyema yakafahamika. Mambo yenyewe ni haya yafuatayo:

3.6.1 Kutoridhika kwa baadhi ya Walioitwa katika Usaili, kwa hoja ya Upendeleo na Ubaguzi:

Kama tulivyokwisha eleza hapo juu, kwamba kati ya wafanyakazi walioajiriwa kwa mwaka 2011, ni pamoja na 'Cashiers' nafasi 3. Nafasi hizi ni kwa ajili ya Tawi la Pemba, ambapo Usaili huo ulijumuisha njia ya maandishi na njia ya maneno. Watu 17 waliitwa katika usaili na hatimae watu watatu kama ilivyyohitajika tokea awali, waliajiriwa na Shirika. Wafanyakazi wenyewe ni Ndg. Tauhida S. Salum; Ndg. Adnan A. Moh'd na Ndg. Moh'd H. Moh'd. Kufuatia hali hii, Ndg. Mrzuk H. Marzuk na Ndg. Rashid K. Shimel waliokuwemo katika Usaili na hawakufanikiwa kuajiriwa, walilalamika kwa kupeleka barua Tume ya Utumishi, Serikalini, kwa lengo la kufanywa uchunguzi wa kina juu ya suala hili **(Kiambatanisho Nam 58)**.

Aidha, Tume ya Utumishi Serikalini nayo ilipokea malalamiko hayo na kuwajuulisha wahusika mnamo Tarehe 29/02/2012 kupita barua yenye kumbu kumbu namba TUS/OR/MW/3/VOL.VII/66 ambayo katika taarifa hii ni **Kiambatanisho Nam 59** na mnamo Tarehe 13/04/2012 Tume ilimaliza uchunguzi wake na kujiridhisha kwamba, uajiri wa wafanyakazi hao 3 katika nafasi ya 'Cashier' umefanywa bila ya upendeleo na kwa usahihi mkubwa **(Kiambatanisho Nam 60**). Pamoja na maelezo hayo, kwa upande wa Kamati mambo yako tofauti. Kamati ilipokuwa inafanya mahojiano na wafanyakazi husika pamoja na vijana waliolalamika juu ya suala hili, lakini pamoja na kukutana na Uongozi wa Tume ya Utumishi Serikalini, mambo yafuatayo yamejitokeza:

3.6.2 Kuajiriwa kwa watu wasio na sifa na kuacha kuajiri wenye sifa zilizohitajika:

Kwanza tunapenda kukumbushia kwamba, kwa mnasaba wa malalamiko ya Vijana

wawili waliopeleka malalamiko yao kwa Tume ya Utumishi Serikalini, walidai kwamba, Uajiri wa Cashiers watatu haukufuata taratibu ikiwa ni pamoja na kukosa sifa za msingi zilizohitajika. Kwa upande wa Kamati, baada ya kupitia taarifa mbali mbali zilizowasilishwa kwake, imegundua kwamba, kuajiriwa kwa Ndg. Tauhida Suleiman Salum hakukufuata taratibu zilizowekwa. Kwa mfano, kama utarejea barua ya Shirika la Umeme iliyoeleza kwa maandishi kwa Tume ya Utumishi Serikalini, baada ya kutakiwa kufanya hivi kwa mujibu wa barua ya tarehe 28/03/2012 yenye kumbu kumbu namba TUS/OR/MW/3 VOL.VII/78 **(Kiambatanisho Nam 61)**, Ndg. Abbas Juma Faki, kwa niaba ya Meneja Mkuu wa Shirika aliieleza Tume kwamba, tarehe ya mwisho kupokea maombi ya nafasi hiyo ilikuwa ni 30/10/2011, **(Kiambatanisho Nam 62)**, na tarehe hii ndio pia imetakiwa kwa mujibu wa tangazo la Ajira hizo katika Gazeti la Zanzibar Leo. Hata hivyo, kwa mujibu wa barua ya maombi ya Ndg. Tauhida Suleiman Salum, maombi yake alipeleka Tarehe 04/11/2011, sawa na siku 4 za ziada baada ya tarehe ya mwisho wa kupokelewa kwake **(Kiambatanisho Nam 63)**. Hii ina maana kwamba, kupokelewa kwa maombi ya mfanyakazi huyu kunakiuka taratibu na ni sawa na kusema kwamba, kumepita upendeleo. Utathibitisha kwa uwazi zaidi na usahihi wake, kwa kufahamu kwamba, Ndg. Tauhida ni shemeji wa aliekuwa

Meneja Utawala wa Shirika, Unguja, Ndg, Moh'd Haji. Kwa hali hii, ni rahisi zaidi kufanyiwa upendeleo huo, hata kama muda wa tangazo unaelekeza vyenginevyo.

Aidha, kwa mujibu wa sifa zilizohitajika kwa ajili ya kazi ya 'Cashier', alitakiwa pamoja na sifa nyengine awe amehitimu na kupata cheti cha 'Accounting' wakati Ndg. Tauhida amemaliza masomo ya 'Islamic Banking and Finance' fani inayotofautiana na iliyohitajika (ingawaje inawiyana), huku walalamikaji kwa mfano Ndg. Marzuku Hussein Marzuik, amemaliza Kidato cha Sita na kuhitimu na kupata cheti cha Diploma ya 'Accounting' katika Chuo cha Uongozi wa Fedha, Chwaka **(Kiambatanisho Nam 64)**. Kwa maana hii, Kama Shirika lilizingatia sifa walizozihitaji, ni wazi kwamba, Ndg. Marzuk ambae pia alishiriki katika usaili, alikuwa na haki ya kuajiriwa zaidi kuliko Ndg. Tauhida ambae hakuwa na sifa zilizohitajika katika nafasi hiyo.

Aidha, kwa upande wa Muajiriwa, Ndg. Moh'd H. Moh'd, Kamati imejiridhisha kwamba, hakuwa na sifa zilizohitajika kwa sababu amesomea masuala ya Takwimu katika Kituo cha Mafunzo cha 'Eastern Africa Statistical Centre', kilichopo Dar es Salaam na ni sawa na kusema kwamba, hakusomea 'Accounting' kama vile Shirika lilivyotangaza na kuhitaji **(Kiambatanisho Nam 65)**. Aidha, Kamati imejiridhisha kwamba, Mfanyakazi huyu hakupeleka maombi ya kazi katika muda uliohitajika, na badala yake ameomba tokea tarehe 23/08/2010 huku tangazo la maombi ya nafasi hizi za kazi, likitoka tarehe 12/10/2011. Kukosa sifa zilizohitajika pamoja kushindwa kufuata taratibu za maombi, wakati walikuwepo waliona sifa hizo tena wenye elimu ya juu zaidi kuliko ile iliyohitajika, ila kwa kukosa tu jamaa ama wakubwa wa kuwabeba na kuwafanya kupata ajira, ni wazi kwamba hakuvumiliki na ni haki yao kupeleka malalamiko yao kwa Tume ya Utumishi Serikalini, ili angalau kuona vipi matatizo haya yangepaswa hushughulikiwa.

Linalowauma zaidi walalamikaji hawa ni Wazanzibari wenye haki kama wengine na zaidi kwa kuwa wamecheza pamoja na waombaji wengine ama kwa sababu pia wanaishi maeneo ya karibu, tukizingatia ukaribu, uhusiano na ukubwa wa Visiwa vyetu, wanajua fika kama ilivyoweza kufahamu Kamati kwamba, Ndg. Moh'd H. Mohd, ambae ameajiriwa akiwa hana sifa, ni Mjomba wa Meneja Utawala Pemba,

Ndg. Hafidh Tahir. Kwa ujumla, hali kama hii haiwezi kuvumiliwa na yoyote, na inakiuka Katiba ya Zanzibar na kwenda kinyume zaidi na misingi ya haki.

3.7.0 UAJIRI WA WAFANYAKAZI WA SHIRIKA-UNGUJA NA PEMBA(MWAKA 2011/2012):

Kama ilivyokwisha elezwa awali, kwamba kwa mwaka 2011, Shirika lilihitaji kuajiri wafanyakazi wapya wa kudumu katika nafasi zifuatazo, huku ikiambatanishwa na sifa zilizohitajika na hatimae kutangazwa katika gazeti la Zanzibar Leo la tarehe 12/10/2011. Nafasi hizo ni 'Electrical Engineers' nafasi 4 huku wakitakiwa kuwa na elimu ya 'Bachelor Degree in Electrical Engineering' au ilinayolingana kutoka Chuo kinachotambulika na kushurutishwa umri wa muombaji usizidi miaka 32, ingawaje uelewa wa Kompyuta ni faida. Nafasi ya pili ni 'Mechanical Engineers' waliotakiwa wawe na elimu ya 'Bachelor Degree in Mechanical Engineering au inayolingana na hiyo kutoka Chuo kinachotambulika na Umri usiozidi miaka 32. Nafasi ya tatu ni Computer/IT Engineer, alietakiwa kuwa na elimu ya 'Bachelor Degree in Computer Science au information and Communication Technology' na umri usiozidi miaka 32.

Kwa upande wa nafasi 'Mechanical Technicians' nafasi 2 zilihitajika kwa ajili ya uajiri wakishurutishwa kuwa na elimu 'Ordinary Diploma au Full Technician Certificate in Mechanical Engineering na umri usiozidi miaka 25, huku uelewa wa kompyuta ni faida. Electrical Technicians, nafasi 20 zilihitaji uajiri mpya kwa Unguja na Pemba, huku wakishurutishwa kuwa na Ordinary Diploma au Full Technician Certficate in Electrical Engineering na umri usiozidi miaka 25, wakati uelewa wa Kompyuta ukiwa ni sifa ya ziada. Shirika pia lilihitaji kuajiri 'Civil Technician' nafasi 1 kwa upande wa Unguja lakini kwa sharti la kuwa na elimu ya 'Ordinary Diploma au Full Technician Certificate in Civil Engineering na umri usiozidi miaka 25, wakati uelewa wa Kompyuta ni ziada.

Shirika pia lilihitaji kuajiri 'Procurement Officer', nafasi 1 huku likishurutisha muombaji wa nafasi hiyo awe na elimu ya Degree in Procurement Logistics and Materials Management na umri usiozidi miaka 32, ingawaje uelewa wa Kompyuta ni sifa ya ziada. 'Store Keepers' nafasi 4 zilihitaji kuajiriwa kwa watu wenye

elimu ‘Advance Diploma in Procurement and Materials Management’ (Unguja na Pemba) na umri usiozidi miaka 25. Aidha, ‘Cashiers nafasi 3 zilihitaji kujazwa kwa upande wa Tawi la Pemba, huku wakitakiwa na elimu ya ‘Form IV pamoja na Cheti cha ‘Accounting’ na Cheti cha Mafunzo ya Komputa, huku umri nao usizidi miaka 25. Nafasi 2 za Madereva nazo zilihitaji wafanyakazi wapya wakiwa na leseni ya daraja C na kumaliza masomo ya Sekondari, huku umri ukitakiwa usizidi miaka 25.

Nafasi 3 za Wasomaji Mita nazo zilihitaji kuajiriwa wafanyakazi wapya, ambao walitakiwa kuwa na elimu ya Form IV, huku Cheti cha Ufundi, VETA ni faida, na umri usiozidi miaka 25. Na nafasi za mwisho ni za ‘Secretaries’ nafasi 2, waliotakiwa wawe na Elimu ya ‘Form IV, Cheti cha Mafunzo ya Kompyuta na umri usiozidi miaka 25. Baada ya kuzipitia sifa zilizohitajika, na kufanya usaili wa Waajiriwa waliohusika, Kamati imegundua mambo yafuatayo, kwa upande wa Unguja na Pemba:

3.7.1 Kukiukwa kwa taratibu za maombi ya kazi, Tawi la Pemba:

Kifungu cha 3(7) cha Kanuni za Utumishi za Shirika, kinaeleza utaratibu wa kuomba kazi, ambapo paragrafu ya awali (a) inaeleza kwamba, ‘Maombi yote ya nafasi za kazi katika Shirika yatawasilishwa kwa Meneja Mkuu kwa utaratibu uliowekwa’. Maelezo ya kifungu hiki yanafahamisha kwamba, maombi yote yaliyotolewa matangazo yake kama tulivyokwisha eleza hapo juu, yalitakiwa yafike kwa Meneja Mkuu wa Shirika. Aidha, utaratibu ulioelezwa katika gezeti hilo la Zanzibar Leo la tarehe 12/10/2011, ni kutaka kila muombaji, bila ya kujali Unguja ama Pemba, kupeleka maombi yake kwa Meneja Mkuu wa Shirika.

Pamoja na maelekezo haya, maombi yote yaliyofanywa Pemba, yamepelekwa kwa Meneja wa Tawi, Pemba. Na jambo la kushangaza ni Uongozi wa Shirika, pamoja na Bodi yake kukubaliana na maombi haya wakati yanakiuka taratibu zilizowekwa, na kisheria ni sawa na kupelekwa kwa mtu asiye na mamlaka ya kuyashughulikia, hivyo haikupaswa kwa Shirika, kuendelea kuyakubali maombi ambayo, yamekiuka masharti yaliyowekwa katika taarifa ama tangazo la nafasi za kazi, lakini pia yanakiuka taratibu za Kanuni za Utumishi za Shirika.

3.7.2 Kutotimizwa kwa sharti la Umri, kinyume na maelekezo ya Maombi:

Tunafahamu kwamba, katika matangazo iliyoyatoa Shirika kwa waombaji wa mwaka 2011, **(Kiambatanisho Nam. 66)**lilihitaji kwa kila muombaji kwa mujibu wa nafasi atakayoiombea kutovuka umri uliowekwa. Jambo la msisitizo ni kwamba, umri huu umewekwa huku ukishurutishwa katika maombi, ili kumfanya Muombaji afahamu, na hatimae Shirika liweze kupata wafanyakazi wenye nguvu watakaoweza kulitumikia kwa muda mrefu. Hata hivyo, sharti hili limekiukwa kwa kiasi kikubwa katika maombi ya waombaji na jambo la kushangaza ni Shirika, kukubali kuwaajiri huku kabla litoa sharti hilo, bila ya kuzingatia uhalisia wa waombaji. Kwa mfano, Ndg. Ali Haji Makame, alieajiriwa kama Afisa Manunuzi (Procurement Officer), alitakiwa asizidi miaka 32, ingawaje yeye ameajiriwa akiwa na umri wa miaka 34 **(Kiambatanisho Nam 67).**

Aidha, suala hili pia linamhusu Ndg. Fadhil Makungu Is-Hak mwenye umri wa miaka 30, wakati nafasi yake ya kuajiriwa (Mechanical Technicians), ilitaka asizidi miaka 25 **(Kiambatanisho Nam 68).** Kwa mnasaba wa maelezo haya na ushahidi ulionukuliwa, ni wazi kwamba, Shirika halikuzingatia sifa ya Umri wa waombaji wake, kinyume na maelelezo yaliyotolewa katika matangazo ya maombi. Na kwa kuwa mamlka ya idhini ya Uajiri hufanywa na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika, huku Meneja Mkuu na watendaji wenzake ni watekelezaji wa maagizo ya Bodi, ni wazi kwamba, wamekiuka maelekezo hayo, na picha inayojengeka ni kwamba, Uongozi wa Shirika hutekeleza majukumu yao kinyume na maagizo ya Bodi.

3.8.0 WAFANYAKAZI WALIOFICHWA NA KUWASILISHWA KWA TAARIFA ZAO MBELE YA KAMATI:

Pamoja na Kamati kufanya juhudi zote za kutaka kuwasilishiwa mbele yake, Waajiriwa wote wa Shirika kuanzia mwaka 2008 hadi 2012, kuna wafanyakazi taarifa zao hazikuwasilishwa mbele ya Kamati, mpaka pale Kamati ilipotumia mbinu za ziada za kupata taarifa za kwamba wameajiriwa na Shirika, na hatimae kutaka taarifa zao. Kwa lugha nyengine, kitendo hiki kinapingana na kifungu cha 9 cha Sheira Namba 4 ya mwaka 2007, kinachoeleza Wajibu wa Ofisa yoyote wa Serikali (Ikiwa ni pamoja na Watendaji wa Shirika), kumpatia Mjumbe yoyote wa Baraza taarifa anazozihitaji, isipokuwa tu, labda taarifa hiyo inahusika na masuala ya kiusalama.

Kwa hili, Kamati kupitia Wajumbe wake imeomba na kuhimiza mara kadhaa bila ya mafanikio. Kwa mnasaba wa taarifa hizo zilizopatikana baadae, baada ya Kamati kulazimisha kupatiwa, pamoja na mambo mengine zinahusika na Waajiriwa watano wa Shirika kwa mwaka 2009/2010 na mwaka 2011/2012, ambapo mambo yafuatayo yamejitokeza.

3.8.1 Kufanywa Uajiri bila ya kuzingatia sifa halisi iliyohitajika na Shirika:

Itakumbukwa kwamba, katika maelezo yetu ya awali tulieleza kwamba, mbali na mwaka 2011 ambapo Shirika lilifanya mageuzi makubwa ya Uajiri, uajiri uliokuwa kabla ya hapo haukufuata taratibu zote za ajira wakati Kanuni za Utumishi na sheria ya Shirika zilikuwepo kabla ya mwaka 2011. Miongoni mwa kasoro hizo ni kuajiriwa wafanyakazi bila ya kuzingatia sifa halisi zinazostahiki na hili kwa kiasi kikubwa limeathiri haja ya kutangazwa kwa uwazi kwa nafasi za ajira hizo na hatimae, wafanyakazi ama waliotumikia Miradi kadhaa iliyosimamiwa na Shirika, kwa mfano Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini ndio walioajiriwa, huku hakuna usaili uliofanyika. Aidha, wafanyakazi waliokuwa wanaajiriwa kama wa muda, ndio waliajiriwa wa kudumu kwa mnasaba wa haja iliyokuwepo.

Kwa upande wa wafanyakazi hawa watano waliofichwa taarifa zao, suala hili la kuajiriwa bila ya vyeti asilia (original) na badala yake kuaminiwa na kutakiwa kuleta vyeti hivyo baadae liliendelea. Kwa mfano Ndg. Abubakar Chum Mwinyi, alieajiriwa mwaka 2009 kama Mfanyakazi wa kudumu na Msomaji Mita, alipoomba ajira, pamoja na kuambatanisha na vyeti vyengine, alieleza Shirika kwamba, amemaliza masomo ya Kidato cha Pili (Form II) katika Skuli ya Sekondari ya Kiembe Samaki mwaka 2003, lakini hajaambatanisha cheti cha msingi (Original) ya cheti hiki **(Kiambatanisho Nam 69)**. Hali hii ililifanya Shirika, baada ya kupita miaka miwili ya Uajiri, ndipo alipotakiwa kuwasilisha angalau kivuli cha cheti chake si zaidi ya tarehe 15/02/2012.

Tunachosisitiza kufahamika ni kwamba, kwa mujibu wa barua hiyo ya tarehe 8/02/2012 tuliyoifanya **Kiamtabanisho Nam 70** cha ripoti hii, Mfanyakazi huyu sio tu kwamba hakuwa na 'Original Certificate' ya kumalizia masomo yake ya Kidato cha II, lakini pia hata cheti chenyewe hakuwa nacho. Na tuthibitishe maneno haya kwa nukuu ifuatayo ya barua hiyo, "……Unajuulishwa kwamba, kumbu kumbu zilizomo ndani ya OPF yako zinaonesha (ardhihali ya

kuingia kazini), kiwango chako cha elimu ni (Kidatu cha 3)[9] bila ya kuwemo cheti husika".

3.8.2 Kutowasilishwa kwa maombi ya kazi katika Uajiri wa baadhi ya Wafanyakazi hawa:

Pamoja na kifungu cha 11(1) cha Kanuni za Utumishi za Shirika za mwaka 2005, kueleleza ulazima wa kila muombaji wa ajira katika Shirika kujaza fomu maalum ya maombi, ambayo kwa kawaida ni barua ya maombi ya kazi, Mfanyakazi huyu, Ndg. Abubakar Chum Mwinyi hajathibitishwa na Kamati kwamba alipeleka maombi ya kazi kwa Meneja Mkuu wa Shirika, wakati alipotaka kuajiriwa. Suala kama hili pia linamhusisha Ndg. Jokha Zubeir Mtemvu akiwa ni miongoni mwa wafanyakazi waliofichwa kwa Kamati, aliaejiriwa kama Mpokea Simu, kama pia linavyohusika kwa Ndg.Ameir Makame Mlenge, alieajiriwa mwaka 2009 kama Msoma Mita. Na kama pia linavyohusika kwa Ndg. Mbaraka Nyange Hamadi, aliaejiriwa kama Msoma Mita, mwaka 2011.

3.9.0 MAMBO MENGINE YA UJUMLA YALIYOJITOKEZA JUU YA SUALA LA AJIRA UNGUJA NA PEMBA:

Suala la msingi ambalo kila mtu angeweza kujiuliza na kwa mnasaba wa Hadidu rejea inayohusika na Ajira, ni vipi Kamati ingeweza kuthibitisha upendeleo unaofanyika katika taratibu nzima za Ajira katika Shirika la Umeme. Na ndio maana kwa upande wa Kamati, kama tulivyokwisha eleza awali, kwamba suala hili lilihitaji kuonana na watumishi hao pamoja na kuangalia upatikanaji wa fursa mbali mbali ndani ya Shirika, iwapo zina upendeleo katika kupatikana kwake lakini pia fursa (Privilege) zinatolewa kama vile nafasi za masomo (Ruhusa na ufadhili wake); safari za kikazi ambazo zinawagusa watu wachache tu, pamoja na kwamba baadhi ya safari hizo zingewahusisha watu wengine hasa mafundi, lakini pia hata fursa ya mgao wa matumizi ya uniti za umeme ikiwa pia ni pamoja na ile fursa ya kugaiwa fedha kwa ajili ya Sikukuu. Pamoja na wingi wa kasoro hizo zinazojika katika kuonesha dalili za upendeleo ambapo Kamati inaamini hufanywa

[9] Ifahamike kwamba, barua hiyo imekosewa iliposema Kidatu cha 3, kwani katika Ardhihali husika ni Kidatu cha 2 na hata uwazi wa jambo hili unathibitika na ukweli kwamba, kwa mwaka 2003 alipomaliza masomo yake Mfanyakazi huyu, hakukuwa na mitihani ya Kidatu cha 3.

makusudi na Managementi ya Shirika, katika ripoti hii tutafafanua zaidi upendeleo wa masomo na athari zake katika kubadilishiwa misharaha na upandishwaji wa vyeo, kwani kuna mahusiano makubwa na hoja yetu tunayoizumgumzia. Hivyo basi, ni vyema tukapata ufafanuzi ufuatao:

3.9.1 Mafunzo ya Kazi:

Hebu na tuanze kwa kuangali namna gani Shirika linafanya upendeleo katika utoaji wa fursa za mafunzo ya ndani ama nje ya nchi. Katika hili, kwanza ieleweke kwamba, kama zilivyo Taasisi nyingi za Serikali, Shirika la Umeme nalo hutumia fedha nyingi katika kutoa fursa ya mafunzo kwa watendaji wake. Linafanya hivi kwa lengo la kujenga uimara wa nguvu kazi katika kukabiliana na mabadiliko ya kiutendaj,ili Shirika liweze kuwa na ufanisi katika utendaji wake na lipate tija na kwa upande wa wananchi waendelee kupata huduma zilizo bora wakati wote. Jambo hili likitekelezwa ipasavyo, huwa ni moja kati ya motisha kwa watendaji kazi na kuongeza ufanisi unaohitajika; lakini lisipotekelezwa vyema basi huwa ndio chanzo cha mgogoro na uvunjwaji moyo kwa wale wanaokoseshwa nafasi za masomo hayo.

3.9.2 Utekelezaji wa Mafunzo hayo :

Ijapokuwa kwa mtazamo wa kawaida unaonesha dhahiri namna ambavyo Shirika limejitahidi kuwasomesha watendaji wake, lakini ukweli ni kwamba fursa hizo hazikuwa zikitolewa kwa watu wote wenye sifa ya kuzipata. Kamati imejiridhisha kwamba kuna upendeleo wa hali ya juu ambao hauzingatii masharti ya msingi ya utoaji wa mafunzo hayo.

Inaeleweka kwamba kitu cha mwanzo cha kuzingatia katika utoaji wa ruhusa ya kwenda kwenye mafunzo ya kazi, ni mahitaji ya Taasisi yenyewe. Haya yanapatikana endapo Taasisi itafanya uchambuzi wa kujua ufanisi wake, kwa maana ya uwezo wa watendaji wake (Performance Appraisal) na kugundua kwamba kuna umuhimu wa mafunzo. Itafanya tena uchambuzi wa mahitaji hayo (Training Need Assessment) na baadae kujua ni aina gani ya mafunzo yanayohitajika, na ni watendaji wepi wanaohusika na uwezo wa taasisi yenyewe kukidhi gharama hizo na muda halisi wa mafunzo yenyewe.

Ni dhahiri kwamba mahitaji ya mafunzo kwa Taasisi yoyote ni makubwa kulinganisha na bajeti ya Taasisi yenyewe, na kwa maana hiyo ni busara kubwa katika kuangalia mpango wake wa mafunzo lakini vile vile katika kukidhi haja hiyo, fursa hutolewa kwa wale ambao wanakusudia kusoma kwa kujilipia wenyewe ama kwa njia ya mkopo au kwa kutafuta ufadhili kwa njia nyengine yoyote wanayoijua, ilimradi tu wapate ruhusa ya muajiri, ikizingatiwa mno fani anayokweda kuisomea ni ya maslahi kwa Taasisi husika.

Utekelezaji wa jambo hili kwenye Shirika haukuwa mzuri na kuna kila sababu ya kusema kwamba umetawaliwa na maamuzi ya upendeleo. Shirika limewakatalia ruhusa wafanyakazi ambao wana sifa na kuwanyima hata mkopo wa kujilipia wenyewe na kutoa fursa hiyo kwa wale wasio na sifa hizo kwa kuwapa ruhusa na ufadhili pamoja na kwamba wao wenyewe wamejizatiti kujilipia wenyewe gharama hizo.

Kamati ilipata mifano ya watendaji hao, ambao pamoja na ukweli kwamba walikuwa na sifa za kuweza kupewa mafunzo ya kazi na Shirika kwa nia ya kuleta ufanisi wa kweli na wao wenyewe kuomba ufadhili, lakini vilevile kuwa tayari hata kujilipia wenyewe mradi tu wapate ruhusa kwa muajiri wao. Hata hivyo ushahidi unaonesha kwamba Shirika liliwakatalia tena bila ya sababu yoyote ya msingi.

Kwa mfano, **Ndg. Mohammed Khamis Juma**, Mfanyakazi aliekuwa akifanya kazi kama Mkaguzi wa Hesabu za Ndani (Internal Auditor) Tawi la Shirika Pemba, aliomba ruhusa ya kujiunga na Chuo Kikuu cha Dodoma katika mafunzo ya Shahada ya Uzamili katika uhasibu kwa mwaka wa masomo wa 2008/2009. Barua ambayo ameiandika tarehe 17 Septemba, 2008. Meneja Mkuu wa Shirika alimkatalia ombi lake hilo tena bila ya kuainisha sababu yoyote kwa barua ya tarehe za Septemba 2008 yenye kumbukumbu Nam. ZECO/PEM.149 ikiwa na sentensi yenye kubeba jawabu hilo inayosomeka **“Ombi lako la kutaka ruhusa ya kujiunga na masomo halikukubalika”.** Yaano, hakukuwa na maelezo ya sababu zozote isipokuwa aendelee kuwa mstahamilivu hadi mwakani 2009/2010 **(Kiambatanisho Nam 71).**

Ndugu Mohammed kwa kutambua kuwa labda Shirika halikuwa na fedha, basi aliliandikia juu ya kupatiwa mkopo kwa madhumuni ya kujisomesha mwenyewe (Tarehe 31/7/2008) na Uongozi wa Shirika kupitia barua yake ya Tarehe 6/8/2008 nambari ya kumbukumbu ZECO/PE/M.149 ulimkatalia tena. Kutokana na hali hiyo, Mfanyakazi huyu alilazimika kujisomesha kupitia nguvu zake mwenyewe **(Kiambatanisho Nam 72)**.

Hali kama hiyo pia imemkuta **Ndg. Fadhila Abdallah Mbarawa**, ambae nae aliajiriwa Mwezi wa Januari, 2008 kama Fundi (Technician) akiwa na mafunzo ya Cheti cha Ufundi (Full Technician Certificate) katika fani ya 'Electrical Engineering', na kuanza kazi ya ufungaji wa mita za Tukuza na hatimae kuhamishiwa Kitengo cha Masoko.

Ndg. Fadhila aliomba ruhusa ya kwenda masomoni baada ya kukubaliwa na Chuo, mnamo tarehe 28/09/2010. Nae aliomba ruhusa hiyo kwa muajiri wake pamoja na udhamini. Mafunzo hayo yalikuwa katika kiwango cha Shahada ya Kwanza katika fani hiyo hiyo ya umeme, kwa kuamini kwamba kufaulu kwake kutaleta tija kwa Shirika pamoja na yeye mwenyewe. Hata hivyo, kwa bahati mbaya sana Shirika halikuona umuhimu wa jambo hilo kwa upande wake na alinyimwa ruhusa ya kuitumia fursa hiyo, kupitia barua ya tarehe 25/11/2010 yenye kumbu kumbu namba ZECO/PF/F.33, yaani baada ya miezi miwili tokea apeleke maombi, wakati Mfanyakazi huyu akifanya kazi hapo hapo katika Afisi ya Meneja wa Tawi, Pemba **(Kiambatanisho Nam 73)**.

Ndg. Fadhila kwa busara alizokuwa nazo na kuthamini elimu katika kazi zake, hakuvunjika moyo na mwaka uliofuata aliomba tena mafunzo hayo kupitia barua yake ya tarehe 4/4/2011. Hata hivyo, Meneja huyu huyu wa Tawi, Pemba aliendelea tena kutothamini haja ya kumsomesha mfanyakazi wake huyu na ndipo tarehe 14/4/2011 alimjibu kwa barua yenye kumbu kumbu namba ZECO/OPF/F.33 kwa ufupi kabisa kwamba ruhusa hiyo haijakubaliwa, kama hapa tunavyonukuu:

> "Uongozi wa Shirika unapenda kukujuulisha kuwa ombi lako la ruhusa ya masomo kwa mwaka 2011/2012 halijakubaliwa" (**Kiambatanisho Nam 74).**

Bila ya shaka baada ya mwaka tu Mfanyakazi huyu alijijutia kwa nini atake kusoma na ndipo mnamo tarehe 01/03/2012 alipewa uhamisho wa ndani kutoka Kitengo cha Ufungaji Mita za Tukuza na kupelekwa Kitengo cha Marketing, sehemu ambayo sio fani yake ili kumkomesha na kumtaka akatishe haraka hamu na juhudi zake za kutaka kujiendeleza katika fani yake aliyoisomea. **(Kiambatanisho Nam 75).**

Kwa upande mwengine basi, kuna mfanyakazi **Ndg. Mwawanu Ali Juma** ambae ameajiriwa kama Karani Masijala. Nae, mnamo siku ya Tarehe16/2/2009 aliomba ruhusa ya kuhudhuria masomo katika Chuo cha 'London Education and Development' katika fani ya 'ABE- Business Information System' ngazi ya Stashahada ya Juu (Advanced Diploma), huku akiliahidi Shirika kwamba angelipiwa gharama zote hizo za mafunzo yake hayo na familia yake **(Kiambatanisho Nam 76)**. Gharama ambazo zimeambatanishwa katika barua za Tarehe 28/01/2009 kutoka Chuoni ni £3600.00 ikiwa ni gharama za malazi. Wakati huo huo kwa tarehe hiyo hiyo (28/01/2009) Chuo kilithibitisha malipo ya awali yaliyofanywa na Ndg. Mwawanu Ali Juma ya Ada ambayo ni £700 wakati kwa mwaka ni £ 1440 mafunzo ya miaka miwili na nusu.

3.9.3 Kilicholeta Utata.

Barua yake ya maombi ya ruhusa ya masomo iliyokubaliwa na Shirika, ni ya tarehe 16/2/2009 ambayo alilithibitishia Shirika kwamba familia yake ndiyo itakayolipia gharama za mafunzo yake. Ambapo kwa mujibu wa barua hiyo ya maombi yake pamoja na barua aliyojibiwa kutoka chuoni ya kuthibitisha kuchaguliwa kwake kwenye mafunzo hayo, ni ya tarehe 28/01/2009 zikiwa na nambari ya uwanafunzi UCO/TZN/364, na jina la Chuo hicho ni zinathibitisha kwamba chuo hicho alichochaguliwa ni 'London Education And Development Academy (UK)', na mafunzo aliyoyaomba ni ABE- Business Information System ngazi ya Advanced Diploma **(Kiambatanisho Nam 77)**. Hilo amelithibitisha yeye mwenyewe kwenye barua yake ya maombi, kwamba ada ya mafunzo anayotakiwa kulipia Chuoni hapo, ni £3600 na muda wa mafunzo yake, ni miaka miwili na nusu kutoka mwezi Machi, 2009 hadi Julai, 2011.

Aidha, pamoja na kwamba aliahidi Shirika kwamba familia yake ndio itakayomlipia na Shirika kumruhusu kwenda masomoni likiamini tu kwamba halitatoa fedha zake kwa mafunzo hayo, Kamati ilijuulishwa kwamba, Mwawanu aliandika barua kuliomba Shirika, msaada wa gharama za mafunzo pamoja na kuambatanisha na 'Invoice' ya tarehe 24/5/2010, pamoja na barua ya Chuo ambacho ni tofauti na kile alichoruhusiwa na Shirika. Barua na 'invoice' hizo, zina jina tofauti na Chuo husika pamoja na aina ya mafunzo na muda wenyewe; wakati barua ya awali inayotoka Chuo cha 'London Education And Development Academy' ina jina la Chuo cha 'City Business College'. Halikadhalika jina la mafunzo yenyewe katika barua ya mwanzo (iliyoruhusiwa na Shirika), muhusika ameomba kuhudhuria mafunzo ya 'ABE – Business Information System' ngazi ya 'Advanced Diploma' wakati barua ya msaada wa gharama za masomo inaonesha muhusika amesomea 'Business Studies na Invoice' inaonesha mafunzo ya Management Studies ngazi ya Diploma ya Kawaida. Halikadhalika muda wa mafunzo nao ni tofauti, kwani Barua ya awali inaonesha kuwa muda wa mafunzo ni kutoka Tarehe 10/3/2009 hadi Julai, 2011 wakati barua ya pili ni kutoka Tarehe 21/4/2009 hadi Tarehe 31/8/2010 na Invoice inaonesha kutoka mwezi Agosti, 2010 hadi Februari, 2012 **(Kiambatanisho Nam 78).**

Jambo jengine ni kwamba, inaonekana kumbe Shirika la Umeme lilikuwa limemfadhili mfanyakazi huyu katika mafunzo hayo tangu awali kwani katika maombi yake ya Viza, Meneja Mkuu wa Shirika aliuhakikishia Ubalozi wa Uingereza Nchini Tanzania kwamba Shirika ndilo linalogharamia mafunzo hayo ikiwemo Ada, Malazi, Usafiri na gharama nyenginezo, kama inavyosomeka nukuu ya barua ya Meneja Mkuu kwa Ubalozi wa Uingereza kwamba **"Our Organization is confirming for sponsoring for the whole period of her studies in U.K including her school fees, Accommodaton, Tuition fees, Transport and any other expenses"**. Yaani, (Taasisi yetu (Shirika la Umeme) inahakikisha kufadhili masomo ya Mfanyakazi wetu huyu kwa muda wote wa masomo yake nchi Uingereza, ikiwa ni pamoja na ada ya masomo, gharama za malazi, usafiri, na ghrama nyenginezo). Haya yanathibitishwa na Barua ya SHIRIKA ya Tarehe 18/2/2009 yenye kumbukumbu Nam. ZECO/MFU/VOL.1/31 **(Kiambatanisho Nam 79)**.

Suala hilo pia limethibitishwa tena na Meneja Mkuu kwenye fomu ya maombi ya fedha za kigeni inayotolewa na Afisi ya Katibu wa Baraza la Mapinduzi, ambapo kipengele nambari 8 cha maelezo ya msafiri kinachoeleza anaegharamia gharama za safari kilichojazwa kwa uwazi kabisa kwamba, anaegharamia ni ZANZIBAR ELECTRICITY CORPORATION. Yaani (Shirika la Umeme la Zanzibar). Fomu hiyo ilijazwa na kusainiwa Tarehe 19/2/2009 **(Kiambatanisho Nam 80)**.

Hii inaonesha kwamba, kwa mfanyakazi huyu tangu awali Shirika lilikuwa na nia ya kumfadhili masomo yake na ile barua aliyoiandika ya Tarehe 16/2/2009 kwa Shirika ilikuwa ni geresha tu, kwani haiwezikani hata kidogo kwamba mtumishi huyo aandike barua ya kulihakikishia Shirika kwamba gharama za masomo hayo yatalipwa na familia yake Tarehe 16/2/2009, lakini Tarehe 18/2/2009 na Tarehe 19/2/2009, Shirika lithibitishe kwa Ubalozi wa Uingereza nchini na kwa Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi kwamba lenyewe ndio Mdhamini wa mfanyakazi huyo kwa ajili ya kumlipia gharama za mfunzo yake na mambo mengine yote yanayohusiana na kufanikisha masomo hayo. Jambo ambalo limefanyika ndani ya siku mblili tu na wala halikuja kwa malalamiko ya baadae ya kumsaidia endapo atakuwa amekwama katika malipo ya ghrama zilizokusudiwa, wakati huo pengine tayari anaendelea na masomo yake Uengereza.

Hata hivyo Ndg. Mwawanu Ali Juma kuthibitisha kwamba amehitimu mafunzo yake ya Nchini Uengereza, Kamati imefanikiwa kuwasilishiwa vyeti viwili. Kimoja ni cha ‘Graduate Diploma in Management’ kilichotolewa Tarehe 28/9/2011 na chengine ni ‘Diploma in Business Studies’ kilichotolewa tarehe 21/09/2010, Chuo ni City Business College kilichopo Uingereza chini ya Bodi ya ICM.

Suala la ufadhili wake, aina ya mafunzo, chuo alichosoma na kile alichoomba mwanzo pamoja na kiwango cha malipo vimeibua maswali mengi ambayo majibu yake ni kwamba, kuna udanganyifu ambao umepangwa kwa makusudi katika suala zima la kuonesha ni kwa namna gani alivyopewa nafasi hiyo kwa kupendelewa.

Kuna kila sababu ya kuamini juu ya upendeleo huu. Kwanza ajira yake ni Karani Masjala, aina ya mafunzo aliyokwenda kuyasomea ni ya ‘Business Management’

ambayo hayaendani na kazi yake. Lakini jengine, mafunzo hayo hayakuwa kwenye mpango (Training Programme) wakati huo huo Shirika halikuwa na mahitaji ya mtu wa aina hii. Kwani pamoja na kumgharamia huko lakini nafasi yake ya kazi ilibaki pale pale ya Ukarani Masjala na kwa maana hiyo, ile elimu aliyoipata nchini Uingereza haitumiki kwenye Shirika, kama kuitumia basi muhusika ataitumia katika maeneo mengine. Alichoneemeka yeye binafsi ni marekebisho ya mshahara wake (Barua yenye kumbukumbu Nam. ZECO/OPE/M.158 ya Tarehe 6/12/2011 inahusika) na (Barua ya Tarehe 28/11/2011) **(Kiambatanisho Nam 81)**.

Wakati **Ndg. Mohammed Khamis Juma** kama tulivyokwisha mueleza hapo juu, alikuwa anaomba mafunzo kwa kazi anayoifanya, na kwa uwazi yalionekana kwamba ni mahitaji ya Shirika kwani hadi Kamati inatembelea Shirika Tawi la Pemba halikuwa na Mkaguzi wa Ndani. Aidha, kama pia tulivyokwisha eleza katika hoja nzima ya Upotevu wa fedha katika Shirika hili Tawi la Pemba, miongoni mwa sababu zake ni kukosekana kwa Mkaguzi wa Ndani aliyepo huko Pemba. Sasa kama Uongozi wa Shirika ulihitaji kuangalia suala hili kwa ukaribu mno na upeo wa mafanikio kwa maslahi yake, ni kwa nini ushindwe kumuendeleza Mfanyakazi aliyepo kwa gharama ndogo zaidi kuliko fedha zinazopotea?.

Kwa maana hiyo Kamati ilipata mashaka makubwa mno juu ya namna na sababu ambayo imemkosesha nafasi ya ufadhili mtumishi huyu au hata huo mkopo. Hasa ikizingatiwa kwamba, nafasi aliyonayo ni muhimu sana kwake lakini vile vile utendaji wake yeye binafsi na hamu ya kazi katika kuliendeleza Shirika, ungelilisaidia sana Shirika hili kujiendesha kwa faida. Aidha, Vigezo hivyo hivyo pia vinapatikana kwa watumishi wengine ambapo Ndg. Subira Omar ambae aliomba nafasi ya kusoma akakataliwa na hatimae baadae alikubaliwa.

Kwa kuunganisha na mfano wa **Ndg. Fadhila Abdallah Mbarawa** ambae si tu alikosa ufadhili lakini hata ile ruhusa ya kwenda masomoni. Hii ni tafsiri na taswira yenye kuonesha ni kwa kiasi gani hali ya upendeleo wa waziwazi ambao katika ajira (Utumishi) ya Shirika upo na ambao unarudisha nyuma maendeleo ya watumishi na kulitia hasara Shirika kutokana na kukosa rasilimali watu zenye upeo na uwezo mkubwa wa kazi wenye kuleta ufanisi na badala yake raslimali fedha kutumika bila ya kuleta tija, na matumizi yake ni kwa maslahi ya watu binafsi.

Kamati iliarifiwa kwamba Ndg. Fadhila Abdalla Mbarawa alimuandikia muajiri wake barua mnamo Tarehe 5/1/2010, ya kuomba masomo katika ngazi ya Shahada ya Kwanza (Electric Engineering) na kukataliwa kwa barua ya Tarehe 22/1/2010 (ZECO/PF/F.33). Hata hivyo, hakukatika tamaa na hamu yake ya kupata fursa ya kusoma, haikukomeshwa na majibu ya awali. Hivyo, alijaribu tena kuandika Tarehe 28/9/2010 na kujibiwa Tarehe 25/11/2010 vile vile akiwa amekataliwa sababu zikiwa ni kwamba masomo lazima yawe kwenye mpango (Training Programme) na vile vile yasaidie utendaji wa Afisi. Sababu ambazo hazikujulikana kabisa wakati wa maombi ya **Ndg Mwawanu Ali Juma**, yalishughulikiwa siku moja tu baada ya maombi yake na kupewa fedha za masomo tena za kigeni.

Baada ya kukataliwa fursa hiyo, Ndg. Fadhila aliakhirisha kujiunga na Chuo kwa tamaa ya kwamba mwaka unaofuata atakuwemo kwenye mpango huo na akamkumbusha muajiri wake Tarehe 4/4/2011 juu ya nia yake hiyo na Tarehe 14/4/2011 (ZECO/OPF/F.33) akajibiwa kwamba aendelee kusubiri tu na hapakuwa na sababu tena kama zilivyoanishwa kwenye barua za awali. Hapa tena Shirika lilikosa hata sababu za kumdanganya badala yake ni majibu ya kuendelea kuvuta subra **(Rejea Viambatanisho Nam 73 na 74)**.

Kesi hizi za kuomba ruhusa ya masomo kwa wafanyakazi wa Shirika, lakini Shirika hukataa kuwasomesha, ni mashuhuri sana katika utendaji wa Shirika. Kwani hata Ndg. Aisha Omar Khamis aliyeomba tarehe 10/03/2011 alijibiwa kwamba Shirika haliwezi kumsomesha eti kwa sababu masomo yake hayamo katika mpango wa mafunzo. Masaibu haya pia yamewakumba Ndg. Saleh Mussa Alawi na hata Ndg. Salum Mussa Alawi **(Kiambatanisho Nam. 82).**

Jambo la kushangaza zaidi ni kwamba Shirika hili hili linasomesha wafanyakazi wengine ndani ya mwaka huo huo walioomba wenzao, ila wao labda kwa sababu wana hadhi tofauti na wengine, lakini hatimae husomeshwa tena kwa gharama kubwa, tena husomeshwa bila ya kuzingatia nafasi zao za kazi. Basi jengine la kufahamu ni hili lililomsibu Ndg. Othman Faki Omar kupitia barua ya tarehe 28/06/2011 alijibiwa kwamba:

"Shirika linafuraha kutaka kujiendeleza kimasomo kwa maendeleo ya Shirika na wewe binafsi. Hata hivyo, kutokana na taaluma uliyonayo ya fani yako ya Mechanic Technician tunaihitaji hivi sasa haitowezekana upatiwe mafunzo ya I.T"**(Kiambatanisho Nam 83)**

3.9.4 Utambuzi na Uhalali wa Vyeti na Mabadiliko ya Mshahara:

Hali hiyo hiyo ya upendeleo inayopatikana katika Utumishi (Ajira) ya Shirika, inaonekana katika suala zima la kuthibitisha kipi ni cheti halali na kinastahiki kurekebishwa mshahara, kwa mtumishi ambae atakuwa amekipata baada ya kuhitimu mafunzo yake.

Kigezo kikubwa katika suala zima la utambuzi wa uhalali wa vyeti, ni wapi muhusika amekipata cheti hicho na si kwamba Cheti hicho kimetolewa na Chuo gani ambacho kinatambuliwa rasmi. Hilo limethibitishwa kutokana na baadhi ya madai ya wafanyakazi ambao wamefaulu masomo yao katika vyuo vinavyosimamiwa na Bodi moja, lakini wengine vyeti vyao vikatambuliwa vyengine visitambuliwe.

Ndg. Fatma Mzee Said kwa mfano, aliwasilisha cheti cha 'Advanced Diploma in Business Studies' ambapo mitihani yake inasimamiwa na Bodi ya ICM. Sambamba na cheti alichowalisilisha **Ndg. Mwawanu Ali Juma**, tofauti iliyopo ni kwamba Ndg. Fatma yeye mafunzo yake ameyafanyia katika kituo cha Zanzibar wakati Ndg. Mwawanu yeye alifanyia mafunzo hayo Uingereza. Kamati imeshindwa kutofautisha vyeti hivyo kwa sababu vyote vimetolewa na Chuo kimoja, tofauti yake ni maeneo tu ya wapi Chuo na Kituo ama Tawi la Chuo kilipo, lakini Shirika lilimuarifu Ndg. Fatma Mzee Ali kwamba yeye cheti chake eti hakitambuliwi na Idara ya Utumishi, Serikalini **(Kiambatanisho Nam.84),** wakati Ndg. Mwawanu Ali Juma, kama alivyotambuliwa na kupatiwa ufadhili wa masomo yake, vile vile cheti chake kimetambuliwa na Shirika, bila ya hata kupelekwa Idara ya Utumishi Serikalini (**Kiambatanisho Nam 85 Rejea pia Kiambatanisho Nam 81)**, kinachohusiana na barua Nam. ZECO/OPF/F.027 ya Tarehe 24/8/2011, kinahusika).

Wakati huo huo **Ndg. Faida Khamis Haji** ambae ni Karani sehemu ya Utawala, nae alijiendeleza kielimu kwa gharama zake katika ngazi ya Stashahada kwa mafunzo ya kwenye Chuo cha 'Institute of Commercial Management' na Chuo cha 'Cambridge International College' vyote vya Uingereza.

Aliwasilisha vyeti vyake vya kuhitimu masomo, kwa barua ya tarehe 30/10/2007 na kukumbushia tena Tarehe 15/4/2009 kwa lengo la kubadilishiwa mshahara wake, lakini hakupata majibu yoyote. Mfanyakazi huyu hakuchoka kukumbushia na ilipofika Tarehe 27/04/2012, alikumbushia tena kwa mara nyengine **(Kiambatanisho Nam 86)**, lakini jambo la kutia wasiwasi ni kwamba kwanini asipate majibu ama anastahiki au la. Na kwa maana hiyo alikuwa hatandewi haki si tu kwa sababu ya kuwa hajibiwi barua zake, lakini kama anastahiki basi muda unapita na haki zake zinapotea. Tunachothibitisha ni kwamba, hadi Kamati inapita kufanya kazi zake, Mfanyakazi huyu bado hajajibiwa maombi yake.

Katika hili la upendeleo, pamoja na yote hayo, Kamati inaendelea kufafanua kwamba, kwa kiasi kikubwa upendeleo huo ulikuwa unatekelezwa kwa baadhi tu ya watumishi, ambao huduma wanazopewa ni za aina ya kuonesha kwamba wao ni watumishi muhimu mno kuliko wengine (V I Ps Status). Kwa kuchukulia mfano wa mtumishi huyu huyu Ndg. Mwawanu Ali Juma, Mkuu wa Masjala namna ya maombi yake yalivyokuwa yakishughulikiwa, Kamati iliridhika kabisa kwamba alichokuwa akifanyiwa si chengine isipokuwa ni upendeleo usiokuwa na kificho.

Kwa mfano, alipewa dhamana ya kuwa Mkuu wa Masjala Tarehe 28/11/2006 lakini kwa muda wote huo alipopewa dhamana hiyo hakulalamika juu ya malipo ya mshahara anaolipwa kwamba haukuwa na tofauti kulingana na dhamana aliyopewa. Cha ajabu aliliandikia Shirika malalamiko hayo Tarehe 2 Februari, 2009 ya kudai mshahara wenye hadhi na dhamana aliyonayo, lakini pia na tofauti yote (Arears) kwa miaka miwili na miezi mitatu nayo pia alipwe. Shirika bila ya pingamizi yoyote Tarehe 16/02/2009 (ZECO/PE/M.154) lilikubali kumlipa kama alivyoomba **(Kiambatanisho Nam 87)**.

Kamati ilikuwa na maswali mengi ya kujiuliza, Je muda wote huo, yaani tokea mwaka 2006 hadi 2009, Shirika lilikuwa halijui kama Mfanyakazi huyu alikuwa na

haki hiyo? Na jee, yeye mwenyewe Ndg. Mwawanu, vile vile hakujua! Kwanini asilalamike mwanzo! Au miaka hiyo na muda tolionao sasa kulikuwa na tafauti ya Uongozi ambao ama aliogopa kwamba hata angedai haki zake za kuongezewa mshahara, basi asingeliipata au si kwa kiwango cha huduma anazozitaka yeye!. Unataka kusema kwamba, katika hali yote hii hakuna upendeleo wa dhahiri? Naamini utakubaliana na Kamati, ingawaje bado utakuwa na maswali mengi, juu ya Ukaribu ama uhusiano wa Mfanyakazi huyu kwa Meneja Mkuu wa Shirika, na tafauti iliyopo ya wafanyakazi wengine waliobakia! Ni kitendawili kinotaka uteguzi.

Kwa upande wa Kamati, ilipata wasiwasi huu kutokana na mtiririko wa huduma alizozipata Ndg. Mwawanu Ali Juma, kwamba si tu kwa sababu alikuwa mtendaji wa Shirika sawa na watendaji wengine, ni dhahir kwamba kulikuwa na sifa ya ziada aliyokuwa nayo; ambayo hiyo ni siri kati yake na muajiri wake, tafsiri kwa hili kila mmoja na yake. Mtiririko wa huduma hizo ni kama ifuatavyo :-

- Tarehe 16/2/2009 Ndg. Mwawanu Ali Juma aliomba ruhusa ya kwenda kusoma kwa kulipiwa gharama hizo na familia yake.
- Tarehe 17/2/2009 (mapema sana, sawa na siku moja tu baada ya maombi yake) alipata jibu la ruhusa hiyo kukubaliwa bila ya pingamizi yoyote.
- Tarehe 18/2/2009 Shirika lilimuombea Visa kwa Ubalozi wa Kiingereza, Nchini Tanzania na kuthibitisha kwamba Shirika lenyewe ndio mfadhili wa mafunzo hayo (kwa asilimia mia moja).
- Tarehe 19/02/2009 Shirika liliakhirisha likizo la Ndg. Mwawanu Ali Juma arudi kazini kwa ajili ya eti kushughulikia kazi kwani Kamati ya P.A.C ya Baraza la Wawakilishi itakuwa kwenye Shirika la Umeme. **(Kiambatanisho Nam 88)**
- Tarehe 19/2/2009 Shirika lilimjazia fomu ya matumizi ya fedha za kigeni kwa ajili ya safari za nje.

Ukiachilia mbali ule utata ulioelezwa mwanzo juu ya tofauti ya vyeti na mafunzo aliyoomba na suala zima la kulipiwa gharama za masomo yake lakini pia namna maombi yake yanavyoshughulikiwa; ni kwa haraka mno lakini pia ni kwa kadri anavyotaka yeye kwa asilimia mia moja. Hakuwa akipata kipingamizi chochote, iwe analoomba limo ndani ya utaratibu na sheria au hata liwe nje ya utaratibu na

sheria basi majibu yake ni sawa tu *(Positive).* Hii imeonesha tofauti kubwa iliyopo kati yake yeye na watumishi wenzake.

Kamati hii inaamini kama Taasisi zote za Serikali zingelikuwa zinashughulikia maombi ya watumishi wake na wananchi kwa ujumla kwa kipindi kifupi tu, kama Shirika lilivyojikita kuyashughulikia ya Ndg. Mwawanu, basi Zanzibar hii ingelikuwa mbali sana kimaendeleo. Hata hivyo, kila mtu atajiuliza masuala mengi ambayo yanapata majibu tafauti, juu ya utukufu wa Ndg. Mwawanu na utumishi uliotukuka wa Meneja Mkuu kwa Mfanyakazi huyu, wakati wafanyakazi wengine ambao ni sawa na Mfanyakazi huyu kwa misingi ya Utumishi ya Shirika, wakisota na kuendelea kulalama chini kwa chini, huku wakiamini kupitia Ripoti hii, Serikali italishughulikia suala hili ipasavyo, kwa maslahi ya kuboresha shughuli za Umma.

3.10.0 Muhtasari wa Mambo yaliyobainika na Kamati kufuatia Uchunguzi wake wa Hadidu hii Rejea:

i. Uajiri wa Wafanyakazi hawa haukufuata taratibu za Uajiri kama zilivyoelezwa katika Sheria na Kanuni za Utumumishi za Shirika.

ii. Maombi ya Ajira ya Wafanyakazi wengi kwa Upande wa Pemba yameombwa kwa Meneja wa Tawi, Pemba, kitendo ambacho kinakiuka taratibu za Kanuni za Utumishi, za Shirika.

iii. Kamati haikupatiwa sifa zilizohitajika na Shirika wakati wa kutangazwa nafasi hizi, na ni sawa pia kusema kwamba, haijapatiwa Ripoti inayoonesha utaratibu mzima uliotumika tokea kufanya uteuzi wa baadhi ya wananchi walioomba (Short List), Usaili, na matokeo ya Usaili huo, kwa kipindi cha mwaka 2008 hadi 2010, na badala yake taratibu hizo zilifuatwa kwa mwaka 2011 Pekee.

iv. Kuanzia mwaka wa 2008 hadi 2009, Wafanyakazi waliajiriwa bila ya kufanyiwa Uhakiki wa Kiusalama (Security Vetting) na Mamlaka inayohusika na suala hili (G.S.O).

v. Tume ya Utumishi Serikalini haikufanya ipasavyo katika uchunguzi wa malalamiko ya wananchi watatu kuhusiana na nafasi ya ‘Cashier’ kwa mwaka wa ajira 2011.

vi. Kuna upendeleo mkubwa sana katika upatikanaji wa fursa za kusoma na kudhaminiwa na Shirika, pamoja na ubadilishwaji wa mshahara kwa muamala wa elimu husika dhidi ya wafanyakazi wa Shirika hili.

HADIDU REJEA NAM. 4

IWAPO MALI ZA SHIRIKA ZINAUZWA KWA KUFUATA TARATIBU ZA SHERIA YA UUZWAJI NA UGAVI WA MALI ZA SERIKALI NA SHERIA NYENGINE ZINAZOHUSIKA.

4.0.0 Ufafanuzi wa Hadidu Rejea :

Ni jambo lisilo na shaka yoyote juu ya Muongozo wa kuuza mali za Taasisi yoyote ya Serikali, ikiwa ni pamoja na Shirika la Umeme la Zanzibar, kwa kufuata masharti yaliyoelekezwa na Sheria ya Ununuzi na Uuzaji (Ugavi) wa Mali za Serikali, Namba 9 ya mwaka 2005. Katika kufahamu hili, Kamati ikiongozwa na Sheria husika, ilikutana na Uongozi wa Shirika pamoja na kufanya ziara kadhaa katika mali za Shirika, kwa malengo ya kuona, namna gani Shirika hili linauza mali zake.

Katika hadidu hii rejea, Kamati imetakiwa kuchunguza namna gani Shirika linauza mali zake kwa kufuata masharti yaliyowekwa na Sheria hii Namba, 9 ya mwaka 2005, pamoja na Sheria nyengine zinazohusika. Suala hili linahitaji kufahamika kwa makini kwa sababu, pamoja na muda uliokabidhiwa Kamati, na mali nyingi za Shirika, kama Kamati ingelifanyia kazi kwa kuchunguza mali zote zinazomilikiwa na Shirika, (huku ikifahamika hata nguzo na mita zote za wateja wake ni mali za Shirika, pamoja na kwamba zinanunuliwa na wateja wenyewe wakati wanapohitaji huduma ya kuungiwa umeme), ingelitosha kupewa angalau miaka miwili au zaidi, na Kamati ingelazimika pia kufanya kazi bila ya kupumzika. Hata hivyo, kama tutakavyoona hapo baadae, Kamati imejiridhisha kuifanyia kazi hoja hii, kwa kupata mfano tu wa mali hizo.

4.1.0 Utaratibu wa Uuzwaji wa Mali za Shirika kwa mujibu wa Sheria inayohusika :

Aidha, Katika kuhakikisha kwamba hoja hii inajibika kwa ufanisi, ni vyema kwanza kuiangalia Sheria husika inaelekezaje. Miongozo yake ndio itakaonesha ukamilikaji wa zoezi hilo. Katika kuutekeleza utaratibu huo, ni vyema ikaeleweka njia za Uuzaji wa Mali za Taasisi ya Serikali, ambazo kimsingi zimeainishwa na kifungu cha 40(1) cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2005, ambapo ufafanuzi wake wa kina wa taratibu zipi zingelifuatwa, umefafanuliwa na kanuni ya 175 ya Kanuni

za Sheria hii. Ni vyema sasa tukafahamu njia za kutumiwa na Shirika la Umeme, wakati imeamua kuuza mali zake kama ifuatavyo :

Kwa mujibu wa kifungu cha 40(1)(a) cha Sheria hii, Namba 9 ya mwaka 2005, Shirika lingeliweza kuuza mali zake kupitia njia ya Mnada wa hadhara, ambapo mali husika ya Shirika, ambapo gharama halisi ya mali hiyo ama hizo, haitazidi kiwango kilichofanyiwa tathmini ya kitaalamu na kuelezwa katika muongozo wa tathmini hiyo.

Shirika pia linaweza kuuza mali zake kupitia mapatano ya moja kwa moja, pale ambapo mauzo hayo katika soko lililo wazi, litahusisha masuala ya haki za binaadamu na thamani halisi ya bidhaa hiyo haipungui ile iliyowekwa katika thatmini ya kitaalamu kama ilivyofanywa.

Kuiharibu mali hiyo, nayo ni njia moja wapo ya Ugavi wa Mali za Shirika, ingawa hii kwa mujibu wa Sheria hiyo, hukubalika kuwa ni sawa na kuuza ama kwa lugha nyengine, kuhaulisha mali husika. Njia hii itatumika pale ambapo mali hiyo imeshapoteza thamani yake na wala haina maslahi ya umma wala haina athari ya kiusalama.

Aidha, Kifungu hiki cha 40(1)(d) pia kimeeleza njia ya kuiuza mali husika kama mali kachara au kuibadili na kuwa na hadhi hiyo. Huku pia njia ya kuiuza mali husika, ikiwa ni njia moja ya hizo zinazokubaliwa kufuatwa wakati wa uuzaji wa mali za Shirika. Kama pia ilivyokubalika kukihaulisha ama kuipeleka mali hiyo kwa chombo chengine cha Shirika chenye mamlaka yanayohusiana na mali za Shirika, kama njia hii inavyokubaliana na maelekezo ya kifungu cha 40(1)(f) cha Sheria hiyo.

4.2.0 Utaratibu wa kufuatwa kwa ajili ya Uuzaji wa Mali za Shirika:

Kanuni ya 175 ya Kanuni za Sheria ya Manunuzi na Ugavi wa Mali za Serikali ya mwaka 2005, inaweka utaratibu wa kufuatwa pale ambapo Taasisi yoyote ya Serikali, ikiwa ni pamoja na Shirika la Umeme, imeamua kuuza ama kuharibu ama kwa kutumia njia yoyote kati ya hizo tulizozieleza hapo juu, kwa ile lugha maarufu ya Ugavi wa mali hizo. Katika kuona mali za Shirika zinauzwa inavyostahiki

kisheria, taratibu zifuatazo zilitarajiwa kufuatwa kama Kanuni za Sheria Namba 9 ya mwaka 2005, zinavyoelekeza:

Kuwepo haja ya kuuzwa kupitia Kitengo cha Watumiaji (User Departments):
Hatua ya mwanzo kabisa ni kwa mtumiaji (User Department) kuthibitisha kwamba kifaa kilichopo hakifai kwa matumizi. Kanuni hiyo ya 175, inasomeka kama ifuatavyo:

> "The Procurement Management Units will receive the list of items recommended by the Board to be disposed off from the user department"

Ikimaanisha, Kitengo cha Watumiaji, ndio cha kwanza chenye jukumu la kuhakikisha kwamba, kifaa kilichopo hakifai kwa matumizi na kinahitajika kiondolewe ikiwa ni pamoja na kuuzwa. Na Uondoaji huo utafanywa kwa kuiandikia Bodi ya Zabuni na kutoa ufafanuzi wa kina kuhusiana na kutofaa kwa vifaa hivyo na huku ikisisitiza haja ya kuuzwa kwake. Baadae, Bodi ya Zabuni itakaa kujiridhisha juu ya vifaa hivyo vilivyoshauriwa kuuzwa, ambapo nayo ikiridhika, basi itatoa idadi halisi ya vifaa vinavyostahiki kuuzwa na njia moja wapo inayofaa kuuzwa kwake kwa kuviwasilisha kwa Kitengo cha Manunuzi (Procurement Management Units).

Aidha, Kitengo hiki cha Manunuzi kitalazimika kuwasilisha idadi ya vifaa ama mali zinazohitaji kuondolewa, ikiwa ni pamoja na kuuzwa kwa Meneja Mkuu wa Shirika, ambae atathibitisha njia ya kutumika ya kuuzwa kwake, na hatimae mali ama vifaa hivyo vitauzwa.

4.3.0 Hali Halisi ya Uuzwaji wa Vifaa Vichakavu vya Shirika, katika Tawi la Pemba:

Kuhusiana na viifaa chakavu vilichopo kwenye Tawi la Pemba, ilistahiki kwa Kitengo cha Watumiaji husika, kufuata taratibu tulizokwishazieleza hapo juu, ili ziweze kuuzwa kwa misingi ya sheria. Na kutokana na ukweli kwamba, Shirika la Umeme Tawi la Pemba, lilikuwa linahitaji kuvihaulisha baadhi ya vifaa vyake ambavyo kwa wakati huo vilikuwa havihitajiki tena kwa matumizi ya Shirika. Katika kutimiza azma hiyo liliandaa mazingira ya uuzwaji wa vifaa hivyo.

4.3.1 Kilichobainika na Kamati

Barua ya tarehe 12/12/2010 yenye kumbu kumbu namba ZECO/8/8/VOL 1/133 ambayo katika ripoti hii ni **Kiambatanisho Nam 89**, inahusiana na ruhusa iliyoombwa na Meneja Mkuu kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kuruhusiwa Shirika lake kuuza vifaa chakavu, baada ya kukiri katika barua hiyo kwamba tayari walikwishapata idhini ya Bodi ya Zabuni ya Wakurugenzi. Pamoja na hatua hii, suala hili kwa Kamati linahitaji kwanza kuthibitishwa iwapo kweli Bodi ya Zabuni ilikaa na kuridhia, lakini je hapo kabla, kuna kikao chochote cha Kitengo cha Manunuzi kilichokaa kupitia orodha ya mahitaji ya kuuzwa kwa vifaa hivyo kutoka Kitengo cha Watumiaji? Masuala haya hayajithibitishwa uhalali wake mbele ya Kamati.

Hata hivyo, kufuatia barua hiyo tuliyoinukuu hapo juu, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo aliruhusu uuzwaji wa vifaa chakavu, kupitia barua yake ya tarehe 17/1/2011 yenye kumbu kumbu namba MFEA/M.30/4/02/VOL.VII/ ambayo katika ripoti hii ni **Kiambatanisho Nam 90**, ingawaje bado kuna suala la msingi la kujiuliza! Kwamba, katika barua ya kuomba ruhusa ya kuuzwa vifaaa hivyo ambayo tumeifanya Kiambatanisho Nam. 83 cha ripoti hii, miongoni mwa vifaa vilivyotakiwa kutolewa ruhusa na kuja kufanyiwa tathmini na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ni Gari Land Rover yenye namba SLS 1023 na Toyota Pick Up yenye Namba SLS 1045.

Jambo la kushangaza, katika ruhusa iliyotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ajili pia ya kutiwa thamani, gari zote mbili hizo ambazo ndio mada kuu yetu hapa, hazikutolewa tathmini na ni sawa pia kwamba hazikupata idhini ya wamiliki wakuu wa mali za Serikali, Zanzibar. Sasa unaweza kuendelea kujiuliza, gari hizi zimeuzwa kwa utaratibu upi na thamani halisi ni ipi na imetolewa na mamlaka ipi? Masuala yote haya pamoja na kukosekana jawabu zake, ni dhahiri kwamba uuzwaji wake haukufuata matakwa ya sheria zinazohusika wala taratibu za kiutawala.

Basi na tuendelee kushangaa juu ya barua iliyoruhusu uuzwaji wa vifaa hivyo vichakavu kutoka kwa Meneja Mkuu wa Shirika, kwenda kwa Meneja wa Tawi Pemba. Barua yenye kumbu kumbu namba ZECO/MUMW/VOL.1/206

(Kiambatanisho Nam 91), inaagiza Meneja wa Tawi auze vifaa hivyo kwa njia ya mnada, kwa kile kilichofahamishwa kwamba, tayari uuzaji wake umeshapata idhini ya Bodi ya Wakurugenzi. Hapa tunapata shaka, kwamba ni nani alieuza vifaa hivyo, ni Meneja wa Tawi ama Kitengo cha Manunuzi cha Shirika? Iwapo tunahitaji majibu ya kisheria, basi kifungu cha 175(3) cha Kanuni za Sheria Namba 9 ya mwaka 2005, kinatosheleza kwa sababu kimeeleza uuzwaji wa mnada ufanywe na Kitengo cha Manunuzi kwa mujibu wa Kanuni hizo, lakini kwa kuwa Kamati imeelezwa kwamba uuzaji wake umefanywa na Uongozi wa Shirika, Tawi la Pemba, inatosheleza pia kuthibitisha kwamba, taratibu za uuzaji huo hazikuridhiwa na Sheria zinazohusika.

Lakini pia ni vyema kufahamu kwamba, Barua hiyo ilipokelewa Afisi ya Tawi, Pemba kutoka Unguja ni ya Tarehe 17/12/2011, siku hiyo ya Jumamosi, ambapo kwa Kawaida Shirika halifanyi kazi na zaidi za Kiutawala. Sasa tuseme kwamba ni kweli barua hiyo inakubaliwa katika taratibu za kiutawala? La kushangaza zaidi ni kwamba, imepokelewa siku hiyo hiyo Jumamosi na wala haikutumwa kwa njia ya Fax au Email, sasa ni kweli kwamba iliandikwa ama imefuata baada ya kukamilika kwa njia na taratibu zote za uuzaji. Basi mambo ndio yaliendelea hivyo, na baada ya kupokelewa barua hiyo Pemba, Meneja wa Tawi alimuandikia Dokezo Afisa Utawala kwa hatua ya usimamizi, wakati Afisa huyo wa Utawala alimwandikia Dokezo Afisa Uagiziaji kwa hatua za mnada siku ya Jumapili ya Tarehe 18/12/2011. Mnada wenyewe nao ulikuwa siku hiyo hiyo ya Jumapili, ni vitu vya kutia shaka sana.

Aidha Barua hiyo ya kuruhusu iliyotoka kwa Meneja Mkuu wa Shirika zaidi ya kueleza juu ya idhini ya Bodi na kusisitiza kufuatwa kwa taratibu za mnada ili kuondosha malalamiko, hakukuwa na maelezo mengine ambayo ni ya msingi ya kuonesha Orodha halisi ya vifaa ambavyo vinahitajika kufanyiwa mnada huo na wala hakukuwa na marejeo ya Barua nyengine yoyote yenye kuonesha kupatikana kwa orodha hiyo.

Kwa maana hiyo kulikuwa na utata juu ya ruhusa hiyo ya Bodi ama ilikuwa haina orodha kamili ya vifaa vinavyohitajika kuuzwa, au kulikuwa na ongezeko la vifaa vyengine ambavyo havikuwemo katika orodha ya mwanzo na kwa hivyo kukosa

baraka ya ruhusa ya Bodi. Hilo lilidhihirika wazi kwani hata ile orodha aliyokuwa nayo Afisa Uagiziaji, ambae ndie aliyepewa jukumu la kusimamia mnada huo ilitafautiana na vifaa halisi vilivyopigwa mnada siku hiyo.

4.3.2 Orodha ya vifaa vilivyouzwa (Iliyopokelewa kutoka kwa Mkuu wa Utawala wa Tawi la ZECO – Pemba)

1. Transformer 500KVA mbili (2)
2. Transformer 1500KVA moja (1)
3. Transformer 100KVA mbili (2)
4. Transformer Single Phase moja (1)
5. Transformer House mbili (2)
6. Gari SLS 1045 moja (1)
7. Gari SLS 1023 moja (1)
8. Propeller Shafts nne (4)
9. Starter House moja (1)
10. Mapande ya vyuma mchanganyiko

4.3.3 Ripoti ya Mnada wa Kuuza Vifaa Chakavu Uliofanyika Tarehe 18/12/2011

Afisa Uagiziaji ambae ndie alieachiwa kusimamia uuzwaji wa vifaa hivyo kwa upande wa Shirika, akishirikiana na madalali mmoja kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo (Afisi ya Unguja) na mwengine kutoka Wizara hiyo hiyo Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo (Afisi ya Pemba), aliviainisha vifaa vilivyouzwa siku hiyo ya Tarehe 18/12/2011 kwa Taarifa aliyoiandika Tarehe 27/12/2011 ni kama ifuatavyo :-

(1) Gari Defender SLS 1025, ameuziwa Ndg. Shaibu Hassan Kaduara, (Mfanyakazi wa Shirika la Umeme, Tawi la Pemba) kwa thamani ya Tsh. 3,550,000/- na kwa tarehe hiyo, alikuwa tayari ameshalipa jumla ya Tsh. 2,550,000/-.

(2) Gari Toyota Hilux, aliuziwa tena Mfanyakazi huyu huyu wa Shirika Tawi la Pemba, Ndg. Shaibu Hassan Kaduara kwa thamani ya Tsh.2,250,00/- na kwa tarehe hiyo alikuwa tayari ameshalipa jumla ya Tsh.1,850,000/-.

(3) Makachara ya Transformer ameuziwa Ndg. Ali Makame Issa kwa thamani ya Tsh. 2,020,000/- na kwa Tarehe hiyo alikuwa tayari ameshalipa Tsh. 505,000/-.

JUMLA YA MAUZO YOTE YALIKUWA NI TSH. 7,820,000/-
Toa 10% ya Kamisheni ya Dalali zinabaki Tsh. 7,038,000/-. Kilicholipwa ni Tsh. 1,905,000/- ukitoa cha Dalali ambacho ni Tsh. 782,000/- zitabaki Tsh. 1,123,000/-. **(Kiambatanisho Nam 92).**

Pamoja na orodha hiyo kuelezwa hapo juu, vifaa vilivyouzwa havihusiani na vile vilivyoombewa ruhusa na idhini kama tulivyokwisha eleza hapo kabla, na ndio maana Kamati ikawa na wasi wasi sana juu ya Meneja Mkuu wa Shirika kuagiza kwa Meneja wa Tawi juu ya kuuzwa kwa vifaa kachara bila ya kuviainisha vifaa gani. Lakini kama haitoshi, kwa nini Kamati isipatiwe utaratibu uliokamilika wa kuuzwa kwa vifaa hivi, na badala yake kupewa taarifa vipande vipande.

4.3.4 Mchanganuo zaidi

Taarifa ya Afisa Utawala imeonesha kwamba, miongoni mwa vifaa vilivyouzwa ilikuwa ni mauzo ya jumla ya Transformer sita (6), wakati taarifa ya aliyesimamia mnada huo (Afisa Uagiziaji) mchanganuo wake unaonesha kwamba Transformer zilizopigwa mnada siku hiyo, tena zilikuwa ni makachara ambayo ni ya Transformer ya KVA 500 (mbili), KVA 100 (moja) na ya KVA 50 (moja) jumla yake ni Transformer nne (4). Aidha Transformer House na Transformer Single Phase nazo zilikuwemo kwenye mnada huo. Lakini Transformer ya 1500KVA moja haimo kwenye orodha wa vifaa vilivyopigwa mnada aliyonayo Afisa Uagiziaji na wala hana taarifa nayo. Lakini alikiri kwamba Transformer hiyo iliondolewa katika eneo ilipokuwepo.

Vifaa vyenginevyo ambavyo havikuwemo kwenye orodha hiyo ni ‘Propeller shafts’ nne, ‘Starter House’ moja na Mapande ya machuma mchanganyiko. Ingawa mauzo ya mapande ya vyuma tu ndiyo Afisa huyo aliyashuhudia baada ya kupata maelekezo baadae wakati mnada wa awali umeshamalizika. Hata hivyo Transformer hiyo haipo kwenye nafasi yake.

Pamoja na yote hayo Kamati haikuweza kuiona Barua inayoonesha kwamba Tawi la Shirika Pemba lilikuwa linahitaji kuuzwa kwa vifaa hivyo. Na badala yake, imekuwa kama Shirika Makao Makuu, ndilo lenye nia hiyo na Tawi la Pemba kazi yake ni kutekeleza tu. Jengine ni kwamba Bodi ya Zabuni ya Shirika haikushirikishwa kwenye mchakato huo jambo ambalo ni kinyume na Sheria. Kamati haikuarifiwa juu ya hata kuwepo kwa Bodi hiyo, licha ya kuhusishwa kwake.

Kutokana na utata huo Kamati imeamini kabisa kulikuwa na kutokufatwa kwa taratibu za kisheria katika mauzo hayo, jambo ambalo limesababisha ubabaishaji wa kutokufahamika hata vifaa halisi vilivyouzwa na hatimae 'Transformer' moja kupotezwa katika mazingira hayo tatanishi.

4.4.0 Mambo mengine Yanayohusiana :

4.4.1 Matumizi ya Mali za Shirika : *Taarifa ya kupinduka kwa Gari la Shirika la Umeme SLS 1111 :*

Pamoja na kwamba, hoja hii inahusiana na namna ya namna ya Uuzaji wa mali za Shirika, na kwa kuwa Kamati imepewa dhima ya kuchunguza juu ya suala hili, lakini pia miongoni mwa sababu za kuwepo kwake, imeona ni vyema pia ikaangalia kwa namna gani mali za Shirika zinatumika, huku zikipelekea kuharibika na kuwa ni sehemu ya mauzo ya mali hizo. Ni uzoefu wa kawaida kwa Kamati hii kufuatilia mali za Serikali, utunzaji na matumizi yake, katika kazi zake za kawaida, na Wajumbe wake wanafahamu fika kwamba, katika maeneo ambayo Kamati hii hutoa ripoti yake kwa msisitizo mkubwa, ni pamoja na kukiukwa kwa taratibu za uuzaji na ununuzi wa mali za Serikali.

Aidha, pia Kamati inafahamu kwamba, miongoni mwa tatizo kubwa la uuzaji wa mali za Serikali, ni pamoja na kuwepo kwa baadhi ya watendaji wasio na uaminifu, ambao kwa makusudi huhujumu mali za Taasisi zao, kwa malengo ya kuzifanya zionekane zimeharibika na hatimae kupata nafasi ya kujiuzia bila ya kufuata taratibu zilizopo. Kwa Mfano, Kamati inafahamu kwamba, kuna baadhi ya watendaji wasio waaminifu, wanaoziharibu kwa makusudi gari za taasisi zao, ili

zishindwe kufanya kazi kwa muda mfupi, lakini inapotokezea zimelala na kutofanya kazi kwa muda mrefu, inakuwa ni hoja nzuri ya kuuzwa kwake.

Kwa kuzingatia hali hii, na kwa kuwa Shirika nalo ni sehemu ya Taasisi ya Serikali, Kamati imeona ni vyema kuangalia namna ya mali zake zinavyotumika, kwa maslahi ya hoja ya Uuzwaji wa mali za Shirika ama upotevu wa fedha na utumiaji mbaya wa nafasi za baadhi ya watendaji wa Shirika hili. Kwa hali hiyo, ni vyema tukapata ufafanuzi wa namna ya gari hii SLS 1111, ilivyopinduka na hatimae kutofaa tena kwa matumizi ya Ofisi. Je kuna hatua zozote zilizochukuliwa na kama hazipo, nini hatma ya gari hiyo ?

Basi na tuanze kupata maelezo haya kwamba, miongoni mwa magari ya Shirika la Umeme ni Fuso lenye nambari za usajili SLS 1111. Gari hilo lilikuwa likitumika kwa ajili ya kubebea wafanyakazi (mafundi) wanapoenda kazini (field), hasa nje ya mji au wakati mwengine hutumika kwa ajili ya kubebea nguzo za umeme pamoja na vifaa mbali mbali.

Katika safari zake za kikazi siku ya Jumanne ya Tarehe 17 Mei, 2011 ambapo gari hiyo ilipangiwa kuwapeleka wafanyakazi pamoja na vifaa kwa ajili ya kazi ya kujenga line ya Umeme huko Nungwi na ikiwa safarini huku ikiwa na wafanyakazi kumi na vifaa vyao pamoja na nguzo nne za umeme ilipata ajali na kupinduka. Pamoja na kwamba wafanyakazi walipata majaraha madogo lakini gari iliharibika vibaya kiasi cha kwamba halikufaa kabisa kwa matumizi ya Shirika.

4.4.2 Suala la kutafuta gari nyengine

Kutokana na kuendelea kuwepo kwa kazi, Shirika lililazimika kukodi gari kwa madhumuni hayo. Kwa maana hiyo, Shirika lilichukua hatua ya kufanya mkataba na gari la mtu binafsi Ndg. Said Khalfan Said wa Maungani, Zanzibar.

Afisa Usafiri (TO) wa Shirika, Ndg. Ali Ramadhan Chum alimwandikia barua Meneja Mkuu wa Shirika juu ya ombi la kukodi Gari ili iweze kufanya kazi badala ile iliyoharibika kutokana na ajali. Barua hiyo iliandikwa Tarehe 13/06/2011 yenye Nam. ZECO/OM/VOLL.II/2011/784. Wakati mkataba uliofungwa baina ya mkodishaji (mmiliki) na Mkodishwaji (Mteja) ulifungwa Tarehe 9 Juni, 2011.

Kutokana na hali hii, Kamati ilianza kupata mashaka na hilo, inakuwaje barua ya maombi ije mwisho (Tarehe 13/6/2004) na mkataba ndio uje mwanzo (Tarehe 9/4/2011).

Shirika lilikodi gari hilo lenye nambari ya usajili Z 185 BE (Canter 3Tons) kwa bei ya Shilingi laki moja na Hamsini elfu kwa siku. Ambapo mmiliki wa gari atamlipa mwenyewe dereva na atalijaza mafuta gari lake hilo, wakati kazi itakuwa kuanzia saa 1 :30 asubuhi hadi saa 12 :30 jioni kwa siku za Jumatatu hadi Ijumaa. Mkataba huo ni wa mwezi mmoja na umekuwa ukiongezwa kila inapomalizika hadi hapo haja itakapokwisha au vyenginevyo vyovyote.

Mkataba huo ulirejewa tena na tena na barua ya maombi ya tarehe 21/2/2012 ndio ambayo Kamati iliyoiona. Kutokana na kwamba kwa mwezi mmoja gari hilo linafanya kazi kwa muda wa siku ishirini ukitoa zile siku za mapumziko kwa jumla ya malipo ya shilingi Milioni tatu (3, 000,000/) ndio yanayohitajika na hivyo kwa kipindi cha miezi tisa (kutoka Juni, 2011 hadi Februari, 2012) jumla ya malipo yote yaliyolipwa hayapungui Shilingi Milioni Ishirini na Saba (Tshs 27,000,000/-) fedha ambazo zinaweza kabisa kununua gari nyengine. Hii inategemea idadi ya siku za mapumziko zilivyo kwa mwezi husika.

Hata hivyo Kamati ilipomhoji mmiliki wa gari hilo Ndg. Said Khalfan juu ya mwenendo mzima wa shughuli zake kwa mujibu wa Mkataba alikiri kwamba kwa upande wake hakukuwa na matatizo yoyote na kukiri kwamba wakati mwengine Shirika kupitia kituo chake cha Petroli huwa linamtilia mafuta na kama kumkopesha na baadae wakati wa malipo linamkata fedha zake hizo. Kamati haikuridhika na hilo kwa sababu ni kinyume na mkataba kwa mujibu wa kifungu cha 6(6) ambacho kinasomeka :-

> ***'Kuhakikisha kuwa gari imejaa mafuta kila inapowasilishwa kwa MTEJA kwa ajili ya kazi'.***

Lakini sababu ya pili hii itakuwa na sura nyengine endapo gari la binafsi linaweka mafuta wakati kila mmoja anajua kwamba mafuta ni jukumu lake na pale hapauzwi mafuta hivyo suala linakuja hata kama anakatwa fedha za mafuta kupitia

malipo yake, jee fedha hizo zinaenda wapi!. Wakati hesabu yake tayari imetoka kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa matumizi ya magari ya Shirika.

Katika kadhia hii ya ukodishwaji wa gari Kamati imehisi kwamba huo ni ubadhirifu wa fedha usio na sababu, kwani Shirika lenyewe lina uwezo wa kununua gari itakayoweza kufanya kazi.

Kwa ujumla, Kamati inaendelea kusisitiza kwamba, Shirika hili lina kila uwezo wa kumiliki gari zake wenyewe bila ya kulazimika kukodi, iwapo gari hizo na mali nyengine zitasimamiwa ipasavyo kwa maslahi ya Shirika.

4.4.0 Muhtasari wa Mambo yaliyobainika na Kamati kufuatia Uchunguzi wake wa Hadidu hii Rejea:

i. Shirika linauza mali zake bila ya kufuata utaratibu ulioelezwa na Sheria Namba 9 ya mwaka 2005 na Sheria nyengine zinazohusika.
ii. Baadhi ya wafanyakazi wa Shirika ambao wamepewa dhima ya Udereva, hawajali thamani halisi ya Gari za Shirika na matokeo yake hupelekea ajali za mara kwa mara dhidi ya gari za Shirika.
iii. Shirika linaingia hasara zisizo za lazima kwa kukodi magari kwa lengo la kutekeleza majukumu ya Shirika huku magari ya Shirika yakitumia bila ya uangalifu na hatimae hupata ajali zisizo za lazima.

HADIDU REJEA YA TANO:

IWAPO UPATIKANAJI WA MAJENERETA 32 YALIOPO MTONI ULIFUATA SHERIA ZINAZOHUSIKA NA KWA NINI HAYATUMIWI KWA MANUFAA YA WANANCHI WA ZANZIBAR.

5.0.0 Ufafanuzi wa Hadidu Rejea :

Kamati ilitakiwa kufuatilia na kujiridhisha kuhusu upatikanaji wa majenereta 32 yaliyokuwepo Mtoni kama ulifuata Sheria zinazohusika na kama hayatumiwi kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar. Kwa ufupi, Kamati ilifuatilia hoja hii kwa siku tatu zinazohusisha mjadala wa pamoja na Shirika, kufanya ukaguzi wa majenereta hayo katika eneo la Mtoni na kupata ufafanuzi unaohusiana na hoja hii, pamoja na kukutana na Kampuni iliyopewa kazi ya kuleta na kuyafunga iitwayo, Mantrac Tanzania Ltd iliyopo Dar es Salaam, Tanzania.

Unapofanya marejeo ya hoja hii, kuna vitu viwili vinahitaji kuangaliwa kwa karibu mmno, suala la kwanza ni taratibu zilizotumika hadi kupatikana kwa majenereta hayo, hii ina maanisha pamoja na taratibu za manunuzi zilizoelezwa kwa ufasaha katika Sheria ya Manunuzi na Ugavi wa Mali za Serikali, Namba 9 ya mwaka 2005 pamoja na Kanuni zake, na sehemu iliyobakia ni Kamati kujiridhisha iwapo majenereta hayo yanatumiwa ama hayatumiwi kwa matumizi yaliyokusudiwa. Na kwa hali hiyo, ufafanuzi wa hoja hii utahusiana zaidi kuangalia maeneo hayo mawili makuu. Ili kupata usahihi wa ufafanuzi wake, ni vyema tukafuata maelekezo yafuatayo:

5.1.0 Utata wa Ufafanuzi wa Fedha za Kunulia Majenereta 32:

Katika kuhoji juu ya haja na sababu ya upatikanaji wa majenereta 32 yaliyopo Mtoni, ambapo Kamati imepewa kazi ya kuyafuatilia, ni kuwepo kwa utata mkubwa juu ya usahihi wake, huku kukiwa na kauli tofauti kutoka kwa Uongozi wa Shirika na kauli za Serikali, ikiwa ni pamoja na Wizara inayolisimamia Shirika hili kwa ujumla. Kuna kauli kwamba, Majenereta hayo yamenunuliwa kwa fedha za Mradi wa MDRI, kwamba ni fedha zinazotokana na msamaha wa Madeni, ambapo Tanzania hunufaika, lakini na Zanzibar nayo hunufaika kwa upande wake. Kwa lugha hii, unapohitaji kufahamu juu ya taratibu zilizotumika kununuliwa kwa majenereta hayo, unalazimika pia kufahamu taratibu za matumizi ya fedha hizo za

Msamaha wa Madeni. Ikiwa ni pamoja na utaratibu wa matumizi ya fedha za MDRI kutokabidhiwa kwa taasisi inayopatiwa fedha, kwa maana hii Shirika la Umeme, lakini hupatiwa bidhaa/huduma ilizohitaji, yaani Majenereta 32 na malipo hufanywa moja kwa moja na IMF Kupitia Benki Kuu ya Tanzania.

Kauli hii pia imetofautiana na ufafanuzi uliopewa Kamati hapo awali, kwamba, fedha za kununulia majenereta hayo, zinatokana na Ufadhili uliofadhiliwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, juu ya haja ya kujinasua na hali tete ya kukosa umeme kwa kipindi chote cha miezi mitatu. Kwa ufahamu huu, unapotaka kuhoji juu ya taratibu za manunuzi ya Majenereta hayo na matumizi ya fedha hizo, jawabu inakuwa ni nyepesi tu, kwamba maelekezo ya Wafadhili ndio yaliyofuatwa zaidi kuliko hata taratibu nyengine, kwa maana, Wafadhili wana taratibu zao na Sheria zao za Fedha na matumizi ya fedha hizo, kwa Kawaida hufahamu wao wenyewe, kwani Shirika lilipewa tu majenereta hayo bila ya wao kuhusika na ununuzi wake.

Aidha, pia kuna kauli kwamba, Serikali kweli ilipewa msaada na Wafadhili, lakini msaada huo ulikuwa wa fedha, na tokea awali fedha hizo zilikabidhiwa kwa Serikali, na ikabakia dhima ya kuyanunua Majenereta hayo. Katika hali hii, kwanza fedha hizi huwa ni za Serikali kama fedha nyengine za Msaada, na hakuna sababu yoyote ya kuzitumia, bila ya kufuata taratibu za Sheria za Fedha za Umma. Na hivyo basi, kama taratibu za Sheria ya Manunuzi na Ugavi wa Mali za Serikali, Namba 9 ya mwaka 2005 na Sheria za Fedha zingelifuatwa ipasavyo, basi Shirika lingelinunua Majenereta linaloona yanafaa kwa matumizi yao, huku Wafadhili wakitaka tu waone umeme umepatikana na wajisikie wametoa mchango wao wa kuisaidia Serikali na nchi ya Zanzibar kwa ujumla.

5.2.0 Haja ya kupatikana kwa Majenereta 32:

Miongoni mwa mambo ya msingi kufahamika kuhusiana na hoja hii, ni pamoja na kufahamu haja ya kupatikana majenereta 32 yaliyopo Mtoni. Yaani, ni kujiridhisha juu ya umuhimu wa kupatikana kwake, lakini pia ni sababu zipi zilizopelekea kuwepo na presha na ulazima wa kununuliwa. Hata hivyo, jawabu ya suala hili zilitegemea sana tofauti ya majibu, kama tofauti hiyo ilivyopatikana juu ya fedha za kununuliwa kwake. Kamati ilipohoji suala hili, ilielezwa kuwa, majenereta hayo yamenunuliwa kutokana na kuzimika kwa umeme nchi nzima (Unguja) kwa muda

wa miezi mitatu, kuanzia Disemba 2009 hadi Machi 2010 katika wakati huu, Serikali ilihitaji kupatikana kwa umeme wa dharura, ili nchi iondoke katika giza. Baada ya Serika kushauriwa haja ya majenereta hayo, ndipo ilipotafuta Wahisani wa kusaidia kupatikana kwake.

Lakini kabla ya kwenda ndani kidogo kuhusiana na hoja hii, kuna suala jengine muhimu sana kujiuliza; nalo ni sababu zipi zilizopelekea kukosekana kwa umeme Unguja kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu mfululizo? Je, Serikali imetoa ripoti gani kuhusiana na tatizo hilo kubwa lililowakabili wananchi wa nchi hii na kukwaza shughuli mbali mbali za kiuchumi na kimaendeleo! Kwa ufupi, Kamati haikupata majibu ya kuridhisha kuhusiana na sababu zilizopelekea kukosekana kwa umeme kwa kipindi chote hicho, na imebakia kuwa na shaka kubwa ambayo haitaodoka mpaka pale itakapoundwa Tume huru ya Uchunguzi juu ya kadhia hii.

Kwa mfano, eti Kamati ilipokutana na Uongozi wa Shirika la Umeme na kuhoji suala hili, ilielezwa kwamba, kulikuwa na fundi aliekuwa anaezeka kibanda kilichopo katika eneo linalohusika na waya, na katika ujenzi wake aliwahi kudondosha nyundo ambayo ilikwenda kugonga sehemu yenye Tenki ambalo ni la kioo na kufanya ufa ambao uliruhusu kidogo kidogo kuingia hewa, na hatimae mripuko mkubwa ukatokea. Jambo la kushangaza ni majibu haya ambayo hayana hata hadhi ya kitaalamu, lakini pia Kamati imefichwa kwa kutopatiwa jina la fundi huyo aliyehusika na uekezaji wa kibanda, na hivyo haifahamiki kama alikuwa mtu binafsi, Mfanyakazi wa Shirika ama Kampuni nyengine inayohusika na kazi hizi.

Jambo la ajabu zaidi ni kukosekana kwa Ripoti yakinifu inayozungumzia suala hili kwa undani, ikiwa ni pamoja na sababu zake, gharama zilizotumika kurejesha umeme huo, hatua zilizochukuliwa dhidi ya waliohusika na mambo mengine. Kwa ufupi, Serikali imekaa kimya mpaka leo, haina hata haja ya kulizungumzia suala hilo, basi hata historia yake isiekwe na kuwasaidia wazanzibari wajao baadae!

Na miongoni mwa masuala ya msingi (ambapo pia tutafahamu baadae) ni ile shaka ya haja ya kununuliwa kwa majenereta hayo na mazingira ya kuharibika kwa umeme Zanzibar. Yaani, Kamati ilipokuwa inafanya mahojiano na Kampuni iliyouza Majenereta hayo (Mantrac) ilieleza kwamba, kwa kawaida wao hawatengenezi ama hawaagizi majenereta ya aina hii mpaka wapate oda maalum kwa ajili ya kununuliwa. Na hii ina maana, Shirika kuamua nunua majenereta

hayo, kama tutakavyoona baadae, na kwakuwa sababu ya kukosekana kwa umeme ina utata, ni wazi kwamba shaka ya kuwepo kwa uharibifu wa makusudi wa umeme uliokosekana miezi mitatu Unguja, itaendelea kuwepo, kwamba ni hujuma zaidi kuliko sababu nyengine inayoweza kuelezeka.

Na katika maeneo ambayo ni muhimu kushughulikiwa ni kufanyika kwa ukaguzi wa fedha zilizotumika kurejeshea huduma ya umeme baada ya kukatika kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu, mbali na majenereta 32 ambayo mpaka leo hayatumiki ipasavyo!. Lakini je, vipi fedha za wananchi walipakodi zinathaminiwa matumizi yake? Kamati kwa upande wake ilielezwa na Uongozi wa Shirika la Umeme kwamba, wao tu kama Shirika, mbali na fedha za Serikali, wametumia fedha zisizopungua Bilioni moja! Lakini ni nani anaethubutu kukagua fedha hizo? Na ni nani anaepinga kwamba, kuna shaka nyingi za matumizi halali kisheria ya fedha hizo, ukizingatia kwamba mambo yalilazimika yafanywe tu, kwa namna yoyote iwayo, alimuradi umeme urudi!

Basi, na tuendelee juu ya mjadala wa haja ya kunuliwa kwa majenereta hayo 32, ambapo Kamati ilielezwa kwamba, yametokana na Ufadhili wa nchi ya Norway, Sweden na Uingereza, ambazo ndizo nchi tatu zilizohusika na ufadhili, huku Kamati ikielezwa kwamba, nchi ya Norway ndio ilichukua jukumu lote la usimamizi wa kupatikana kwa majenereta hayo na hivyo ni sawa na kusema kwamba, nchi ya Norway ndio iliyomtafuta Mshauri Mwelekezi wa kuishauri Serikali juu ya hatua zilizohitajika kufuatwa na kupatikana kwa majenereta hayo. Katika hali kama hii, ni sawa na kusema kwamba, Shirika la Umeme baada ya kushiriki katika kutoa ushauri wa kupatikana kwa majenereta ya dharura, haikupata fursa ya kushirikishwa juu ya aina gani ya majenereta yanayotakiwa kwa ajili ya kuondosha tatizo hili na kwa matumizi mengine ya dharura, wala wapi yangelipatikana, kwa ufupi wa maneno ‘Haikushirikishwa’!.

Ni mshauri Mwelekezi wa Norway, ndie alieelekeza idadi halisi ya majenereta ya kununuliwa na wapi yangelipatikana. Maelezo haya sio lazima uyaone ya msingi, ingawaje ndio yaliyotamkwa na Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme wakati akiwa katika kikao cha pamoja na Kamati mbele ya Kampuni ya Mantrac, iliyopo Dar es Salaam. Kwa ujumla, majereta hayo yamenunuliwa katika kipindi hicho kigumu na cha dharura kuu, kiasi ambacho, hata upatikanaji wake umelazimika kwenda katika

dharura kubwa, na kama ushauri wa majenereta hayo ungelikuja leo, sio Shirika hili la Umeme lingelishauri kununuliwa kwake.

5.3.0 Taratibu za Sheria zilizotumika kununuliwa kwa Majenereta hayo:

Kama tulivyokwishasema awali kwamba, pamoja na mambo mengine, suala la msingi katika ununuzi wa majereta hayo ni kufuatwa kwa taratibu za Sheria namba 9 ya mwaka 2005 na Kanuni zake. Na kama hii ndio hali, ni vyema kwanza tukajiridhisha juu ya haja ya kununuliwa kwake kisheria. Labda suala la kwanza ungeanza kujiuliza juu ya kanuni za msingi kuhusu ununuzi wa mali za Serikali, na ungefanya hivi kwa kuongozwa na kifungu cha 19 cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2005 inayoelekeza kuwepo kwa Mpango wa Manunuzi na Ugavi wa mali hizo. Kwa maana hiyo, ni vyema tukafahamu iwapo Shirika lilipanga ama lilikuwa na mpango wa kununua majenereta ya dharura kwa ajili ya kuondosha tatizo la kukosekana kwa umeme; lakini pia, kama mpango huo ulikuwepo, jee, ulikidhi mahitaji yake kisheria?

Wakati Kamati inahojiana na Uongozi wa Shirika na hata katika kikao cha pamoja na Kampuni ya Mantrac, ilipata jawabu moja kwamba, hakukuwa na mpango wowote wa kununuliwa kwa majenereta hayo hapo kabla na haja yake imetokana na nchi kuwepo katika giza la miezi 3. Aidha, suala hili pia linahusisha kukaa ama ununuzi wa majenereta hayo kupitishwa na Bodi ya Zabuni ya Shirika ama ya Serikali, baada ya kupokea haja ya ununuzi wake kutoka Kitengo cha Watumiaji au kwa kupitia utaratibu mwengine wowote unaohusika. Kwa ujumla, hakukuwa na Bodi ya Zabuni yoyote iliyokaa na kujadili haja ya kununuliwa Majenereta hayo.

Yote haya yamefanywa kwa kukidhi hali ya dharura iliyokuwepo wakati huo na ni sawa na kusema kwamba, kazi ya kumtafuta Mshauri Mwelekezi wa Ununuzi wa Majenereta, kazi ya kuiteua Kampuni ya Mantrac iliyouza na kuyafunga majenereta hayo, kazi ya kuweka msingi (Base line) wa eneo la kuwekea majenereta hayo hapo Mtoni, badala ya kufanywa na Mamlaka husika za Manunuzi, ikiwa ni pamoja na Bodi ya Zabuni, Kitengo cha Manunuzi, Kitengo cha Watumiaji (User Department) ama Kamati ya Tathmini, zimefanywa na Mshauri Mwelekezi wa Norway. Na kwa hali hii, Kamati imejiridhisha bila ya

shaka yoyote kwamba, taratibu za Sheria ya Ununuzi wa Majenereta hayo hazikufuatwa, bila ya kujali sababu zilizoelezwa na kuonekana ni za msingi.

5.4.0 Uhalisia wa Mkataba baina ya Kampuni ya Mantrac Tanzania Ltd na Shirika la Umeme:

Pamoja na maelezo ya hapo juu, Kamati ilipofika mbele ya Kampuni ya Mantrac ili kupata ufafanuzi wa mambo mbali mbali, ilielezwa kwamba, Kampuni yao imeingia katika Mkataba na Shirika wa kuuza majenereta 32 na kuyafunga, kupitia njia zote zilizokubaliwa na sheria, yaani Sheria Namba 9 ya mwaka 2005. Kwa maana hii, pamoja na Kamati kujiridhisha juu ya maelezo ya hapo juu yaliyopatikana kutoka kwa Uongozi wa Shirika la Umeme, wakati Kamati ilipokutana na Uongozi wa Mantrac, walijisafisha kwa kueleza kwamba, wamefuata taratibu zilizopo katika kuuza majenereta hayo, na zaidi maelezo yao wakiyasimamia kwa Mkataba ulioingiwa baina yao na Shirika la Umeme. Kamati nayo imeupitia Mkataba huo na imeona vyema kutoa maelezo yafuatayo:

5.5.0 Utaratibu uliotumika kununuliwa kwa Majenereta hayo 32:

Kwa kuwa katika Ununuzi wa Majenereta 32 yenye gharama kubwa na umuhimu wa kipekee kwa Taifa, ulistahili kufanywa kwa njia ya Zabuni, lakini haikufanyika, aidha na kwa bahati mbaya hata njia ya ‘qoutation’ iliyoelezwa kwamba imetumika imeshindwa kuthibitishwa kwa Kamati. Na kwa kuwa mazingira yaliyojiri wakati huo yalihitaji majenereta hayo kununuliwa kwa haraka mno na kwa dharura, ingawaje pia Bodi ya Zabuni ilitakiwa iidhinishe njia mbadala badala ya Zabuni, kama inavyoelezwa na kifungu cha 32(2) cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2005, jambo ambalo halikufanywa. Ni vyema sasa tukafahamu utaratibu uliotumika katika ununuzi wa majenereta hayo kwa kuyapitia kwa kina maelezo haya.

Hatua ya kwanza, baada ya kukosekana kwa umeme nchini kutokana na kukatika kwa waya wa baharini kutoka Dar es Salaam, Kamati ilielezwa na Uongozi wa Shirika kwamba, kikao cha Maafa cha Makatibu Wakuu kilikaa na kujadiliana juu ya suala zima la kutafuta suluhisho la tatizo hili, huku Shirika la Umeme nalo likiwakilishwa na Ndg. Abdalla Haji Steni, ambae kwa wakati huo alikuwa ni Mkuu wa Mains. Kufuatia kikao hicho, Njia ya msingi ya dharura iliyoonekana

inafaa ni kutafutwa kwa Umeme wa Majenereta yenye uwezo mkubwa wa kutosheleza haja, huku suluhisho la kudumu la kupatikana kwa umeme huo likiendelea kufuatiliwa kidogo kidogo. Kamati ilielezwa kwamba, baada ya kikao hiki kukaa, maamuzi yaliyowafikiwa ni kutafutwa kwa Wahisani watakaoisaidia Serikali kwa kuipatia fedha za ununuzi wa majenereta yaliyohitajika. Hata hivyo, Kamati haikuweza kupatiwa taarifa zozote juu ya aina ya majenereta yaliyotakiwa ama kupendekezwa na kikao hicho kama vile ilivyokoseshwa gharama za majenereta hayo.

Hatua iliyofuata ni kuwatafuta Wafadhili hao, ambapo Kamati imeshindwa kupata uhakika wake, ni nani na kupitia Mradi gani, Wafadhili hao wamejuilishwa juu ya haja ya ununuzi wa majenereta. Hii ni kwa sababu, wakati wa mahojiano, Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme amekiri mbele ya Kamati kwamba, yeye hafahamu chochote iwapo ni Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ama ni kikao hicho maalum cha Maafa, kilichosimamiwa na Makatibu Wakuu ndicho kilichohusika na kupeleka ombi (Proposal) la Mradi huo kwa Wafadhili. Hata hivyo, imejiridhisha kwamba, wafadhili hao ambao ni Norway, Uingereza na Sweden, walipatikana na kukubali kuisaidia Zanzibar kutokana na hali ya giza ambapo Msimamizi Mkuu wa matumizi ya fedha zilizotolewa na Wahisani hao, ilikuwa ni nchi ya Norway na kwa hatua hii ndie alieteua Mshauri Mwelekezi ambapo Kamati ilijuilishwa ni Kampuni ya ‘Norplan’ iliyopo Norway.

Baada ya Kampuni ya ‘Norplan’ kuteuliwa na Ubalozi wa Norway kuwa Mshauri Mwelekezi wa Mradi ama Ununuzi wa Majenereta yote 32, Kamati imejuilishwa kwamba, Kampuni hii ndio iliitafuta Kampuni ya Mantrac na kuipa kazi ya kuleta majenereta hayo na kuyafunga (Supply and Installation) katika eneo la Mtoni-Zanzibar, huku ikiingia Mkataba na Kampuni ya Salcom Contractor, iliyopewa kazi ya kueka msingi (Base Line) ya eneo lilitumika kukaa majenereta hayo. Tunapenda ifahamike kwamba, ufafanuzi huu ndio uliotolewa na Uongozi wa Shirika kwa Kamati, ingawaje kwa uchambuzi wa Kamati, suala la nani aliehusika na ununuzi wa Majenereta hayo, litaelezwa hapo baadae.

5.6.0 Kampuni ya Mantrac na Mahusiano yake na Shirika:

Eneo jengine muhimu kulifahamu kwa mujibu wa hoja hii, ni Kampuni ya Mantrac, ambayo hapo juu tumeieleza kwamba ndio iliyoteuliwa na Mshauri

Mwelekezi wa Mradi huu wa Majenereta 32 na hatimae Kampuni hii imeiuzia Shirika majenereta hayo. Ili kuifahamu vyema Kampuni hii, ni sawa kama tutapata maelezo juu ya uwepo wake Nchini Tanzania na kazi inazozifanya, namna ilivyolifahamu Shirika la Umeme na uhusiano wao ulivyo hivi sasa kuhusiana na majenereta hayo.

Tukianzia na Uwepo wa Kampuni hii, Kamati imeelezwa kwamba Kampuni ya 'Unatrac International' yenye makao yake makuu nchini Marekani, ni Kampuni iloyopewa ruhusa kamili na Kampuni ya 'Caterpillar' yenye makao makuu yake nchini Marekani, ya kuuza vifaa vyote vinavozalishwa na Kampuni hii ya 'Caterpillar'. 'Unatrac International' iliyopo Marekani ndio yenye dhamana hiyo huku ikiwa na matawi yake katika nchi 5 za Afrika, ikiwa ni pamoja na nchini Tanzania. Kwa lugha hii, Kampuni hii ya Mantrac Tanzania Ltd, nayo imepewa ruhusa kamili ya kuuza bidhaa za Kampuni ya 'Caterpillar' nchini na kupata msaada kamili wa Kampuni ya 'Caterpillar' juu ya bidhaa zozote itakazoziuza ama kuvifanyia biashara yoyote kwa Kampuni hii ya 'Mantrac Tanzania Ltd'. **(Kiambatanisho Nam 93).**

Meneja wa Kampuni hii akitoa ufafanuzi wake kuhusiana na namna gani walilifahamu Shirika la Umeme, kiasi ya kuweza kupewa kazi husika, alithibitisha kwamba, waliwahi kufika katika Shirika na kuzieleza kazi zao tokea hata halijatokea tatizo la kuzimwa kwa umeme katika kipindi cha miezi mitatu mfululizo. Alisema kwamba, baada ya kutokezea tatizo la umeme, wao waliitwa (akikusudia kupitia tangazo la 'Qoutation') na kufanikiwa kupeleka maombi yao na hatimae walifanikiwa kushinda na kupewa kazi hiyo ya 'supply and installation' ya majenereta. Aidha, kuhusu malipo waliyolipwa kwa kazi hiyo, Kamati kwa kipindi kirefu cha kufuatilia hoja hii haikufanikiwa kupata uhakika wa bei hiyo, ingawaje baada ya kujitokeza tena haja ya kupewa kiwango maalum cha majenereta hayo, Meneja wa Shirika alikuwa hana uhakika wa bei yake, na kuahidi kuwasilisha kwa Kamati taarifa za bei hiyo kwa siku zinazofuata, jambo ambalo hajalifanya hadi leo tunawasilisha ripoti hii.

Hata hivyo, suala la msingi lilikuwa, je fedha zilizolipwa kununulia majenereta hayo zimetoka katika Mfuko wa Shirika, Akaunti maalum ya Mradi iliyosimamiwa na Shirika ama zimetoka moja kwa moja kutoka mikononi mwa Wahisani

(Uingereza, Sweden na Norway)?. Katika kutoa ufafanuzi wa suala hili, Meneja wa Shirika alieleza Kamati kwamba, fedha hizo hazitokani na Akaunti yoyote inayoihusisha Shirika lake, yaani sio kupitia Akaunti ya Shirika wala Akaunti iliyolipwa kutoka katika Mradi huu. Hata hivyo, baada ya kuwasili Ndg. James Serre, Meneja Mauzo wa Kampuni ya Mantrac, aliithibitishia Kamati kwamba wao wamelipwa USD 1,208,800 kupitia Cheki iliyotolewa na Benki ya Watu wa Zanzibar **(Kiambatanisho Nam 94)**. Hali hii imeithibitishia Kamati kwamba, fedha hizo zimetolewa katika Akaunti maalum ya Mradi huu uliosimamiwa na Shirika. Aidha, Meneja Mkuu ameficha ukweli uliohitajika kwa Kamati.

Jambo jengine ambalo Kamati inaona ni la msingi kufahamika kuhusiana na uhusiano wa Shirika na Kampuni ya Mantrac Tanzania Ltd, ni Mkataba ulioingiwa baina ya Taasisi mbili hizi na ni vyema tukaueleza Mkataba huo katika maeneo yake ya msingi, ili kuwepesisha uelewa unaohitajika. Kwanza tunapenda tufahamike wazi kwamba, katika wakati wote wa kazi za Kamati, taarifa za Shirika hazikuwa wazi moja kwa moja, na mara nyengine zilifichwa kabisa. Moja katika maeneo ambayo Kamati imekosa kupewa taarifa za wazi ni eneo hili. Kwa mfano, Kamati ilipohoji juu ya kuhusika kwa Shirika na Mradi huu, haikuwa rahisi kwa Meneja Mkuu kukiri mbele ya Kamati namna gani Shirika lake limehusika, na mara zote alieleza kwamba, Shirika halikuhusika na mradi huu tokea awali isipokuwa limehusika katika kuyasimamia majenereta hayo 32 baada ya kufungwa na kufanya kazi; yaani kuhusika katika kuyaendesha na kutoa huduma iliyokusudiwa.

Pia kuhusiana na kupatikana kwa Kampuni hii ya Mantrac, Meneja wa Shirika aling'ang'ania kwamba Shirika halikuhusika, yaani mambo na maelewano yote baina ya Kampuni ya Mantrac na majukumu yake ya kuuza majenereta 32 hadi kufungwa kwake, yameingiwa na Mshauri Mwelekezi kutoka Kampuni ya 'Norplan'. Sasa tunapoamua kuupitia Mkataba huu uliowasilishwa kwa Kamati na Kampuni ya Mantrac, tunafahamu mambo mengi ambayo bila ya kupatikana kwa ufafanuzi kutoka kwa Kampuni ya Mantrac sambamba na kupatikana kwa Mkataba huu, ukweli huo tusingeliweza kuueleza kama ulivyo usahihi wake.

5.6.1 Mkataba wa Kutoa huduma ya majenereta 32 yenye uwezo wa Megawat 25 (25 MW):

Mkataba huu ambao katika taarifa yetu tunaufanya ni **Kiambatanisho Nam 95,** umeingiwa baina ya Shirika la Umeme na Kampuni ya Mantrac Tanzania Ltd, kwa ajili ya kusambaza (Supply), kusafirisha (Transport), kufunga (Install) na kazi ya kuzalisha umeme (Commission the Power Plant) katika eneo la Mtoni Zanzibar. Mkataba huu wa Tarehe 01/02/2010, unaonesha wazi kwamba pande zote mbili zimeridhiana kutekelezwa kwa kazi hiyo huku maelezo ya kina juu ya sifa za majenereta na kazi yote yakitolewa katika maelezo ya Mkataba huo. Kwa mujibu wa Mkataba huu, kazi yote iliyokabidhiwa kwa Kampuni ya Mantrac ina thamani ya USD 12,985,000 ni sawa na Tsh. 19,477,500,000 (kwa kiwango cha Dola moja kwa 1500 wakati huo).

Jambo jengine muhimu kufahamika katika Mkataba huu ni hizi hati 6 zilizotambuliwa kuwa ni sehemu ya Mkataba na kwa maslahi ya ufafanuzi huu, ni vyema tukazipitia angalau kwa uchache hati moja baada ya nyengine:

5.6.2 Barua ya kukubaliwa (Letter of Acceptance) ikiambatanishwa na kumbu kumbu za Mkutano wa Majadiliano kabla ya kufungwa kwa Mkataba:

Barua hii imeandaliwa na Shirika la Umeme na kutiwa saini na pande zote mbili zilizohusika na Mkataba, inathibitisha kukubaliwa kwa Kampuni ya Mantrac kufanya kazi inayohusiana na majenereta yote 32. Katika barua hii, ambapo Shirika kama ilivyojieleza katika Mkataba kuwa ni Mwajiri (Employer) na Kampuni ya Mantrac kuwa ni Mjenzi (Contractor), ina lengo hilo hilo la kazi ya kutengeneza kituo cha kuzalishia umeme wa majenereta hayo eneo la Mtoni Zanzibar, huku ikitajwa bei na ukubwa wa kazi kama ilivyoelezwa katika Mkataba (Rejea Kiambatanisho hiki), utaratibu wa kumaliza kwa kazi hiyo na kukabidhiwa kwake.

Aidha, katika barua hiyo pia imeambatanishwa na kumbu kumbu za Mkutano uliofanywa na Viongozi wa Shirika, Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika, Washauri wa Mradi kutoka Shirika la Umeme, Washauri Waelekezi wa Mradi kutoka ‘Norplan’, Viongozi wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi,

Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na Viongozi wa Kampuni ya Mantrac. Lengo la mkutano huo ni kujadiliana kuhusu maombi ya Kampuni ya Mantract ya kukubaliwa kuwauzia Shirika majenereta 32, kabla ya Kampuni hii kukabidhiwa kazi hiyo, huku taarifa ya wazi kwamba Kampuni hii imekubaliwa na kuwa mshindi wa zabuni iliyotangazwa na tathmini iliyofanywa, inathibitisha wazi kwamba, lengo la Mkutano huo ni kujadiliana vipi Mkataba wa kazi hiyo ungeweza kufungwa baina ya pande mbili zilizohusika.

Kitu cha msingi tunachokitaka kifahamike katika kipengele hiki ni namna gani Shirika la Umeme na Serikali kwa ujumla zilivyohusika katika kupatikana kwa majenereta 32, kinyume na maelekezo ya Meneja Mkuu wa Shirika hili kudai kwamba, wao hawakuhusika katika taratibu za kupatikana kwa Kampuni ya Mantrac bali walihusishwa siku moja tu, pale Mwakilishi wao aliposhiriki katika kikao cha Maafa cha Makatibu Wakuu waliokaa kujadiliana namna ya kupata Majenereta ya dharura.

5.6.3 Nyongeza ya Mkataba (The Addenda nos):

Jambo jengine muhimu liliomo katika Mkataba huu uliokabidhiwa kwa Kamati, ni nyongeza ya Mkataba inayozungumzia haja ya uwepo wa Mradi huo na uwezo wa majenereta yanayohitajika. Njia iliyotuumika ya kumpata Mjenzi, yaani Kampuni ya Mantrac, ambapo imetumika njia ya Dharura (Emergency Procurement Method) kama ilivyoelezwa kwatika kanuni ya 27(1) ya Kanuni za Manunuzi na Ugavi wa Mali za Serikali, Namna zabuni hiyo ilivyofanyiwa tathmini na hatimae kufanikiwa kwa Mantrac, namna ya mapatano baada ya kukubaliwa huko na kabla ya kuingia katika Mkataba yalivyofanyika.

Vile vile imezungumzia hati zilizokusudiwa kuwa sehemu ya Mkataba, Mpangilio wa Uongozi wa Shirika, Upeo wa kazina muda wa kukamilika kwa kazi ya kufungwa na kuanza kazi kwa majenereta hayo, huku kazi itakayofanywa ikihakikishiwa kufanywa katika kiwango bora na cha ufanisi sana, na sehemu ya mwisho ni kulitambulisha Shirika kama ni mwajiri wa Mradi huo.

Jambo la msingi tunalojifunza katika sehemu hii ni kwamba, Shirika linatambua kwamba, Kampuni ya Mantrac imepewa kazi ya kuleta majenereta 32 kupitia taratibu za manunuzi zilizotumika kuipata Kampuni hii, ambayo ni njia ya dharura,

yaani ni kwa mnasaba wa hali ya kukosekana kwa umeme Unguja nzima. Maelezo haya sio yaliyotolewa na Meneja Mkuu wa Shirika, ambae muda wote alisimamia hoja ya kutohusishwa kwa Shirika lake katika utaratibu mzima wa kumpata Kampuni ya Mantrac na kwa hoja hii, ni sawa na kusema kwamba, Uongozi wa Shirika uliufahamu ukweli ila lilikusudia kuipotosha Kamati.

5.6.4 Masharti ya Jumla na Maalum (The General and Special Condittions of Contract):

Mkataba huu pia umejumuisha masharti ya jumla ambapo miongoni mwayo ni pamoja na namna ya usafirishaji wa Majenereta hayo, ulipaji wa fedha za dhamana (Performance Security) na muda wa kuwasilishwa kwake, uasili wa majenereta husika (Country of Origin), msamaha wa kodi kwa majenereta yanayohusika kwa kuletwa nchini na Kampuni ya Mantrac, namna ya ulipwaji wa gharama za majenereta na kazi ya kuyafunga kwa Kampuni ya Mantrac, ikiwa ni pamoja na haki za wafanyakazi wa Mantrac na namna ya ulipwaji wa fidia kwa hasara zozote baina ya Shirika na Kampuni, utatuzi wa migogoro itakayotokea baina ya Shirika na Kampuni hii na mambo mengine yanayohusiana.

Kwa upande wa masharti Maalum yaliyohusika katika Mkataba huu ni pamoja na Nyaraka muhimu zitakazohusika wakati wa mgogoro baina ya pande hizi mbili, baada ya kukamilika kwa Mkataba, nafasi ya vifaa ambavyo hapo awali havikuhusika katika Mkataba, ujuzi wa kazi bei na vyengine vipi vingelishughulikiwa. Nyaraka na Michoro inavyopaswa kutayarishwa, na kuwasilishwa baina ya pande hizo mbili, taratibu za kuonesha uwezo wa Kampuni na uhakika wa kazi atakayoifanya, ukaguzi na majaribio ya majenereta, namna ya uwekaji wake, usafirishaji na uhifadhi, mafunzo yatakayotolewa kwa Shirika kuhusiana na ufungaji mzima wa majenereta na ufanyaji kazi wake na vifaa vitakavyotumiwa na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Miongoni mwa mambo ya msingi yaliyohusika na sehemu hii ya Mkataba ni pamoja na uchambuzi wa kina wa Majenereta hayo ikiwa ni pamoja na aina na uwezo wake (Capacity for the Gensets), sampuli ya mashine (Engine Specifications), sifa za mafuta yake, vigezo vya muundo wake na vielelezo vilivyomo, kwa ujumla, Mkataba huo umejumuisha kila kitu kilichoelezwa ama kilichotakiwa katika Majenereta husika.

Miongoni mwa mahitaji ya Shirika yaliyohusika na Mkataba huo ni pamoja na kupata hakika ya nyenzo (Materials) zitakazotumika na bei ya hakika ya kukamilika kwa kazi hiyo, kuhakikishiwa usafishwaji wa eneo la kuyaweka majenereta husika ili kuwa katika hali nzuri na namna bora ya ujenzi wa sehemu ya kuhifadhiwa kwake, aina ya saruji na maji ya kutumika, namna ya usimamizi wa kazi husika na mambo mengine yanayohusika.

Kwa kumalizia, Mkataba huu pia umejumuisha mapendekezo ya Mantrac kuhusiana na mradi huu, ikiwa ni pamoja na hati ya madai ya malipo juu ya uuzaji wa majenereta yote 32, inayoainisha aina ya majenereta, transforma, namna ya kupokelewa kwake na nchi yanayotokea pamoja na utaratibu wa malipo kwa ufupi wake. Pia inajumuisha utaratibu mzima wa kufungwa na kuanza kazi kwa majenereta hayo na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

5.7.0 Mahusiano ya Shirika la Umeme na Kampuni ya China Railway Jianchang Engineering Co. (T) Ltd:

Kama tulivyokwisha eleza hapo kabla, kwamba mara tu baada ya Kampuni ya Mantrac kupewa kazi ya kuwauzia Majenereta Shirika la Umeme na kuyafunga, kama Kampuni, walilazimika kumtafuta Mjenzi wa Msingi (Civil Works) na kuweka hali ya usafi kwa eneo lote litakalotumika kuwekea majenereta hayo. Kazi hiyo kwa bahati njema, iliombwa na Kampuni kuu mbili; moja ni hii ya Kichina, ya China Railway Jianchang Engeneering Co. (T) Ltd, ama umaarufu wake ni (CRJE), na Kampuni ya pili ni Salem Construction ama umaarufu wake ni (SALCON). Kampuni hizi ziliingia katika ushindani wa bei na namna ya kufanya kazi hiyo, ambapo kwa Upande wa Kampuni ya CRJE walitaka kupewa kazi hiyo kwa gharama za USD 600,413.58 wakati Kampuni ya Salcon, wangeliifanya kwa USD 431,622.80 **(Kiambatanisho Nam 96)**.

Ili Kampuni iridhiwe, ni lazima ikubaliwe na Shirika pamoja na kupata idhini ya Kampuni ya Mantrac. Kwa bahati njema, katika Kiambatanisho tulichokieleza punde hapo juu, Shirika halikuwa na pingamizi ya kupewa kwa Kampuni yoyote hapo kabla, wakati wanapeleka taarifa hizo kwa Kampuni ya Mantrac, ingawaje waliona kwamba, Kampuni ya Salcon ina nafasi nzuri ya kushinda kwa sababu hata bei yake ni ndogo kwa ghrama ya USD 168,790.78 ambapo wao katika kiambatanisho hicho wameinukuu kama 170,000 USD. Aidha, pia mwisho wa

kiambatanisho hicho (Conclusion) ilimalizia kwa Shirika pia kuridhia kupewa kazi hii Kampuni ya Salcon.

Pamoja na hali hiyo, kwa upande wa Kampuni ya Mantrac waliieleza Kamati kwamba, wao tokea mwanzo kama ndio waliopewa kazi kuu ya kuyafunga Majenereta hayo, walitaka kazi ya kuweka Msingi wake (Civil and Electro-mechanical works at the power plant) ifanywe na Kampuni ya Salcon. Hata hivyo, kwa mujibu wa barua ya Tarehe 1/03/2010 yenye kumbu kumbu namba ZECO/CONF.2/10/2/GEN/VOL.11/367 iliyoandikwa na Kaimu Meneja Mkuu wa Shirika, ambae sasa ndie Meneja Mkuu, Ndg. Hassan A. Mbarouk **(Kiambatanisho Nam 97)**, inaelekeza kama kwamba, Kampuni ya Mantrac ilihitaji zaidi kuipa Kampuni ya Kichini ya CRJE zaidi kuliko ya Salcon na hivyo, Shirika kwa barua hiyo imeitambua Kampuni hiyo ya CRJE kuwa ndio iliyopewa kazi.

Aidha, mnamo wiki tu baadae, Meneja Mkuu huyu huyu wa Shirika la Umeme, ameweka bayana kwamba, kumbe ni Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika, ndiyo iliyoamua kazi hiyo apewe Kampuni ya Kichina ya CRJE badala ya Kampuni ya Salcon na matokeo yake, kazi hiyo ikaanza kufanywa na Kampuni ya CRJE. Kwa hali yoyote ile iwayo, jambo la msingi ni kufahamu kwamba, Kampuni ya Salcon haikupewa kazi hiyo kabla, mbali na kuonesha uwezo wao wa kuifanya kazi hiyo kwa ubora na gharama ndogo zaidi.

Jambo la kusikitisha ni kwamba, Kamati ilielezwa na Uongozi wa Mantrac kwamba, Msimamizi wa Mradi huu Kampuni ya Norplan, haijakubali kazi hiyo kupewa Kampuni ya CRJE na wakatishia kujitoa katika Mradi na hili liliwashtua Uongozi wa Shirika na kuamua kukubaliana kwa shingo upande na matakwa ya Mfadhili ambae anasimamiwa na Mshauri Mwelekezi ‘Norplan’. Matokeo yake, Kazi hiyo ikanyang’anywa kwa Kampuni ya CRJE na kupewa Kampuni ya Salcon.

Jambo hili ilikuwa ni sawa na kuvunjwa kwa Mkataba kwa Kampuni ya CRJE na ni sawa na kusema ‘wamenyang’anywa tonge mdomoni’ na kwa namna yoyote ile walidai fidia ambao ingeligharimu USD 86,613.07 ingawaje baadae ilikubalika kulipwa USD 20,786.00 ambazo kwa wakati huo ni sawa na Tsh. 31,179,000/- zilizotoka katika Account ya Shirika la Umeme, kwa kile kinachoitwa uzembe na uroho wa kulazimisha mambo kwa utashi wa viongozi wachache wa Bodi ya

Wakurugenzi, iliyofanya maamuzi bila ya kuzingatia uhalisia wa kazi na ufanisi wake **(Kiambatanisho Nam 98)**.

Katika waraka Namba 438 Uongozi wa Shirika uliomba idhini kwa Bodi hii hii ya Wakurugenzi, iliyosababisha hasara hizo, kutoa idhini ya kulipwa kwa CRJE fedha hizo USD 20,786.00 na Kamati imehakikishiwa kwamba idhini hiyo ilitoka kama ilivyoombwa na hatimae CRJE walilipwa.

5.8.0 Hoja kuhusiana na Taratibu za Manunuzi:

Bila ya shaka bado ipo haja ya kuweka wazi mtazamo wa Kamati juu ya taratibu za upatikanaji wa Majenereta 32 kama ulifuata Sheria, na zaidi kwa kuzingatia kwamba, suala hili limeonekana kupokea miono tofauti inayokinzana, baina ya Uongozi wa Shirika, Uongozi wa Kampuni ya Mantrac na Kamati hii. Kwa hivyo, hebu sasa tuzingatie ile hoja iliyotolewa na Kampuni ya Mantrac juu kununuliwa kwa Majenereta haya kwa Njia ya Dharura (Emergency Procurement).

Kama tulivyokwisha eleza kwamba, kama utafanya rejea ya maneno 'Emergency Procurement' katika Sheria Na.9 ya mwaka 2005 na Kanuni zake, utakutana na kanuni ya 27(1) inayozungumzia suala hili kwa uwazi wake. Hebu na Tujikumbushe kwa kunukuu haya yafuatayo:

> "Katika mazingira yasiyo ya kawaida na ya dharura, pale ambapo Afisa Mhasibu atazingatia kwa maslahi ya Umma, kwamba manunuzi yafanywe, ambayo gharama zake zinazidi kiwango kilichopewa katika Kanuni hizi na muda hauruhusu mamlaka kutumia njia ya kawaida, (Afisa huyo Mhasibu) kwa kuwajibika yeye mwenyewe juu ya manunuzi hayo (atafanya manunuzi hayo), **lakini mara tu baada ya kufanya manunuzi hayo, atamuarifu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo, akimueleza sababu zilizompelekea yeye kuacha kufanya manunuzi kwa njia ya kawaida na kopi ya barua hiyo itapelekwa kwa Bodi yenye mamlaka ya kuthibitisha (kwa Shirika, Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika) na Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma[10]"**

Ukifanya rejea ya nukuu hiyo hapo juu na zaidi katika maneno yaliyokozeshwa, yatakufahamisha kwamba, pamoja kukubaliana kwamba, kweli ununuzi wa majenereta hayo ulifanywa katika kipindi cha dharura kubwa, lakini jee taratibu za

[10] Tafsiri ni yetu.

ununuzi wa dharura kwa mujibu wa Sheria zilifuatwa? Jawabu yake kwa Kamati ilikuwa nyepesi mno, kwamba haikufuatwa kwa sababu Uongozi wa Shirika umeshindwa kuthibitisha kufuata kwa taratibu hizo kwa kumuarifu Katibu Mkuu anaehusika na Fedha ama kopi ya barua hiyo kupelekwa kwa Bodi na Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma.

Kama hili halitoshi, unaweza pia kufanya rejea ya kifungu cha 32(2) cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2005, ambapo utakutana na maelezo yafuatayo"

"The choice of a procurement method shall first be approved by the Tender Boards"

Kwamba, Ni Bodi ya Zabuni ya Shirika la Umeme iliyokuwa na wajibu wa kuthibitisha haja ya kutumika kwa njia ya 'Emergency Procurement' na sio Kikao chochote ikiwa cha Makatibu Wakuu ama chenginecho. Kwa kuwa Kamati imeshindwa kupata uthibitisho wa kuidhinishwa na Bodi, aidha kwa kuridhishwa kwamba, hakuna Bodi yoyote ya Zabuni ya Shirika iliyokaa na kuridhia njia hii, hakuna haja ya kurefusha sana maneno ya ufafanuzi wa hoja hii, Kamati imejiridhisha kwamba, manunuzi ya majenereta hayo hayakuwa halali kisheria.

5.9.0 Matumizi ya Majenereta 32:

Kama tulivyokwisha eleza awali, kwamba, kwa namna yoyote hoja hii ili ijibike vizuri, ni lazima tuangalie iwapo majenereta yote 32 yaliyonunuliwa kwa utaratibu wa hapo juu yanatumika ipasavyo kama ilivyokusudiwa kwa maslahi ya wananchi wa nchi hii. Kamati ilitembelea eneo la majenereta hayo yaliyopo eneo la Mtoni na kuzungumza na mhusika aliyekuwepo katika eneo hilo na kupata maelezo kwamba, majenereta yote isipokuwa moja, yanatumika na kufanya kazi kama kawaida, Kamati pia ilitaka kujaribiwa kwa kuwashwa ili ijiridhishe, jambo ambalo limefanyika kwa uzuri kabisa. Wakati Kamati inahoji juu ya jenereta moja ambalo halikuwepo wakati wa ukaguzi, ilielezwa kwamba liliharibika wakati wa kuletwa kwake na hivyo ikalazimika kurejeshwa kwa Kampuni ya Mantrac. Hata hivyo, katika kikao cha pamoja na Kampuni hiyo, Dar es Salaam, ilielezwa kwamba tayari jenereta hilo limeshawasilishwa na kufungwa katika eneo la Mtoni na linafanya kazi. Kwa maana hii, Kamati imejiridhisha kwamba, majenereta yote 32 yanafanya kazi.

Pamoja na maelezo haya, ni vyema sasa tukaingia ndani kidogo katika ufahamu wa hoja husika inayohoji “Iwapo upatikanaji wa majenereta 32 yaliyopo Mtoni ulifuata sheria zinazohusika na **kwa nini hayatumiwi kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar?**”. Hoja hii kwa upande wa maneno tuliyoyakozesha inahoji juu ya sababu zinazopelekea majenereta hayo kutotumiwa kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar. Yaani, ili kuijibu vizuri, ni lazima kwanza ufahamu iwapo bado yanafanya kazi ama laa, lakini hoja yenyewe inakubali kwamba majenereta yapo na yanafanya kazi, lakini kwa nini hayafanyi kazi iliyokusudiwa kwa ufanisi wake ili wananachi wa Zanzibar wakaondokewa na tatizo la mgao ama kukosa umeme wakati wowote wa maisha yao ya sasa!

Sasa ni vyema tukajikumbusha kwamba, majenereta haya yamenunuliwa wakati wa kukosekana kwa umeme Unguja na kwa ajili ya kuondosha tatizo kama hili wakati wowote wa dharura, yaani yalipaswa yatumike ipasavyo wakati huo wa uhaba wa umeme lakini pia kusiwe na haja yoyote ya kuwepo kwa mgao wa umeme wakati huu tunaondelea nao. Yaani kwa kuwa hivi sasa wananchi wote wa Unguja wanakosa umeme kwa muda wa saa 1:30 katika kipindi cha usiku, kulikuwa hakuna haja ya kuwepo kwa hali hii, kwa sababu majenereta 32 kama yatatumika ipasavyo na kwa lengo lililokusudiwa, tatizo hili halitakuwepo. Aidha, pia hakukuwa na haja ya wananchi kukosa huduma ya umeme kutokana na kuzimwa masaa 12, 6 ama hata saa 1, kama inavyofanyika takriban katika siku nyingi za mapumziko na siku za kawaida wakati wa asubuhi, mchana na usiku.

Kama hali ndio hii, jawabu ya wazi ni kwamba, majenereta hayo 32 hayatumiwi ipasavyo kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar ambao bado wanaendelea kupata machungu ya kukosa umeme wa uhakika na matokeo yake ni kuharibikiwa katika shughuli zao za maisha ya kila siku. Tunapenda ifahamike wazi kwamba, wakati wote wa kazi za Kamati, mjadala juu ya kutotumika ipasavyo kwa majenereta hayo haukubishaniwa. Yaani hata Shirika linakiri kwamba kuyaendesha majenereta hayo ni gharama kubwa na ni sehemu ya kulitia hasara Shirika, lakini jambo muhimu ni kufahamu sababu zipi zinazopelekea majenerea hayo kutotumika kama ilivyokusudiwa.

Kabla ya kuanza kueleza sababu hizo, Uongozi wa Shirika umeieleza Kamati kwamba, majenereta hayo baada ya kumalizika kipindi cha miezi mitatu ya giza

Unguja nzima, sasa yanatumika kupunguza mzigo wa usumbufu wa umeme kwa wananchi kwa kuwashwa wakati umeme unapozimwa. Yaani kama umeme ungelistahiki kuzimwa kwa masaa matatu (kwa mfano), saa 1 ama 12 wakati wa asubuhi, mchana na usiku; basi kwa kutumia majenereta hayo, umeme ungelipatikana kwa kutumiwa majenereta hayo kama mbadala wa umeme husika. Pia husaidia kupunguza mzigo wa matumizi ya umeme wakati wa matumizi makubwa kutokana na shughuli ama tukio Fulani. Kwa mfano wakati wa sikukuu yoyote ile, umeme hutumika kwa kiwango kikubwa, na majenereta hayo husaidia kuongeza uzalishaji wa umeme.

Kwa maelezo haya, ni wazi kwamba majenereta hayo yanatumika, labda tukitaka yatumike ipasavyo, ndio jambo linaloshindikana. Na hili linatokana na sababu kadhaa, lakini kubwa ni ile inayoelezwa na Shirika wakati wote kabla ya Kamati hii kulifanyia kazi suala hili, nayo ni kukosekana kwa mafuta ya kuendeshea majenereta hayo. Hoja hii pia ilisimamiwa wakati wote wa kazi za Kamati, na ilifahamika kwa uwazi wake pale Kamati ilipokutana na Kampuni ya Mantrac. Yaani muda wote huo Kamati ilielezwa kwamba, mafuta yaliyohitajika kuendeshea majenereta hayo ni ghali sana na ni tofauti na mafuta ya kawaida ambayo hutumika kwa majenereta ama mashine nyengine.

Wakati Kamati inapata ufafanuzi wake, ilielezwa na wauzaji wa majenereta hayo kwamba yanatumia mafuta ya Diesel kama diesel nyengine, ingawaje wao kama Kampuni na zaidi wakati wa ‘warranty’ ya majenereta hayo, waliwashauri Shirika kwa maslahi ya uhai wa muda mrefu wa majenereta wasitumie diesel hii, ambayo mara nyingi huwa na ‘calcium’ ambayo huathiri kidogo kidogo uimara wa majenereta. Kwa maana hii, Kamati imeridhika kwamba, majenereta hayo hayatumiwi ipasavyo kwa sababu Shirika halina uwezo mkubwa wa kununua mafuta yanayohitajika.

Wakati Kamati inataka kujua sababu zipi zinazopelekea Shirika hili kushindwa kumudu gharama za mafuta, wakati lilishiriki ipasavyo kununuliwa kwake, na lilipaswa kuyaona haya kabla ya majenereta hayo kununuliwa, ilielezwa na Meneja wa Shirika kwamba, hawapati msaada wowote wa uendeshaji wake kutoka Serikalini (Administrative Costs), kinyume na ushauri ambao wataalamu wa Shirika waliutoa wa kuitaka Serikali ama ingeongeza kodi wakati wa kuingizwa

kwake, ama kuchangia huduma za uendeshaji kama vile ambayo hata TANESCO wanapata kutoka kwa Serikali ya Muungano. Kama ni hivi, si vibaya kusema kwamba, Serikali Kuu imelibebesha Shirika mzigo usiouweza wa kuyasimamia na kuyashughulikia Majenereta yanayotumia mafuta ya gharama kubwa.

5.10.0 Muhtasari wa Mambo yaliyobainika na Kamati kufuatia Uchunguzi wake wa Hadidu hii Rejea:

i. Unununi wa Majenereta 32 umefanywa na Shirika la Umeme kupitia Ufadhili wa USD 1,208,800.00 na kwa namna hii, Shirika lililazimika kununua Majenereta hayo kwa kufuata Sheria zinazohusika na Manunuzi ya Mali za Serikali, Zanzibar.

ii. Shirika limekiuka taratibu za manunuzi kwa kutoshirikisha vyombo vyake vinavyohusika na kazi ya manunuzi, ikiwa ni pamoja na Bodi ya Zabuni ya Shirika na Kitengo cha Manunuzi (PMU).

iii. Shirika limeingia hasara ya Tsh 31,179,000/- ya malipo ya faini kwa Kampuni ya Kichina (China Railway Jianchang Engeneering Co. (T) Ltd (CRJE), ambapo hasara hii imesababishwa na uzembe na ubinafsi wa aliekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Wajumbe wote wa Bodi hii kwa ujumla.

iv. Majenereta 32 hayatumiwi ipasavyo kinyume na makusudio ya kununuliwa kwake, kwa sababu Shirika lilikurupuka kuyanunua bila ya kuangalia ukubwa na uzito wa gharama za uendeshaji wake.

v. Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme ametoa maelekezo yasiyo ya kweli kwa kukana Shirika lake kuhusika moja kwa moja na ununuzi wa majenereta 32.

vi. Serikali haijalichukulia kwa makini tatizo la kukosekana kwa umeme kwa muda wa miezi mitatu mfululizo mwaka 2010 kisiwani Unguja, ikiwa ni pamoja na kutofanya ukaguzi wowote wa matumizi ya fedha zilizotumika kurejeshea huduma hiyo; kufanya utafiti na kufahamu chanzo cha tatizo na utatuzi wake; pamoja na kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria wale wote waliohusika na kadhia hii.

vii. Shirika halikuzingatia uwezo wa kuyaendesha majenereta waliyoyanunua na hivyo kununuliwa kwake kumebakia kuwa mzigo mzito wa Shirika na Serikali kwa ujumla, huku Serikali pia haioni haja ya kusaidia uendeshaji wa majenereta hayo.

viii kwa vile gharama za kununua mafuta ya disel maalum ni kubwa, na kwa sababu majenereta hayo yakitumi mafuta ya disel hii ya kawaida hayatakuwa na madhara, basi ni vyema Shirika litumie mafuta hayo kwa dharura.

HADIDU REJEA YA SITA:

KIWANGO CHA DENI LINALODAIWA ZANZIBAR NA TANESCO, NA IWAPO KUNA SABABU ZA MSINGI ZA KUENDELEA KUWEPO KWA DENI HILO NA ATHARI ZAKE KWA MASLAHI YA ZANZIBAR.

6.0.0 Ufafanuzi wa Hadidu Rejea :

Hadidu hii rejea ilimalizia kufuatiliwa Tarehe 01/10/2012 baada ya Kamati kukutana moja kwa moja na Uongozi wa Shirika la Umeme la Tanzania, TANESCO na Shirika la Umeme la Zanzibar liliwakilishwa na Meneja Mkuu aliefuatana na Meneja wake wa Fedha, Ndg. Riziki Faki Hamad. Kabla ya kikao hicho kilichofanyika Dar es Salaam, Kamati iliwahi kupata maelezo ya hoja hii kutoka kwa Uongozi wa Shirika na ndipo ilipoamua kwenda Dar es Salaam na kukutana na TANESCO. Kwa namna Kamati ilivyolifuatilia suala hili, inaona busara ufafanuzi ufuatao ukapatikana:

6.1.0 Historia ya Deni:

Historia ya deni la Shirika la Umeme la Zanzibar inaanza katika mwaka 2008, kuanzia Tarehe 1 Januari. Inawezekana sana kukawa na deni kabla ya muda huo, jambo kubwa la kuzingatia ni taarifa iliyowasilishwa kwa Kamati, inayoonesha mchanganuo wa deno hilo kuanzia muda tuliokwisha kuueleza **(Kiambatanisho Nam 99)**, huku maelezo yote kuhusiana na deni hili kutoka kwa Meneja wa ZECO na hata Uongozi wa TANESCO, yanakubaliana kwamba deni hilo lilianza wakati huo. Kwa muda huo deni lililokuwa linadaiwa kwa ZECO ni Tsh. 1,871,545,517.70 na kulipwa kidogo kidogo, mara mbili kwa mwezi, ila kutokana na sababu kadhaa, deni hilo hadi kufikia Tarehe 1/06/2012 linakisiwa kufikia Tsh. 22,767,047,816.06

Inaelezwa pia kwamba, Shirika la Umeme la Zanzibar linalifahamu deni hilo katika ngazi mbili. Sehemu ya kwanza ni deni halali wanalodaiwa na TANESCO ambalo hili halibishaniwi na sehemu ya pili ya deni hilo ni deni ambalo Shirika hili linaona halina usahihi wowote ule wa kudaiwa na TANESCO. Katika hali hii,

inafaa upatikane ufafanuzi juu ya madai hayo ya Shirika, na hoja zinazofuata zinatoa ufafanuzi huo:

6.2.0 Msingi wa Deni na kuendelea kwake:

Miongoni mwa vipengele muhimu katika kutoa ufafanuzi wa hoja hii, ni pamoja na kujiridhisha juu ya sababu za msingi zinazopelekea kuwepo kwa deni hilo. Na inafahamika pia kwamba, Umeme ambao Zanzibar tunatumia unatoka Tanzania bara, ambapo Shirika la Umeme la Tanzania, TANESCO ni wakala wa Serikali ya Tanzania lenye jukumu la kununua na kusambaza ama kutoa huduma ya umeme Tanzania bara. Wakati huo huo ifahamike kwamba, TANESCO hununua umeme kutoka nchi jirani ambazo ni Uganda, Zambia na Kenya, na katika hali hii kwa namna yoyote ile, haliwezi kumuuzia mtu ama taasisi nyengine kwa hasara.

Lakini pia imeelezwa kwamba, TANESCO hununua umeme huo kwa nchi hizo bila hata ya kupunguziwa bei, na kwa kawaida kila nchi kati ya hizo, kuna chombo kinachodhibiti bei, ambacho kwa kawaida huwa na asilimia moja ya mauzo ya kila mwezi, ambayo kupatikana kwake kunatokana na kukatwa asilimia moja ya fedha hizo kupitia mapato ya Mashirika ya Umeme na hatimae huchangia kuendesha shughuli za Mamlaka hizo za kudhibiti bei. Kwa Tanzania bara, kuna chombo kiitwacho EWURA (Mamlaka ya Udhibiti wa Masuala ya Nishati na Maji, Tanzania), ambayo pamoja na majukumu mengine, ina dhima ya kudhibiti bei ya umeme unaosambazwa kwa wananchi na watumiaji mbali mbali nchini Tanzania. Na kwa maana hii, kuongozeka kwa bei ya Umeme dhidi ya ZECO, pia kunanasibishwa sana na udhibiti wa bei ya umeme kuanzia mwaka 2008, chini ya EWURA.

Kwa maana nyengine, kabla ya mwaka 2008, TANESCO ndio iliyokuwa inadhibiti bei ya umeme kwa wateja wake wote, ikiwa ni pamoja na Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO), lakini kuanzia mwaka 2008, suala la bei ya umeme kwa wateja wake, TANESCO ilitakiwa kutoa kiwango ambacho EWURA wamekiidhinisha, hali ambayo sio tu kulifanya Shirika hili la TANESCO kutoza bei iliyoidhinishwa na EWURA, lakini pia hulazimika kutoa asilimia moja ya mapato yake na kuipa EWURA, Mamlaka ambayo inategemea kujiendesha kupitia fedha hizo za asilimia moja, zinazotozwa kwa TANESCO na wateja wengine ama vyombo vilivyo chini ama katika mamlaka yake.

Katika kulisisitiza suala hili, Uongozi wa ZECO ukiwa pamoja na Uongozi wa TANESCO, waliieleza Kamati kwamba, kuanzia Januari 2008, bei ya umeme iliyokuwa inauzwa kwa ZECO ni Shilingi 34/- kwa Uniti (kWh); Shilingi 4,755/- kwa kVA na Shilingi 8,534/- kama 'Customer Service Charge. Kwa maana hii, maelezo ya Uongozi wa ZECO yalithibitisha kwamba, Shirika lao lilikuwa angalau linamudu kulipa gharama hizo za umeme kwa TANESCO, kwa kiwango kinachoridhisha. Na kwa wakati huo, ilielezwa kwamba, katika mwaka wa 2008 Shirika la Umeme la Zanzibar, lilikuwa linadaiwa Tsh. 1.871,545,517.70, wakati ambao EWURA bado haijakabidhiwa dhamana ya kusimamia bei husika kwa TANESCO.

Aidha, kuanzia mwezi wa Januari, 2011, bei ya umeme iliongozeka kwa wastani wa asilimia 18%. lakini kutokana na hali kuwa mbaya kila siku na mzigo wa madeni kuongozeka, na zaidi baada ya usimamizi wa EWURA, sasa deni hilo limeongezeka zaidi na kufikia Tsh. 22,767,047,816.06 na Kamati imethibitishiwa kwamba, deni hilo litaendelea kukua siku hadi siku kutokana na utaratibu wa malipo uliopo hivi sasa. Kwa mantiki hii, Kamati imeelezwa kwamba, baada ya kuwepo kwa shughuli za EWURA, ZECO hulazimika kulipia asilimia 3 (Tariff 3) na hii ni baada ya kutoa gharama za usambazaji (Cost of Distribution) ambazo ni asilimia 21.6. Ni sawa na kusema kwa utaratibu huu kwamba, bei ya umeme ilikuwa shilingi 65.86 kwa kWh; Shilingi 8,114.40 kwa kVA na Customer Service Charge ni Shilingi 10,146.00.

Vile vile kuna jambo la msingi kuhusiana na kuwepo na kuendelea kwa deni hilo. Kamati imeelezwa kwamba, kwa mujibu wa huduma ya umeme unaouzwa kwa ZECO, Shirika hili hulazimika kulipia takriban Bilion 3 kwa kila mwezi, wakati uwezo wa Shirika hili la Umeme la Zanzibar, ni kulipia Bilioni 1.6 tu, tena hulipia kwa awamu (Installments) mbili kwa mwezi. Aidha, Kamati imefahamishwa kwamba, makusanyo ya ZECO kwa malipo ya humua yote wanayoitoa Zanzibar, ni sawa na Bilioni 3 kwa kila mwezi, na ni hizo hizo wanazotakiwa kulipa kwa TANESCO kwa mwezi, kwa maana hii, iwapo ZECO wataamua kulipia deni wanalodaiwa na TANESCO, hawataweza kujiendesha.

Kutokana na hali hii, ndio maana ZECO hulipia Bilioni 1.6 (tena kwa kujitutumua), wakati ilitakiwa ilipie Bilioni zote 3. Hoja kubwa iliyoelezwa kwa

Kamati kuhusiana na suala hili, ni malipo makubwa (Tariff) inayotozwa kuanzia mwaka 2008, kiasi kikubwa cha hali hii kimesababishwa na EWURA. Madai haya yaliifanya Kamati kuona ipo haja ya kukutana na EWURA, ili kujiridhisha juu ya maelezo yaliyotolewa na Shirika la Umeme la Zanzibar na kuthibitishwa na Uongozi wa TANESCO, lakini kutokana na uchache wa muda, Kamati haikupata nafasi ya kukutana na Uongozi wa EWURA.

Hata hivyo, Kamati inakubaliana kwamba, Shirika la Umeme halina uwezo wa kulipa deni la TANESCO kwa ukamilifu wake, lakini pia hali hii, pamoja na mzigo wa lawama kutupiwa EWURA, Kamati inaamini kama ZECO wangelisimamia ipasavyo vyanzo vyake vya mapato, na kurekebisha kasoro nyingi za utendaji, kama tulivyozieleza hapo awali katika hadidu rejea zilizotangulia, basi isingelikuwa na mzigo wa deni kubwa kama ililonalo na kama ingelilazimika kuwa na deni hilo, basi ukubwa wake na athari zake kwa wananchi wa Zanzibar, zingelipungua sana.

6.3.0 Hatua zilizochukuliwa na Serikali kulipatia ufumbuzi deni la ZECO kwa TANESCO:

Wakati Kamati inafanya mahojiano na Mkurugenzi kuhusiana na hoja hii, ilifahamishwa kwamba, pamoja na deni linaloikabili Shirika la Umeme la Zanzibar, deni hilo lilikuwa kubwa zaidi hapo awali na hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ilifuatilia suala hili kwa kukaa pamoja na Wizara ya Nishati na Madini ya Tanzania, pamoja na Uongozi wa mashirika yote mawili, ZECO na TANESCO, Tarehe 27/01/2012, kwa ajili ya kuzungumzia namna gani deni hilo litashughulikiwa, lakini pia ilikuwa ni sehemu ya ZECO kuwasilisha malalamiko yao na kero zao, juu ya upatikanaji wa huduma ya Umeme kutoka kwa Kampuni ya TANESCO.

Kikao hicho kilichokuwa na ajenda kuu mbili, ambazo ni deni la Shirika la Umeme la Zanzibar kwa TANESCO na ajenda ya pili ilihusiana na Ongezeko la bei za umeme kwa Shirika hili la Umeme la Zanzibar (ZECO). Kikao hicho pia kilikusudia kuondosha kasoro zilizopo na mzozano wa siku nyingi, kilihimiza sana ushirikiano wa pamoja kwa Taasisi mbili hizi, huku kikijikita kufanya maamuzi yafuatayo, kama tunavyoyanukuu **(Kiambatanisho Nam 100)**:

- “ZECO wako tayari kulipa bei za umeme ambazo zinazingatia uhalisia wa kufikisha umeme Zanzibar kutoka ‘substation’ ya Ubungo- Dar es Salaam, kwa kutambua kwamba, laini ya umeme ya msongo wa kV 132 kutoka Ubungo hadi Ras Kilomoni, ni mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

- ZECO wanatambua gharama kubwa ya kufua umeme kwa kutumia mitambo ya dharura inayotumia mafuta katika kipindi cha mpito.

- TANESCO watafahamu kwa ufasaha gharama halisi za ufuaji umeme katika mfumo wa gridi ya Taifa kwenye ‘busbar’ ya Ubungo baada ya kufanyika ‘cost of service study’ chini ya usimamizi wa EWURA ambayo inatarajiwa kukamilika mwezi wa Julai, 2012.

- Katika kipindi cha mpito, imekubalika kwamba ZECO watalipa bei za umeme zilizoidhinishwa na EWURA tarehe 1, Januari 2010 na tarehe 15 Januari, 2012 baada ya kutoa gharama za usambazaji (distribution costs) ya asilimia 21.6. Hii itafanya bei ya umeme kwa mwaka 2010 hadi tarehe 14 Januari, 2012 kuwa Tsh. 65/kWh badala ya Tsh. 84/kWh na kuanzia tarehe 15 Januari 2012 zitakuwa Tsh. 92/kWh badala ya Tsh. 118/kWh iliyotangazwa kwa mujibu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Masuala ya Nishati na Maji (EWURA). Tofauti inayotokana na malipo hayo, Serikali ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Nishati na Madini itakuwa inailipa TANESCO hadi hapo ‘cost of service study’ itakapokamilika na kutoa gharama halisi ya kusambaza umeme kwa ZECO.

- Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO na Meneja Mkuu wa ZECO wataandaa mchanganuo wa deni linalodaiwa na kuwasilisha Serikalini kwa kuonesha kiwango kinachodaiwa. Aidha, gharama za uwekezaji wa Ras Kilomoni zifanyiwe kazi chini ya usimamizi wa Makatibu Wakuu husika, na

- Baada ya makubaliano hayo, ZECO wapo tayari kutoa mapendekezo kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu nyongeza ya bei ya umeme".

6.4.0 Deni halisi linalodaiwa kwa ZECO:

Baada ya kufuatilia maelezo ya hapo juu, ni wazi kwamba, kila mtu atakuwa na hamu ya kufahamu deni halisi lililokuwa linadaiwa kwa Shirika la Umeme la Zanzibar, na kufuatia suala hili kuulizwa kwa Uongozi wa pande zote mbili, Kamati ilifahamishwa kwamba, kabla ya kufanyika kwa kikao cha pamoja baina ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Wizara ya Nishati na Madini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Shirika la Umeme la Zanzibar lilikuwa na deni la Tsh. Bilioni 62.37, lakini kutokana na mazungumzo hayo, iliwafikiwa kwamba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano italipa tofauti ya Tsh. 39 bilioni Nukta 7 (39,719,620,794.42) huku deni linalobakia, yaani Bilioni 22 (22,654,923,389.22) litaendelea kuwa chini ya ZECO.

Aidha, imeelezwa kwamba, ili deni hilo la Bilioni 22 kuweza kulipwa, mchanganuo uliokubalika ni pamoja na ZECO kutakiwa kulipa Tsh. 5,067,297,860.18 kwa deni linaloanzia mwezi wa Januari 2008, hadi Disemba 31, ya mwaka 2010. Sambamba na hili, pia walitakiwa kulipa kwa kipindi kilichoanzia Januari 1, 2011 hadi Januari 14, 2012 jumla ya Tsh. 17,587,625,529.04.

Pamoja na ufafanuzi huo hapo juu, kuhusu kima halisi cha malipo ya TANESCO ambayo ni dhima ya ZECO kuhakikisha kinalipwa, Kamati imefahamishwa kwamba, mwelekeo wa malipo hayo utapatikana mara tu baada ya EWURA watakapokamilisha tathmini ya gharama. Hii ni kwa sababu, mpaka Kamati inafika kuifanyia kazi hadidu hii rejea, EWURA bado hawajakamilisha kufanya tathmini halisi ya TANESCO, ili kujua namna gani wateja wake, ikiwa ni pamoja na ZECO watalazimika kulipia gharama ya umeme kwa mnasaba wa mabadiliko yaliyokusudiwa.

Hata hivyo, Kamati ilifahamishwa kwamba, kwa matarajio ya ZECO, tathmini hiyo ilitarajiwa iihusishe kwa ukamilifu wake kwa mnasaba wa hoja kwamba, Shirika la Umeme la Zanzibar linatofautiana sana na wateja wengine wa TANESCO, lakini pia, haja ya kufanyika kwa tathmini hiyo imetokana na

mgogoro wa muda mrefu, unaohusiana na uhalali wa bei ya umeme baina ya ZECO na TANESCO. Hivyo basi, kwa namna yoyote ile iwayo, EWURA wanalazimika kukutana na Uongozi wa ZECO, ili utoe maelezo yao ya kina kuhusiana na suala zima la huduma ya umeme wanayoipata kutoka TANESCO.

Kwa maana nyengine, EWURA wametafuta Mshauri Mwelekezi, mwenye dhamana ya kufanya utafiti kamili juu ya mapato yanayotokana na TANESCO na hatimae aishauri EWURA juu ya njia bora za kutumika kuhakikisha mapato hayo yanapatikana kwa wakati na kwa manufaa ya Taifa. Katika kufanya utafiti huo, Mshauri Mwelekezi amekutana na TANESCO mara kadhaa na kupata idadi halisi ya wateja wake wanaopata huduma za umeme, lakini kwa bahati mbaya, pamoja na umuhimu wake, Mshauri huyu Mwelekezi, bado hajakutana na Uongozi wa ZECO, ili nao ukatoa maelezo yao kuhusiana na kazi waliyopewa.

6.5.0 Athari za Deni hilo kwa Maslahi ya Zanzibar:

Kwa ujumla wake inaaminika na kukubalika kwamba, deni hilo lina athari kubwa kwa Zanzibar, za kiuchumi, kisiasa pamoja na kijamii. Kamati ilielezwa hoja hii kwa mnasaba wa Mtumiaji wa mwisho (End User), maelezo haya pia yalisisitizwa kwa kutolewa mfano wa Kampuni za biashara zinazomilikiwa na Mfanya biashara maarufu nchini, Ndg. Salum Bakhressa, ambazo kwa kawaida baadhi yao hupatikana sehemu zote za Jamhuri ya Muungano, kwamba, zinapokuwa Tanzania bara, zinatozwa na kulipia gharama za umeme kwa thamani ya ‘Unit’ moja kwa Tsh. 118 wakati huo huo zinazofanyakazi Zanzibar, hutozwa kwa gharama ya kila ‘Unit’ kwa Tsh. 210. Hii ina maana kwamba, ukichukua gharama za umeme pekee, ni wazi kwamba, wafanya biashara watakimbilia kufanya biashara na kuanzisha viwanda vikubwa nchini Tanzania bara, huku wakiikimbia Zanzibar kwa sababu ya gharama kubwa za umeme.

Sambamba na hilo, miongoni mwa athari za wazi wazi ni pamoja na mzigo mzito wa gharama za umeme unaowakabili wananchi wa Zanzibar, kutokana na kulazimika kulipia umeme kwa gharama ya juu, huku uwezo wa wananchi walio wengi ni mdogo na kipato chao hakilingani na gharama za umeme wanazolipa kwa ZECO. Suala hili liko wazi, kwamba, mara nyingi husababishwa na ongezeko la gharama za umeme kwa upande wa ZECO, ambapo pia hulazimika kwa namna

yoyote ile kuwauzia wananchi kwa gharama ya juu zaidi, ili waweze kujiendesha kwa faida na kuendeleza uhai wa Shirika.

6.6.0 Muhtasari wa Mambo yaliyobainika na Kamati kufuatia Uchunguzi wake wa Hadidu hii Rejea:

i. Shirika la Umeme la Zanzibar hadi mwezi Juni 2012 lilikuwa linadaiwa Tsh.22,767,047,816.06/- na TANESCO.

ii. Shirika linashindwa kulipa deni linalodaiwa na hii pia inatokana na kuwepo kwa Uongozi unaoshindwa kusimamia ipasavyo mapato halisi ya Shirika.

iii. Deni linalodaiwa Shirika la Umeme lina athari kubwa za kiuchumi kwa wananchi na nchi ya Zanzibar.

SEHEMU YA TATU:

7.0.0 HITIMISHO:

Kwa kawaida katika muongozo wa namna gani Kamati za Baraza zingelimalizia uandishi na uwasilishaji wa ripoti yake, kama ilivyoelekezwa na kanuni ya 121(5) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, ni kuzungumzia katika sehemu ya tatu ya ripoti husika, Hitimisho ama muhtasari wa mambo ikiwa ni pamoja na mapendekezo ya Kamati juu ya kazi waliyokwishaifanya. Kabla ya kutoa mapendekezo ya Kamati hii, ni vyema kumpongeza Mhe. Spika na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa maamuzi yao ya kuipa kazi maamulu (yenye hadhi sawa na Kamati Teule), Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (P.A.C), jambo hili ni la kihistoria kwa Kamati ya P.AC ya Baraza, mbali na zile kazi zake za kila siku, kama zinavyoelezwa katika Kanuni ya 118(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2012, leo inahitimisha kazi maalum ya kuchunguza utendaji wa Shirika la Umeme, tunashukuru na kupongeza hatua hii.

Ni wazi kwamba, kazi hiyo iliyohitaji utaalaumu wa kina katika kuchunguza na hatimae kutoa ripoti ya Shirika la Umeme la Zanzibar, inaashiria wazi kwamba, Wajumbe wa Kamati hii wamefainikiwa kwa kiasi kikubwa kueleza walichokigundua katika uchunguzi wao, aidha, ni vyema pia tukafahamu kwamba, haikuwa rahisi hata kidogo kuifanya kazi hii, ukizingatia ukweli kwamba, Shirika hili linafanya kazi ya kitaalamu na pasipo kutoa ushirikiano wao wa dhati kwa Kamati, hali ya ugumu wa kupatikana taarifa sahihi pamoja na namna ya kuzitolea ripoti, ingeliikwaza Kamati. Tunapenda tutoe shukurani zetu kwa Watendaji na Viongozi wote wa Shirika, waliotoa mashirikiano yao kwa Kamati, na zaidi kwa zile Taasisi zilizohusika na kazi za Shirika, ikiwa ni pamoja na Uongozi wa Kampuni ya Mantrac ya Dar es Salaam na Shirika la TANESCO, na taasisi nyengine zilizohusika.

Pamoja na pongezi hizo, Kamati haitaacha kusema kuhusiana na baadhi ya Watendaji ikiwa ni pamoja na Meneja Mkuu wa Shirika, kwa baadhi ya wakati kutotoa mashirikiano yao ya dhati kwa Kamati na hata kujaribu kuficha ukweli, kwa lengo la kuifanya Kamati ishindwe kutimiza wajibu wake. Tunapenda

kuwakumbusha kwamba, maamuzi ya Baraza la Wawakilishi, kuipa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika, kazi maalum ya kuchunguza utendaji wa Shirika la Umeme, badala ya kuunda Kamati Teule, haikuwa na maana ya kutaka kuukomoa Uongozi wa Shirika ama kutoa hujuma na hutuma dhidi ya Shirika lenyewe.

Kwa ujumla wake, kazi hii kukabidhiwa kwa Kamati hii, imefanywa kwa nia njema na kuisaidia Serikali pamoja na Shirika lenyewe katika utekelezaji wa majukumu yake, ili lile lengo la kuanzishwa na kuwepo kwake liweze kuinufaisha nchi hii, lakini zaidi kuwa fanisi katika kutoa huduma zake kwa wananchi. Haitakuwa pia uungwana kwa Kamati kuacha kuwaomba radhi watendaji wa Shirika na Uongozi wake, iwapo kulitokezea kukwaruzana na Wajumbe ama Sekretarieti ya Kamati. Tunafahamu kwamba, Zanzibar ni ndogo na takriban watu wake ni ndugu, na inapotokezea kazi kama hizi za kiuchunguzi kwa lengo la kuwasaidia wananchi wetu, kujuana huku ama muhali kwa namna yoyote hulazimika kuwekwa pembeni, ili ukweli uweze kuchukua nafasi yake.

Kamati inaendelea kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru zaidi wananchi mbali mbali wasiokuwa wafanyakazi wa Shirika ambao waliotembelewa na Kamati na kutoa mashirikiano yao mazuri kwa kueleza taarifa za kweli ambazo zimeisaidia sana Kamati kukamilisha kazi yake. Sambamba na hili, Kamati pia inawashukuru Viongozi wa Bodi ya Wakurugenzi, Tume ya Utumishi Serikalini, Shirika la Utangazaji la Zanzibar na wengine, kwa mashirikiano yao mazuri waliyoyatoa pale walipoitwa na Kamati na kwa utaratibu mwengine uliotumiwa na Kamati kupata taarifa ilizozihitaji, kwa ujumla Kamati inawapongeza na kuwashukuru.

Kamati inashukuru kumaliza kwa salama kazi hii nzito iliyotumwa kuifanya huku ikifahamu kwamba, Serikali, Shirika la Umeme la Zanzibar na zaidi kwa Bodi mpya ya Wakurugenzi iliyoteuliwa mwaka uliopita, wataifanya ripoti hii sawa na kioo cha kujitizamia na kuona kasoro ziko wapi, lakini msisitizo wa Kamati unaelekezwa kwa Serikali kuwa jasiri katika kufanya maamuzi magumu ya kuondosha na kutokomeza kabisa, mapungufu yote yaliyoelezwa wazi katika ripoti hii, bila ya kuwa na muhali kwa maslahi ya nchi na wananchi wake. Si vyema

kuendelea kuficha uovi wa wachache, huku madhara yake yakaendelea kuisakama na kuihujumu nchi na wananchi.

Kamati inaamini kwamba, Ripoti hii ni kisima cha elimu na hekima kisichokauka milele iwapo itafanyiwa kazi, na ni sawa na kidonda kisichopoa milele iwapo Serikali bado itaendeleza kile wananchi wanachokiita 'Kulindana' kwa maslahi ya wachache. Kwa Ripoti hii, Baraza linaendelea kutekeleza vyema majukumu yake ya kusimamia maslahi ya wananchi, na ni Ripoti itakayosaidia sana elimu na maarifa ya wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, lakini wasomaji wanaoutumia muda wao mwingi kujisomea taarifa mbali mbali za Baraza na Mabunge mengine, wamepata rejea itakayotosheleza kiu zao. Kwa kupitia ripoti hii, mambo mbali mbali ambayo kwa muda mrefu ilikuwa ni kilio kwa wananchi dhidi ya utendaji wa Shirika, yamewekwa wazi na kufahamika na hivyo, upeo wa wananchi hao na uelewa wa yepi yanayofanyika katika Shirika, kwa kuisoma ripoti hii yatafikia matilaba.

Kubwa zaidi, baada ya maelezo yote hayo ni kwamba, Kamati itatoa mapendekezo yake kwa mtindo wa kujumuisha hadidu rejea zote zilizohusika na kufanyiwa kazi, na utaratibu huu unaelekezwa na kanuni ya 121(5) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2012, ingawaje haujazoeleka katika Ripoti za Kamati hii ya P.A.C, na ripoti nyengine za Baraza, ambazo hueleza mapendekezo yao katika sehemu ya Maudhui ya ripoti, lakini kwa kukidhi masharti ya kanuni hii, mapendekezo hayo hufanyiwa muhtasari wake katika sehemu ya Hitimisho. Kwa Ripoti hii, Mapendekezo ya kazi ya Uchunguzi kuhusu Utendaji wa Shirika la Umeme kwa mnasaba wa hadidu rejea zilizokabidhiwa kwa Kamati, yataelezwa katika sehemu hii ya Hitimisho kama kanuni inavyoelekeza moja kwa moja katika fasiri yake.

Tumefanya hivyo kwa lengo la kuipa wepesi Serikali kutekeleza mapendekezo machache watakayoweza kuyatekeleza kwa ufanisi, ili ile sababu ya uzito wa utekelezaji wake, isiendelee kuelezwa, kwani sio tu huidhalilisha kwa kuonekana haiko makini katika dhamira yake ya kupiga vita dhidi ya matumizi mabaya ya fedha za umma na matumizi mabaya ya madaraka kwa baadhi ya watendaji wa Taasisi na Mashirika yake, ambapo katika lugha nyepesi ya kileo huitwa

‘UFISADI’, lakini wananchi wa nchi hii na zaidi wale wanaofuatilia kwa makini shughuli za Baraza, hupoteza imani na mapenzi kwa Serikali yao, jambo ambalo haliridhishi na linahitaji kuondoshwa kwa umakini wa kutekeleza mapendekezo ya Kamati za Baraza lakini pale yanaporidhiwa hugeuka na kuwa maagizo ya Baraza la Wawakilishi.

7.1.0 MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSIANA NA HADIDU REJEA ZILIZOHUSIKA:

Kwa mnasaba wa maelezo ya hapo juu, Kamati inatoa mapendekezo yafuatayo kwa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ili iiagize Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na kuitaka itekeleze mambo yafuatayo:

1. Viongozi wa Bodi ya Wakurugenzi waliomaliza muda wao 2012, misisitizo ukiwekwa kwa aliekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Ndg. Moh’d Hashim Ismail, wachukuliwe hatua za kisheria kwa kuliingizia Shirika hasara zisizo za lazima, (Tsh.31,179,000/-) kwa malipo ya faini kwa Kampuni ya Kichina (China Railway Jianchang Engeneering Co. (T) Ltd (CRJE), ambapo hasara hii imesababishwa na uzembe na ubinafsi wa aliekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Wajumbe wote wa Bodi hii kwa ujumla.

2. Menejimenti ya Shirika la Umeme ichukuliwe hatua za kinidhamu, kwa uzembe wa kutosimamia ipasavyo majukumu ya Shirika, kuleta migogoro miongoni mwa wafanyakazi wake, kushindwa kulisimamia Shirika, Shirika kupoteza mapato yake, kujenga mazingira ya upendeleo yenye kuleta ubaguzi katika kazi na kupunguza ufanisi katika utendaji wa Shirika la Umeme kwa ujumla.

3. Wafanyakazi wote wa Shirika waliotajwa kuhusika moja kwa moja ama kwa namna yoyote ile katika ripoti hii, pamoja na Watendaji wa Serikali waliokuwa sio waajiriwa wa Shirika ikiwa ni pamoja na Mkurugenzi wa Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC-TV) alieruhusu Kampuni ya Zanzibar Data Com kutumia umeme kinyume na taratibu na Sheria, wachukuliwe hatua za kinidhamu na kisheria kutokana na kuhusika kwao katika kulihujumu Shirika kwa njia yoyote ile.

4. Serikali ipige marufuku na isimamie kwa udhati Kampuni zote binafsi, ikiwa ni pamoja na Kampuni ya GECCO kufutiwa vibali (ambavyo Kamati inaamini vimetoka kinyume na Sheria ama kwa namna yoyote iliyo), na badala yake kazi zinazohusiana na utoaji wa huduma ya umeme ziendelee kufanywa na Shirika la Umeme pekee, kama Sheria Nam 3 ya mwaka 2006, inavyoelekeza.

5. Watendaji wa Shirika ambao pia ni wafanyakazi ama wamiliki wa Kampuni ya GECCO (pamoja na wafanyakazi wa Shirika wanaosaidia kazi za GECCO) kama walivyotajwa moja kwa moja ama kwa utaratibu wowote katika ripoti hii, wachukuliwe hatua za kinidhamu kwa kudhoofisha utendaji kazi na ufanisi wa Shirika.

6. Kwa kuwa uendeshaji wa majenereta 32 umekuwa ni mzigo mkubwa kwa Shirika, Serikali ama ichangie ruzuku katika Uendeshaji wake, au kutafutwe utaalamu utakaowezesha majenereta hayo kutumia diseli ya kawaida iyenye gharama nafuu au yauzwe na badala yake yatafutwe mengine kwa mujibu wa Sheria, yatakayoweza kutumika kama inavyokusudiwa.

7. Kwa kuwa Kamati imepata wasi wasi kwamba kuna hujuma imefanyika iliyopelekea kukosekana kwa umeme Unguja ndani ya miezi mitatu 2009/2010, Serikali, ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kuwasilishwa ripoti hii, iunde Tume iliyohuru ya Kuchunguza chanzo na sababu zilizopekea kukosekana kwa umeme huo na ripoti yake iwasilishwe na kujadiliwa katika Baraza la Wawakilishi.

8. Kwa kuzingatia matakwa ya Katiba, Serikali, kupitia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar, ifanye ukaguzi wa fedha zilizotumika kurejesha huduma ya Umeme, Unguja baada ya kuzimika na kukosekana kwa kipindi cha miezi mitatu (Disemba hadi Machi, 2010).

9. Bila ya kuathiri masharti ya Katiba, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ifanye ukaguzi maalum wa Hesabu za Shirika kwa kipindi cha miaka mitatu (2009-2012).

10. Kwa kuwa Zanzibar hakuna chombo kinachoratibu bei ya umeme, kama vile EWURA kule Tanzania bara, na kwa kuwa ZECO hujipangia bei kwa matakwa ya EWURA, Serikali ilete Sheria ya kuanzisha chombo

kitakachohusika na kudhibiti bei ya umeme Zanzibar, ambapo pamoja na majukumu yake mengine, kitashauriana kwa karibu na EWURA ili ZECO iweze kutoa huduma bora na fanisi na kupatikana kwa muafaka wa bei ya umeme Zanzibar.

11. Kwa kuwa moja kati ya dosari kubwa ya deni la umeme inalodaiwa ZECO na TANESCO inatokana na Zanzibar kukosa umeme wake, na kwa kuwa katika hili wananchi wa kawaida ndio wanaoumia na kuathirika zaidi, Serikali ihakikishe Zanzibar inazalisha umeme wake wenyewe na sio kuendelea kutegemea umeme kutoka Tanzania bara.

Baada ya kueleza mapendekezo ya Kamati, Kamati inapendekeza zaidi kwa manufaa ya wananchi wetu kwamba ripoti hii baada ya kupitishwa Barazani, iwe rahisi na rafiki kwa kila mtu anaeihitaji. Kwa maana, isiuzwe lakini iwe inatolewa bure na kila anaetaka afike katika Afisi ya Baraza la Wawakilishi ili aweze kuipata angalau kwa njia ya ‘soft copy’. Aidha, kwa kuwa Baraza la Wawakilishi lina tovuti yake (web site), tunapendekeza ripoti hii iwekwe katika web site hiyo, na iwekwe katika hali ya kuhifadhiwa isiharibiwe wala kuandikwa chochote (auditing), lakini iwekwe katika hali ya kuwezekana kupatikana (down loading) kwa kila mtumiaji wa tovuti hiyo kwa njia ya urahisi kabisa.

Tunazidi kupendekeza kwamba, ripoti hii na ibakie katika Maktaba ya Afisi ya Baraza la Wawakilishi, ili iwe rahisi kwa kila mtumiaji wa maktaba hiyo kuipata ripoti hii kwa wepesi, igawaje pia kwa kuzingatia masharti na taratibu za maktaba zilizowekwa. **Mwisho kabisa na kwa msisitizo wa kipekee, Kamati inaliomba Baraza hili tukufu liitake Serikali iyatekeleze mapendekezo ya ripoti hii ndani ya miezi 3 kutoka tarehe ya kuwasilishwa kwa ripoti hii na hatimae Serikali iwasilishe taarifa ya utekelezaji wake katika Baraza hili tukufu.**

Imesainiwa na kuthibitishwa na

Mhe. Omar Ali Shehe,
Mwenyekiti,
Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika,
Baraza la Wawakilishi,

Zanzibar.